

BUNGE LA TANZANIA

---

MAJADILIANO YA BUNGE

---

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Nne – Tarehe 1 Februari, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Asalaam  
alleykum! Amani ya Bwana iwe nanyi! Heri ya mwaka  
mpya! Katibu tuendelee.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 40

**Ukamilishaji wa Ujenzi wa Zahanati ya Nalasi**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA** aliuliza:-

Zahanati ya Nalasi katika kijiji cha Nalasi, Jimbo la Tunduru Kusini, iliishapandishwa hadhi kuwa Kituo cha Afya kuanzia mwaka 2010 kufuatia ahadi aliyoitao Mheshimiwa Rais kwa wananchi:-

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa ujenzi wa kituo cha afya?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa nguvu za wananchi kufyatua matofali zaidi ya 300,000 ilihali utekelezaji wa agizo hilo unachelewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mnamo tarehe 12 Oktoba, 2010 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa katika ziara wilayani Tunduru aliahidi kufanya upanuzi wa Zahanati ya Nalasi iliyopo katika Kata ya Nalasi, kuwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais, Halmashauri katika mwaka wa fedha 2012/2013 iliwasilisha maombi maalum kwa Wizara ya Fedha ili kupata shilingi bilioni 2.4 zinazohitajika kujenga

majengo 12 na nyumba 14 za Watumishi katika kituo hicho lakini hazikupatikana.

Aidha, katika Bajeti ijayo ya mwaka 2013/2014 Halmashauri imewasilisha tena maombi maalum ya shilingi bilioni 2.75 ili kutimiza azma ya upanuzi wa miundombinu ya Zahanati ya Nalasi kama ilivyoagizwa na Mheshimiwa Rais. Majengo yatakayojengwa ni pamoja na jengo la ushauri (*Consultation Block*); wodi ya kulaza wagonjwa; huduma za *HIV/AIDS*; Maabara; Uzazi, Upasuaji; Matibabu; Jiko na Stoo. Pia jengo la kuhifadhi maiti; huduma za Mama na Mtoto na jengo la Nishati (*Power House*).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawapongeza wananchi wa eneo hilo waliochangia nguvu zao kwa kufyatua matofali 300,000 kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati hiyo.

Aidha, ni azma ya Serikali kuhakikisha agizo la Mheshimiwa Rais linatekelezwa na ujenzi huo unakamilika kwa wakati. Hivyo, fedha zilizoombwa zitakapopatikana ujenzi huo utakamilishwa ili kutowavunja wananchi moyo ambao wamechangia nguvu kazi kuwezesha ujenzi wa kituo hicho. (*Makofi*)

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ambayo yanatia moyo kwa wananchi wa Nalasi. Lakini pamoja na shukrani hizo naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali yetu ni moja na kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Waziri yameeleza kwamba maombi haya maalum ya fedha yamepelekwa Wizara ya Fedha na hivi ninavyozungumza Waziri wa Fedha yupo hapa hapa ndani.

Je, Waziri huyu anasemaje juu ya maombi haya ya wananchi wa Nalasi katika kutekeleza agizo hili la Mheshimiwa Rais? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa swali hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kwanza Bajeti inayoidhinishwa hapa Bungeni ndiyo tunayoitumia. Inapotokea kwamba kuna mahitaji ya dharura wakati mwingi uwezekano wa kuyakabili ni fungu lenyewe, lakini inapotokea fungu lenyewe limekuwa dogo kuliko mahitaji basi tunatakiwa tusubiri Bajeti nyingine na hali hivyo ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Na. 41

**Upimaji wa Maeneo Ubungo**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka katika mwaka wa 2012/2013 kuhusu maeneo ambayo hayajapimwa katika Kata za Jimbo la Ubungo ili kuепusha kuendelezwa kiholela?

(b) Je, ni lini uendelezaji wa Mji wa Luguruni (*Satellite Town*) na eneo la Kwembe Kati utafanyika ili kuепusha maeneo hayo kuendelea kuwa mapori na kuibuka kwa migogoro mipya ya ardhi katika Kata za Kibamba na Kwembe?

(c) Je, ni mfumo gani umewekwa wa kupunguza gharama za upimaji wa ardhi na kuharakisha upatikanaji wa Leseni za Makazi na Hati za Ardhi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa John J. Mnyika, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na ( c ) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza kutambua maeneo yaliyojengwa bila kupangwa na kupimwa kwa kutayarisha na kutoa leseni za makazi katika Jiji la Dar es Salaam mwaka 2004 kwa majaribio. Katika kutekeleza

maelekezo ya Sera ya Maendeleo ya Makazi na llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010 mwaka 2011/2012 Serikali kupitia Wizara yangu ilianda Programu ya Taifa ya Kurasimisha na Kuzuia Ujenzi Holela Mijini ya mwaka 2013 – 2022 ambayo itatekelezwa kwa muda wa miaka kumi kuanzia mwaka huu wa 2013.

Utekelezaji wa majaribio (*Pilot Project*) ulianza katika Majiji ya Mwanza na Dar es Salaam. Katika jimbo la Ubungo kasi ya urasimishaji ilianza katika Kata za Mbezi na Msigani kwa kufanya uhakiki. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imetangaza Kata za Manzese na Tandale kuwa eneo la mpango (*redevelopment area*) ambalo litaendelezwa upya kwa kujenga nyumba za ghorofa ili ardhi ya maeneo hayo itumike kikamilifu kwa mujibu wa maelekezo ya Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 haitawezekana maeneo yote ambayo hayajapimwa katika Jimbo la Ubungo kupimwa kwa sababu Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni yenye wajibu wa kutekeleza mpango wa uendelezaji wa maeneo hayo haikutenga fedha za kutosha.

Hivyo, Halmashauri hiyo inashauriwa kutenga fedha katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 kwa ajili ya kuanza kutekeleza Programu ya Taifa ya Kurasimisha na Kuzuia Ujenzi Holela Mijini. Watakapokuwa tayari Serikali kupitia Wizara yangu na MKURABITA itasaidia pale ambapo kutakuwa na mahitaji ya vifaa na wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu namwomba Mheshimiwa Mbunge wa Ubungo kwa kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani wote wa jimbo la Ubungo kuhimiza wananchi wenyewe maeneo hayo kuchangia gharama za upimaji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikwishaanza utekelezaji wa uendelezaji wa Kituo cha Luguruni na Kwembe katika Jiji la Dar es Salaam. Kazi zilizotekelizwa ni pamoja na uthamini wa mali pamoja na ardhi, ulipaji fidia, upimaji na ugawaji wa viwanja.

Zabuni ya kumpata mwendelezaji mwenza (*Core Master Developer*) ilitangazwa mwezi Mei, 2010. Baada ya kuchambua maombi ya makampuni na taasisi zilizoonesha nia ya kushiriki kuendeleza eneo hilo Serikali illiliteua Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) kuwa mwendelezaji mwenza wa eneo hilo. Hivi sasa Wizara yangu inakamilisha taratibu za kisheria za makabidhiano ya Shirika la Nyumba la Taifa na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka huu wa 2013 ambapo utekelezaji utafanyika kwa kushirikiana na sekta binafsi (*Public Private Partnership (PPP)*).

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza mradi wa uwekaji wa mtandao wa alama za upimaji (*National Geodetic Network*). Hadi Januari, 2013 jumla ya alama 1,000 zimesimikwa nchini kote kwa lengo la kurahisisha upimaji ardhi nchini.

Pia, Serikali inatafuta fedha za kujenga kituo cha kupokelea picha za *satellite* (*Direct Receiving Station*) kitakachorahisisha upimaji ardhi nchini. Lengo la mipango hiyo ni kupunguza gharama za upimaji ili Watanzania waweze kupata hati za kumiliki ardhi kwa haraka na kwa gharama nafuu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. Rai ya Mheshimiwa Naibu Waziri ya kuwahimiza wananchi kimsingi tumekuwa tukiitekeleza na wananchi wamekuwa wakichangia, lakini malalamiko yao makubwa ni kwamba wanalipia wanachelewa kupata leseni na hati kwa muda mrefu sana. Sasa nina swali la kwanza kwamba:-

(i) Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwa jukumu hili kimsingi ni la Manispaa ya Kinondoni, lakini Dar es Salaam ina upekee wake kuhusiana na matatizo ya kufumuka kwa makazi holela. Kasi ya ongezeko la makazi holela yasiyopimwa Dar es Salaam ni asilimia sabini (70%), zaidi ya wastani wa kitaifa wa asilimia thelathini (30%) wa miji na majiji mengine.

Katika mazingira haya na kwa kuwa Serikali Kuu inaingia hasara kubwa sana kwenye ulipaji wa fidia ya miradi mikubwa ya maji na barabara kutokana na ujenzi holela, ni kwa nini Serikali Kuu haioni umuhimu wa kuiongezea nguvu Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ili kulimaliza hili tatizo mapema zaidi?

(j) Nashukuru kwamba jitihada zinaanza za kupunguza gharama za Hati na masuala ya leseni. Lakini je, ni lini hasa Serikali inatarajia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya uwekaji wa alama pamoja na ujenzi wa kituo cha kupokea picha za *satellite* ili mzigo huu wa gharama kwa wananchi nchi nzima wa leseni na Hati uweze kupungua?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa John J. Mnyika, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu ombi kwamba Serikali Kuu iongezee nguvu Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni napenda kutoa taarifa ifuatayo kwa Bunge lako Tukufu. Katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 Serikali Kuu inasaidia Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kutekeleza Mradi wa *Community Infrastructure Upgrading Project* ambao sasa hivi unatekelezwa kuitia fedha zinazotokana na msaada wa Benki ya Dunia na kwa mwaka huu wa fedha wamepatiwa shilingi 528,995,626/=. Hivyo huo ni msaada ambao Serikali Kuu imetoa kwa Halmashauri. Serikali itaendelea kutoa msaada pale ambapo uwezo wa Serikali Kuu nao utaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kituo cha kupokelea picha za *satellite* (*satellite receiving station*) ambacho kilipaswa kijengwe hapa Dodoma, mchakato wa zabuni uliishaanza lakini kutokana na miradi ya kipaumbele ambayo iliingizwa katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa

wa Miaka Mitano, ndiyo sababu fedha za kujenga kituo hiki hazikuweza kupatikana kwa wakati.

Lakini Serikali ina nia njema na tunayo matumaini makubwa kwamba ikiwa mapato ya Serikali yataongezeka katika mwaka huu na hasa yale ya kodi za ardhi na nyinginezo, basi ujenzi wa kituo hiki utafanyika katika kipindi kifupi kijacho.

Kwa hivyo, natoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge wa Ubungo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu tushirikiane kuhimiza wananchi walipe kodi ya ardhi kwa sababu tukipata kodi ile kwanza asilimia thelathini (30%) tunairudisha kwenye Halmashauri inayohusika na zinazobaki ndiyo tunatumia kutekeleza miradi hii ya Maendeleo ya Ardhi.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la kwanza alizungumzia habari za Serikali kufanya jitihada za kupunguza gharama za upimaji wa viwanja. Hivi sasa zipo taarifa za kupanda kwa gharama za kupima viwanja kutoka shilingi laki moja na kitu mpaka shilingi milioni moja. Nataka kufahamu.

Je, habari hizi ni za kweli? Kama ni za kweli, ni vigezo gani vimetumika kupandisha gharama kufikia kiwango hicho ambacho ni mzigo kwa wananchi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kibona, Mbunge wa lleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulipokuwa tukiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu tuliwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba, gharama halisi za kupima kiwanja kimoja ni shilingi 50,000/= siyo 100,000/= Lakini tulieleza pia kwamba ili uweze kupata bei au gharama iwe hiyo, ni lazima tukubaliane tupime eneo moja kwa mara moja. Ili kupata *the benefit of what we call the economies of scale*. Ni lazima tupime eneo moja kwa mara moja.

Kwa mfano, kama mtaa mzima tukisema kwamba tunaupima kwa mara moja gharama itakuwa hiyo, lakini kama ni mtu mmoja mmoja inaweza ikafika hadi hiyo shilingi 100,000/=. Lakini hiyo shilingi millioni moja (1,000,000/+) ndiyo naisikia leo, si gharama ambayo iko katika malipo yetu na kwa hivyo labda baadaye nitaonana na Mheshimiwa Kibona ili aweze kutueleza hiyo taarifa imepatikanaje tuweze kufuutilia na kuifanyia kazi. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tuhamie Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Lakini naomba kabla hujaniruhusu kuuliza swali langu nitoe neno la pole. Jana tarehe 31 Januari, 2013 ilitokea ajali ya boti ya mbao ambayo inajulikana kwa jina la *Sunrise* iliyokuwa inatoka mkoani Tanga kwa kupitia Bandari ya Pangani kuelekea Nungwi. Boti hiyo ilizama ikiwa imebeba abiria 32. Kwa taarifa niliyopata rasmi abiria 21 wameokolewa na abiria waliobakia hawajulikani walipo.

Vijana wangu wa Nungwi ambao walishiriki katika uokozi huo wameniletea taarifa kwamba wamefanikiwa kuiokoa boti hiyo na wameipeleka Nungwi katika bandari ya Kendwa. Abiria wote waliookolewa wamesalimika wakiwa salama na wamepelekwa katika hospitali ya Kivunge. Kwa hivyo...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa swali.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba swali langu Na. 42 lipatiwe majibu.

Na. 42

**Ugonjwa wa Moyo kwa Wachezaji**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani kwa wachezaji wetu juu ya ugonjwa wa moyo ambao ni tishio kubwa kwa maisha yao.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali haina mpango maalum kwa wachezaji juu ya ugonjwa wa Moyo. Wachezaji karibu wote humiliikiwa na vilabu vyao na kupata huduma ya vipimo, kinga na tiba kupitia Madaktari wa klabu zao.

Aidha, Wizara yangu inasisitiza wanamichezo wote kupata ushauri wa kitaalam katika hospital za Wilaya, Mikoa na Hospitali za Rufaa kila wanapohisi kuwepo dalili za matatizo ya moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wizara yangu itaendelea kufanya jitihada za kuimarisha kitengo cha Tiba na Kinga kwa wanamichezo ili kuendelea kutoa

nasaha, elimu, ushauri na pia kushughulikia matatizo ya magonjwa ya moyo kwa wachezaji kila yanapojoitokeza na kuhimiza wanamichezo kuwa na tabia ya kupima afya zao mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kukujulisha kuwa Michezo na matukio yote yanayofanywa Uwanja wa Taifa, utaratibu umewekwa kuhakikisha kuwa gari la Huduma ya Kwanza la Muhimbili lenye vifaa vyote vinavyohitajika kwa Tiba ya dharura linakuwepo.

Utaratibu utawekwa kuhimiza viwanja vingine vinavyotumika kwa michezo mbalimbali kuwa na vifaa thabiti vyta ya huduma ya kwanza siyo tu kwa ugonjwa wa moyo bali dharura yejote ya majeraha michezoni.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwulize swali moja la nyongeza. Matukio haya ya ugonjwa wa moyo na kuanguka viwanjani wachezaji yamekuwa yakiwaathiri wachezaji duniani kote na kumbukumbu zinaonyesha hata Tanzania yamewahi kutokea tulipoteza mchezaji Hussein Tindwa, tarehe 26 Juni, 2003 mchezaji maarufu wa Afrika Mark Vivian Foo alianguka na kupoteza maisha. Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa duniani.

Je, pamoja na kwamba wachezaji wanamilikiwa na vilabu vyao, lakini Tanzania kama Taifa na wachezaji hawa

hawa ndio wanaoshiriki katika timu ya Taifa na kutoa mchango wao mkubwa?

Je, Serikali ina mipango gani endelevu wa kuhakikisha upimaji wa afya kwa wachezaji wetu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa hapa Tanzania kuliwahi kutokea tukio kama hilo mwaka 1977 timu ya Nigeria ilipocheza hapa na kweli mchezaji huyo alifariki na ni kweli kwamba matukio haya yanaendelea kutokea katika dunia.

Nataka nimhakikishie tu kwamba Serikali kwanza itakiimarisha kitengo cha Kinga na Tiba kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa wataalam na Madaktari wa timu, na niombe tu kwamba vilabu vyote vihakikishe vinaajiri madaktari ambao wana uzoefu kwa ajili ya Tiba na Kinga katika vilabu vyao.

Lakini la tatu, niwaombe wachezaji kupima afya zao mara kwa mara kila wanapohisi pia kuna dalili za magonjwa kama hayo ili yasitokee tena. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kutokana na habari ambazo Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi ametupatia hapa kuhusu boti ambayo imezama jana ikielekee huko Nungwi kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote ningependa kutoa pole na salaam za rambirambi kwa familia za wote waliohusika na

mkasa huu na tunawaombea marehemu basi Mwenyezi Mungu azipokee roho zao na kuziweka mahali pema peponi, Amina.

Na. 43

### **Muswada wa Sheria ya Kupata Habari**

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA (K.n.y. MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE)** aliuliza:-

Ni kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikitoa ahadi ya kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Kupata Habari (*Right to Information (RTI)*) ahadi ambayo mpaka leo hajatekelezwa; na haki ya kupata taarifa mbalimbali ni ya Kikatiba ambayo imeainishwa katika Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

Je, Muswada huo utawasilishwa lini Bungeni ili upitishwe kuwa Sheria itakayowezesha wananchi kwa ujumla na vyombo vyta habari kuweza kufaidika na haki hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu

swali la Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombé, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipokea maoni ya wadau wa habari na Haki za Binadamu ya kutaka kuwepo kwa sheria mbili za masuala ya habari; moja ni Sheria ya Kusimamia Vyombo vyá Habari na nyininge ni Sheria ya Haki ya Kupata Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali baada ya kupokea mapendekezo ya utungwaji wa Sheria hizo, kwa sasa inaona ni muhimu kuwa na Sheria ya Kusimamia Vyombo vyá Habari itakayounda vyombo muhimu vyá kusimamia utendaji wa vyombo vyá habari nchini na Sheria ya Haki ya Kupata Habari ikifanyiwa utafiti kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali iko katika hatua za mwisho za vikao vyá maamuzi ili kuwasilisha Bungeni Muswada wa kutunga Sheria ya Kusimamia Vyombo vyá Habari.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ameleta majibu ya Sheria ya Kusimamia Vyombo vyá Habari swalí ambalo Mheshimiwa Filikunjombé hakuliuliza, yeye aliuliza Sheria ya Haki za Raia kupata habari.

Kwa kuwa katika majibu aliyoyatoa ametumia maneno 109; na kwa kuwa kati ya maneno 109 ni maneno 17 tu ndiyo yanayohusu majibu ya Mheshimiwa Filikunjombé

na maneno 92 yanahusu majibu ya swali ambalo halikuletwala.

Sasa nataka Mheshimiwa Naibu Waziri aliambie Bunge lako Tukufu hili kama yeye angeenda kuzindua uwanja wa mpira halafu katika *coverage* ya TV anamwona dereva wake ndiyo anazindua kwa maneno 92 na yeye anasalimia tu maneno 17 kama ingekuwa ni sahihi?

Swali la pili, kwa kuwa Ibara ya 18 imetamka bayana raia kuwa na haki ya kupata habari na kumekuwa na tabia ya wananchi kutopata habari hasa zinazohusu Mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanakuta maeneo wanayoishi Serikali imefunga mikataba lakini hawana habari juu ya mikataba ile. Je, atuhakikishie ataleta lini Bungeni humu Sheria ya raia kupata haki za habari ili tuondokane na mambo watu wanaandamana kwenye gesi, watu wanaandamana kwenye madini kwa sababu ya kutopata habari juu ya kinachoendelea kwenye mikataba? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tu niseme kwamba swali linahusu sheria, haki ya kupata habari. Nimeeleza katika majibu ya msingi kwamba Serikali imekaa na wadau ilipokea maoni mbalimbali ikaonekana kwamba sheria zinazotakiwa kutungwa ziwe mbili yaani Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari na Sheria ambayo

imeulizwa ya haki ya kupata habari. Lakini mchakato wa sheria hii ya Kusimamia Vyombo vya Habari ni matokeo ya Sera ya Utangazaji ya mwaka 2003 iliyotamka wazi kwamba Serikali itazifanyia marekebisho sheria zote za habari kuwa na Sheria moja.

Lakini mchakato huu ulianza mwaka 2007, na ndiyo maana Serikali imekuja na majibu kwamba ilipokea maoni hayo hiyo haki ya kupata habari bado inafanyiwa utafiti kwanza. Kwa hiyo, Serikali imejipanga kuja na Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari na katika majibu yangu ya msingi yameeleza hivyo.

Nataka niseme tu kwamba lazima tuendelee kufanya utafiti na katika Afirka kuna nchi 14 ambazo tayari ndiyo wana sheria hii. Kwa hiyo, Tanzania hivi karibuni tulipeleka Wabunge wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwenda kujifunza India na walipelekwa na MCT na inaonekana hata MCT wenyewe bado wanataka kupata uzoefu huo.

Kwa hiyo, Serikali inaona tuendelee kufanya utafiti na hayo ndiyo majibu ya Serikali kwamba tutakuja na Muswada wa Kusimamia Vyombo vya Habari ili kuwa na Vyombo thabiti vitakavyosimamia suala zima la Habari.

Suala hili ni kwamba wananchi wanayo haki ya Kikatiba kabisa kupata habari imetamkwa katika Katiba na sisi tunasema tupo ndani ya Serikali tumejipanga kuna Maafisa Habari kwa kila Wizara na kwa kila sehemu kutoa habari muhimu zinazohitajika. (*Makofi*)

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Swali langu ni moja ambapo nataka kujua. Ni vipi Serikali itashirikiana na wadau wa habari ambao walitoa Muswada huo toka mwaka 2008 ili kuhakikisha wananchi wana haki ya kupata habari? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi kwamba sheria hii inafanyiwa utafiti. Kwa hiyo, kufanyiwa utafiti ni pamoja na kuwasikiliza wadau kama ambavyo anashauri Mheshimiwa Mbunge na Serikali itakuwa tayari kuwasikiliza wadau hao.

Na . 44

### **Uwiano wa Askari Polisi na Raia**

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE** aliuliza:-

(a) Je, Askari Polisi mmoja wa Tanzania analinda wananchi wangapi?

(b) Je, kwa uwiano huo kuna upungufu wa Askari Polisi wangapi katika mipango yetu ya ulinzi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mbunge wa Jang'ombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi lina jumla ya Askari wapatao 38,847 waliopo kazini na 3,000 wanaendelea na mafunzo ya awali katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi. Kwa mujibu wa Sensa ya Taifa iliyofanyika mwezi Agosti, nchini yetu ina jumla ya watu 44,929,002, watu 43,925,434 wako Tanzania Bara na 1,303,568 wako Tanzania Zanzibar. Kutokana na takwimu hizo uwiano wa Askari kwa raia ni 1:1,156 yaani hivi sasa Askari mmoja analinda wananchi 1,156.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano unaokubalika Kimataifa ni Askari Polisi mmoja kuwalinda wananchi wapatao 400 – 500. Ili kutekeleza uwiano unaokubalika Kimataifa Jeshi la Polisi linatakiwa kuwa na angalau Askari 89,858. Kwa kutumia viwango hivyo vyta uwiano wa Askari na raia Kimataifa, Jeshi la Polisi Tanzania lina upungufu wa Askari 48,011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya juhudzi za makusudi kuziba pengo hili kwa kuajiri Askari ili kulijengea uwezo Jeshi la Polisi katika eneo la rasilimali watu. Mathalan, idadi ya Askari imeongezeka kutoka 28,000 mwaka 2006 hadi 38,000 mwaka 2012, na kwa hivi sasa zaidi ya Askari kama nilivyosema 3000 wanapatiwa

mafunzo katika Chuo cha Taaluma ya Polisi, Moshi.  
*(Makof)*

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, je Jeshi la Polisi lina mkakati wowote wa kuajiri vijana katika kuboresha uwiano huo?

La pili, uwiano wa raia na Polisi ni muhimu, lakini uwiano wa kijinsia ni muhimu sana kwa hili. Je, katika hawa Askari 38,847 Askari wa kike ni wangapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba kwa sababu bado uwiano siyo mzuri, Jeshi la Polisi linaendelea kuajiri vijana kila Bajeti inaporuhusu na tutaendelea hivyo tukiwa na lengo la kuhakikishia kwamba tunatoa huduma kwa Watanzania kwa karibu kuliko ilivyo sasa.

Swali la pili, uwiano wa Askari wa kike na kiume, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba Askari wote ni 38,847 na kwa sasa Askari 7,450 ambao ni kama asilimia 19 ni jinsia ya kike na hii hasa imekuja kwa sababu ya mahitaji wakati mwingine ya kazi maalum. Kwa hiyo, inawezekana kwamba bado ni vigumu kupata uwiano ambao ungekuwa kubwa kuliko huu. Hata hivyo, jitihada zinaendelea kuhakikishia kwamba uwiano tunauweka vizuri zaidi ili nasi tuwe tunashiriki kwenye *affirmative action*. *(Makof)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuelewa tatizo la upungufu wa Askari, Jeshi la Polisi huwa linaruhusiwa kuwa na *auxiliary police* ambao huwasaidia kwa kuwalipa fedha kidogo.

Pili, vilevile hutumia utaratibu yale maeneo ambayo hayana uhalifu mkubwa hupelekwa Askari kidogo na yale ambayo yana uharibifu mkubwa hupelekewa Askari wengi.

Je, utaratibu huu umesitishwa kwani bado yale maeneo ambayo yana uharibifu mkubwa bado yanaonekana vilevile yana upungufu mkubwa wa Askari kwa sababu gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba utaratibu ambao ameueleza Mheshimiwa Mbunge ndiyo ambao tunautumia katika kugawa Askari. Pamoja na hivyo kwa sababu Askari wote kwa ujumla ni wachache bado kunaweza kukaonekana kuna upungufu.

Mfano mmoja, ni kwamba pale ambapo kuna matatizo mfano, Kanda ya Dar es Salaam, Ranya tunahakikisha kwamba tunazipa nafasi ili Askari wawepo wengi kwa sababu ya huduma zinazohitajika kule.

**NAIBU SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Vincent Nyerere, upendeleo maalum kwa sababu wewe ni shemeji wa Polisi. (*Kicheko*)

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa, uchumi wa nchi unakua kwa zaidi asilimia 6 na Askari hawatoshi na vijana wapo tayari kwa nini Serikali isitangaze ajira kila mwaka wa fedha angalau asilimia 6.8 kwa ongezeko la Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri wote ni wadau katika kuhakikisha ajira hii inafanikiwa. Kwa hiyo, uchumi ukikua tuamue kama Bunge kwamba asilimia sawa ya uchumi iwe sawa na asilimia ya ukuaji wa Jeshi la Polisi kwangu mimi ninalikaribisha. (*Makof*)

Na. 45

### **Imani ya Wananchi kwa Jeshi la Polisi Zanzibar**

**MHE. TAUHIDA C. GALOS NYIMBO** aliuliza:-

Matukio mbalimbali yanayotokea hivi sasa huko Tanzania Zanzibar yamepelekea wananchi kupoteza imani kwa Jeshi la Polisi kwa kushindwa kuwajibika na kupoteza haiba ya Kizanzibar:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wa Zanzibar ili waweze kurudisha imani yao kwa Jeshi la Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Galos Nyimbo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba yapo matukio yenyeye sura ya kisiasa yaliyowahi kutokea Zanzibar. Matukio hayo yalisababishwa na watu mbalimbali wenye sura na msimamo wa kidini, ambayo yalisababisha uharibifu wa mali za Serikali na watu binafsi.

Hata hivyo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na wananchi kwa ujumla matukio yote hayo yaliweza kudhibitiwa na hali sasa ni shwari kuliko ilivyotegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wananchi wa Zanzibar wana imani kubwa sana kwa Jeshi la Polisi katika kulinda usalama wao na mali zao. Wananchi waliopo Zanzibar wamekuwa wakitoa ushirikiano mkubwa kwa Jeshi la Polisi kuweza kudhibiti vitendo hivyo, kwa kuwafichua wahalifu wanaofanya vitendo hivyo viovu. Jeshi la Polisi litaendelea kuwaelimisha wananchi ili kuona umuhimu wa kudumisha amani na utulivu katika maeneo yao. (*Makofl*)

**MHE. TAUHIDA C. GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa wewe unatoka Zanzibar utakubaliana nami kwamba kumekuwa na tatizo la makusudi ndani ya Jeshi la Polisi Zanzibar kupewa taarifa mapema na kukawia kuzifanyia kazi badala yake?

La pili, Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar kumekuwa na vituo vingi vya Polisi, lakini vituo hivyo havina uzio vimezungukwa na makazi ya watu. Nitatoa mfano, kituo cha Mwanakwerekwe wakati sisi tunakua kituo kile kilikuwa hakijazungukwa na makazi ya watu. Leo hii nimesimama hapa kumejengwa jengo kubwa la biashara nadhani kwamba kiusalama vituo hivi Naibu Waziri si halali kwa usalama wa Askari Polisi wanaokaa mahali pale? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kuhusu kupewa taarifa mapema na kuchukua hatua wakiwa wamechelewa. Hili linaweza likawepo, lakini sina ushahidi nalo.

Ninachojua ni kwamba Polisi wanachukua hatua za haraka na kwa sababu kila wakati kunakuwa askari wa doria na askari ambao pia tunao kikosi maalum cha *Quick Response* sidhani kama hili linaweza likatokea nje ya kuwa na matatizo ya *logistics*. Hata hivyo kama hili lipo naomba nizungumze zaidi na Mheshimiwa ili anipe ushahidi na taarifa ili niweze kuzifanyia kazi na hili lifanyiwe kazi lisitokee tena. (*Makof*)

Tatizo la vituo kuwa havina uzio. Nakubaliana naye kwamba kuna vituo ambavyo havina uzio na nafasi ya kutosha na mfano mmoja ni huo wa Mwanakwerekere. Lakini pamoja na mahitaji ya Jeshi la Polisi kuwa na kituo pale pia utaratibu wa kugawa ardhi unafanywa na taasisi ambayo pengine inatumia *factors* nyingine nje ya hivyo na Polisi wakishapewa eneo lao na likiwa na mpaka inakuwa ni vigumu kuweza kufanya vinginevyo.

Lakini kituo cha Mwanakerekwe chenyewe kipo kwenye eneo ambalo mwanzoni lilikuwa ni eneo la maonesho na kila taasisi ilikuwa na eneo lake, kwa hiyo isingeweza kujipanua. Hata hivyo tutaweza kuangalia athari ya mambo na ikiwezekana tutatafuta ufumbuzi unaoweza kupatikana. (*Makofi*)

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa uhalifu nchini unasababishwa kwa asilimia kubwa na ukosefu wa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa niliwahi kupendekeza hapa Bungeni kwamba Serikali ijikite kwenye mpango wa *Crime Prevention Programme*. Sasa naomba kujua Serikali iliyafanyia kazi mapendekezo yangu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, elimu sio mara zote na wala sio kigezo muhimu katika uhalifu. Inawezekana ikawa tabia na umaskini ni vigezo muhimu zaidi kuliko elimu.

Ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge alitoa mawazo hayo na *Prevention Mechanism* ni kazi yetu na tuna programu hiyo inaendelea. Kwa hiyo, siyo utekelezaji wa maagizo au maelekezo uliyotupa, lakini ni maelekezo ya shughuli zetu ambazo kwa jumla tunazifanya.

Njia muhimu tunazozitumia sio tu kwenda kupiga mabomu pale ambapo kuna maandamano, lakini tunajaribu kuwaelimisha watu kama njia muhimu ya *prevent* matatizo haya. Tunatumia taasisi ambazo ni muhimu za kijamii hasa, watu wa dini na kadhalika ambao waumini wao ndio mara nyingi wanakuwa au wahanga au wahalifu. (*Makofi*)

Na. 46

### **Udhibiti wa Bidhaa Feki**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Bidhaa zisizo na viwango (bidhaa feki) zimeendelea kuuzwa na kununuliwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini na kusababisha watu wengi kupata hasara:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kudhibiti bidhaa hizo zinazotengenezwa ndani na nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kutoeleweka na watu wengi kuhusu maana ya bidhaa bandia (feki) na bidhaa zisizo na viwango (hafifu) au bidhaa duni. Watu wengi wanazichanganya hizi. Bidhaa bandia ni bidhaa zinazotengenezwa kwa kuiga nembo au alama ya bidhaa halisi ambazo zinasimamiwa na Tume ya Ushindani (*FCC*). Aidha, bidhaa zisizo na viwango ni zile zisizofikia viwango vya kitaifa au kimataifa ambazo husimamiwa na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufanuzi huo nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa bidhaa zote hizi, zisizo na viwango na bandia zimeendelea kuuzwa na kununuliwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini na kusababisha watu wengi kupata hasara. Udhibiti wa bidhaa bandia umeendelea kusimamiwa na Wizara yangu kuitia Tume ya Ushindani (*FCC*) ambayo imekuwa na mikakati mbalimbali ya udhibiti kama ifuatavyo:-

(i) Kuzitambua bidhaa hizo kwa kushirikiana na wamiliki wa nembo na alama za bidhaa husika kwa kuzingatia Sheria ya Alama za Bidhaa ya mwaka 1963 na marekebisho yake. Aidha, ni kosa kwa mtu asiye na ridhaa ya mmiliki kutumia alama au nembo ya mtu mwingine kuzalisha bidhaa zinazofanana na bidhaa halisi.

(ii) Kuendesha ukaguzi katika maeneo ya biashara kwa kushirikiana na wamiliki wa nembo na alama za bidhaa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *TBS* ipo mifumo mbalimbali ya kudhibiti ubora wa bidhaa ikiwa ni pamoja na kuchukua sampuli kutoka viwandani na kuzipima kwenye maabara (*Mark Certification Scheme*). Mfumo mwingine ni wa kutumia *Tested Product Certificate* kwa bidhaa ambazo hakuna kiwango cha kitaifa. Aidha, mzalishaji anayetumia mfumo huo hupewa *Tested Product Certificate* na haruhusiwi kutumia nembo ya ubora isipokuwa maneno kuwa imethibitishwa na *TBS*. Pamoja na hayo, kuanzia mwezi Februari, 2012 *TBS* imeanza kutumia Sheria ya Ukaguzi wa Bidhaaa Nje ya Nchi (*Pre-shipment Verification of Conformity to Standards (PVOC)*) ili kuhakikisha kuwa bidhaa zisizo na ubora haziingii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wafanyabiashara wanaopatikana na makosa ya kuuza bidhaa zisizo na ubora au bandia, huchukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kuteketezwa kwa bidhaa hizo kwa mujibu wa sheria na mamlaka husika.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Akizungumza na Waandishi wa Habari Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda, mwishoni mwa mwaka wa jana 2012 alisema asilimia 20 ya bidhaa zinazoingizwa nchini ni bandia na akazitaja kwamba ni matairi ya magari na pikipiki,

mafuta ya kupaka, maziwa ya watoto, nyaya za umeme na vyakula mbalimbali. Pia alisema kwamba kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo kuna bandari bubu zipatazo 32 za kupakua vifaa vya bandia.

Je, swali, kusuasua kwa Serikali uzembe huu na udhaifu na kutodhibiti tatizo hili kwa muda mrefu ni lini utamalizika?

Pili, kwa madhara yanayotokana na tatizo hili ni makubwa kwa mfano mafuta ya kupaka huchubua ngozi, maziwa ya watoto, watoto wanaharisha sana, nyaya za umeme, nyumba nyingi zimeungua moto.

Swali. Serikali sasa ipo tayari kuunda Tume Maalum ya kuwatambua wale wote walioathirika na angalau kuweza kuwasaidia kundi la watoto ambao wameathirika na maziwa ambayo sio salama, maziwa bandia?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu kuenea kwa bidhaa bandia. Kama alivyosema Mbunge kwamba Waziri alikiri kwamba asilimia 20 mpaka 30 ya bidhaa hizi bado zimo na zinaonekana kwenye maduka yetu. Kuna uzembe labda lakini naomba nikiri kwamba kweli anavyosema Mbunge ni sawa kwamba bidhaa hizi bado zinaonekana na si uzembe kwa kweli. Serikali kupitia Wizara yangu inajitahidi sana kupitia vyombo vyake *TBS, FCC*.

Lakini kwa bahati mbaya sana wakati Serikali inajitahidi na wale wabadhirifu au wahalifu wale ambao wanavunja sheria ambazo zipo nao wanajitahidi kweli kweli. Sheria zipo kama hii sheria ambayo nimesema kwamba ni

alama za bidhaa ya mwaka 1963 pamoja na marekebisho yake inakataza kabisa kutengeneza bidhaa bandia ni makosa, kuingiza bidhaa bandia ni makosa, kuuza au kuhifadhi ni makosa, lakini bado wako watu ambao siyo wazalendo, siyo waadilifu wanazidi kufanya mambo haya yote.

Kwa hiyo, bado sasa hivi tunapambana sana. Serikali hasa Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi zingine au Wizara zingine tumeamua tushirikiane pamoja. Tushirikiane na vyombo vyetu *TBS*, *FCC* na Wizara ya Afya kwa maana ya *TFDA*, Polisi tujaribu kutatua tatizo hili la wahalifu hawa ambao wanakatazwa kutengeneza, kuingiza na kuuza au kuhifadhi, lakini bado wanaendelea.

Kwa hiyo, hili siyo uzembe bali ni janga au changamoto kubwa sana ambayo tunaendelea nayo.

Kwa bidhaa ambazo tayari zimeshaingizwa kusema kweli ambazo zinaleta hasara kubwa sana kwa watoto wetu kama maziwa, vifaa vya umeme, vifaa vya magari ambavyo havina ubora na vimeshaingia kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba je kuna utaratibu gani wa kupata angalau fidia. Zipo taratibu kwa mfano kama *TANESCO*.

Kama utakuwa umeathirika na umeme na kama utathibitisha wana utaratibu wao. Lakini kwa utaratibu kusema kwamba kama mtoto amekunywa maziwa ambayo siyo bora na kama taarifa tunazo kamili nafikiri hilo

linaweza likazungumzwa na likaelewka tukaangalia namna ya kufidia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swalii hili limechukua muda mrefu naomba tuendelee na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvumi. Swalii linaulizwa na Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake namwona Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Na. 47

### **Viwanda Vinavyosafirisha Samaki Wazima Nje ya Nchi**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. AMINA N. MAKILAGI)** aliuliza:-

Vipo baadhi ya Viwanda nchini vinasafirisha Samaki wazima badala ya Minofu:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya viwanda hivyo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, Kanuni ya 91(a) inatamka wazi kuwa mtu ye yeyote haruhusiwi kuuza nje ya nchi samaki au zao lingine la uvuvi hadi samaki au zao hilo lichakatwe kwenye Kiwanda au eneo lililoidhinishwa na Mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuweka kanuni za kuchakata samaki kabla ya kusafirisha nje ya nchi ni kuongeza mazao ya uvuvi. Mfano samaki aina ya Sangara huchakatwa na kutoa mazao kama vile ngozi, minofu, mabondo, mapanki, utumbo na mafuta. Aidha, uchakataji huongeza thamani ya mazao hayo katika soko na kuongeza ajira kwa wananchi, pato kwa wenyewe viwanda na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo, wapo baadhi ya samaki ambao huchakatwa au kusafirishwa wakiwa wazima kuto kana na maumbo yao au hitaji la soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Viwanda vya kuchakata samaki haviruhusiwi kusafirisha samaki ambao hawajachakatwa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imebahatika kuwa na maziwa makubwa na yenye samaki wengi na wa kutosha ambao wangeweza kutusaidia sana kukuza ajira na uwekezaji katika nchi yetu. Kwa kuwa tuna *Tanzania Investment Bank* na kwa kuwa pia tuna *Tanzania Investment Centre* na kwa kuwa tuna Wizara inayoshughulikia masuala haya ya uvuvi.

Je, Serikali haioni sasa kwa kuunganisha nguvu ya vyombo hivi vyote nilivyovisema ione umuhimu wa kufungua viwanda vingi vya samaki si tu katika Jiji la Mwanza pia kwenye maziwa ya Nyasa, Tanganyika ili kutusaidia kutatua tatizo kubwa la ajira kwa vijana wetu wa Tanzania na kuongeza kipato kwa wananchi wa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali hili anaonyesha kabisa kwamba pamoja na tamko zuri sana la Mheshimiwa Waziri kuititia Serikali tatizo la kuuza samaki hawa kabla hawajachakatwa bado lipo katika nchi yetu.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kupambana na hawa wawekezaji ambao wanaharibu uchumi wa nchi yetu kwa kufanya utafiti na kuwabaini watu hao na kuwachukulia hatua na kutoa taarifa za hatua zilizochukuliwa ndani ya Bunge hili?

#### **WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lake la kushirikiana na *TIC* nakubaliana na ye ye kabisa kwamba Serikali inashirikiana na *TIC*, Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara yangu mimi katika kutafuta wawekezaji ili waweze kuanzisha viwanda vya kuchakata samaki na hasa kwenye maji ya bahari yaani kwenye samaki wanaotoka kwenye maji ya chumvi kwa sababu ya kule Ziwa Victoria tayari viwanda vinatosha.

Lakini vilevile kufungua viwanda kwenye maziwa ya Nyasa, Tanganyika kwa sababu kule hatujapatumia hatuna viwanda vya kutosha kule. Kwa hilo linafanyika na *incentives* mbalimbali, mazingira mbalimbali ya kibiashara yanatolewa kwa wawekezaji kwa sababu Serikali kazi yake ni kutoa mazingira mazuri, Serikali haiwezi ikafanya biashara ama kufungua viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nakubaliana na Mheshimiwa Jenista Mhagama kuhusiana na suala la kupambana na watu ambao wanavunja sheria na kusafirisha samaki ambao hawajachakatwa. Lakini ningependa nitoe maana ya kuchakata. Maana ya kuchakata kutohana na Sheria Namba 22 ya Mwaka 2003 Sheria ya Uvuvi. Maana ya kuchakata ni pamoja na kukata minofu, pamoja na kusafisha samaki, pamoja na kuhifadhi kwa kutumia chumvi ama kwa kutumia barafu, lakini ni pamoja na kukausha kwa kutumia moshi na kuweka kwenye makopo pamoja na kugandisha. Kwa maana hiyo hata kama samaki hajakatwakatwa ili mradi amesafishwa hiyo ndiyo maana halisi ya kuchakata. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi Waheshimiwa Wabunge. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali.

Na. 48

### **Ujenzi wa Barabara ya Lami - Kibondo**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI** aliuliza:-

Wananchi wa Kibondo wanahitaji sana barabara ya lami:-

(a) Je, ni lini barabara ya Nyakanazi – Kibondo – Kigoma itakamilika na imetengewa fedha kiasi gani?

(b) Katika kitabu cha orodha ya ahadi za Mheshimiwa Rais aliahidi kilomita 1.5 za lami Kibondo Mjini. Je, ni lini ahadi hiyo itatimizwa?

(c) Je, ni lini barabara ya Kimataifa ya kutoka Kibondo – Mabamba hadi mpaka wa Burundi itajengwa kwa lami?

#### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mbunge wa Muhammwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Nyakanazi –Kibondo –Kigoma sehemu ya Kidahwe – Nyakanazi yenye urefu wa kilometra 310 utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kimetengwa kwa ajili ya kufanya matayarisho ya kuanza ujenzi wa barabara hii.

Aidha, barabara hii ipo katika orodha ya miradi iliyopewa kipaumbele katika miradi iliyoinishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Barabara za Jumuiya ya Afrika

Mashariki ambapo Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na nchi wanachama inatafuta fedha za ujenzi kutoka kwa wafadhali mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za Mheshimiwa Rais zinatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa kuwa barabara za Kibondo Mjini ziko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, namshauri Mheshimiwa Mkosamali ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo kuziweka kwenye mpango ili zijengwe kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekwishaanza maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kidondo – Mabamba hadi mpakani na Burundi kilomita 40 ambapo katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 kiasi cha shilingi milioni 144.67 kutoka katika Mfuko wa Barabara zilitengwa kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara hii.

Aidha fedha za nyongeza kiasi cha shilingi milioni 150 kutoka Mfuko wa Barabara zimetengwa katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo. Serikali inaendelea na taratibu za kumtafuta Mhandisi mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii ambapo baada ya kazi hiyo kukamilika Serikali inatafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ninamaswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba kila mwaka zimekuwa zinatengwa fedha kidogo sana kwenye ujenzi wa barabara hii ambayo

ni muhimu sana kwa wananchi wa Kigoma na hata juzi kuna Mbunge mwengine wa Kigoma ameuliza swali hilihili. Sasa nataka majibu sahihi kwenye Bajeti ijayo barabara hii itakuwepo, itatengewa fedha za kutosha au haitatengewa? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili. Kwenye jibu (b) Mheshimiwa Naibu Waziri ameniambia mimi nikawasiliane na Halmashauri. Mimi sio karani wa Rais kwanza, Rais aliahidi ana watu wake anaowaagiza kufuatilitia ahadi zake na hii barabara siyo ya Halmashauri.

Hii barabara Rais aliahidi kujenga kwa Barabara za *TANROADS*. Sasa naomba atupe majibu sahihi kama Rais aliahidi uongo au alitoa ahadi za kutafuta sifa tu ili achaguliwe au barabara hii itajengwa? Kama haijengwi aseme kwamba Rais alisema uongo pale Kibondo ili tujue kuliko kuwa anatupa majibu eti mimi nikawasiliane na nani, mimi sio karani wa Rais.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na hili la pili ambalo nimemwelekeza awasiliane na Halmashauri kusudi waiweke ile barabara kwenye mpango. Huu ni utaratibu wa kawaida. Rais akiagiza Serikali ni moja Halmashauri ya Wilaya iko kwenye Serikali hiyohiyo ya Kikwete. Kwa hiyo, akisema atajenga ndiyo maana yake hiyo. Kwa hiyo, mipango yote hiyo lazima ianzie kwenye Halmashauri.

Kwa hiyo, zipo barabara ambazo Wizara ya Ujenzi inazishughulikia na zipo ambazo zinashughulikiwa na Halmashauri na Mfuko wa Barabara unagawa asilimia 30

wanapata Halmashauri na asilimia 70 zinakwenda Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo ni sahihi kabisa na si kwamba Rais ameahidi kitu ambacho si sawasawa.

Swali la pili kwamba je, mwaka wa fedha utakaofuata zitawekwa fedha za kutosha. Jibu ni kwamba kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, barabara hii ni kipaumbele tayari. Ndiyo maana tunasema tunatafuta fedha kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kilomita 310 unazungumza bilioni 310. Haiwezekani ukasema kwenye Bajeti moja ukaweka bilioni 310/-.

Kwa hiyo, ni kwamba tumeshaiweka hii barabara ni kipaumbele na ndiyo maana tumeshatenga fedha za kuanza maandalizi. Ukiweka bilioni tatu, maandalizi ya ujenzi maana yake hata kuanza kufidia barabara itakapojengwa. Kwa hiyo ni sehemu ya maandalizi na ni sehemu ya ujenzi wa barabara hiyo. Nikuhakikishie wewe na wananchi wa Kigoma kwamba Serikali imedhamiria kujenga barabara hiyo ya kutoka Kidahwe mpaka Nyakanazi kwa kiwango cha lami.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Siku zinavyozidi kwenda mji wa Bunda unakua na Mheshimiwa Rais katika ahadi zake za kampeni pale Bunda alisema zitajengwa kilomita 10 za lami.

Lakini pia nachukua fursa hii kuipongeza Serikali mpaka sasa hivi tayari kilomita tano zimeshajengwa na si kila Halmashauri ina uwezo wa kukusanya mapato, zimetofautiana. Sasa napenda kujua Mheshimiwa Naibu

Waziri katika mwaka ujao wa fedha hizi kilomita tano zitakuwa sehemu za utekelezaji?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga ni kuchagua. Tutakapowasilisha Bajeti yetu ya Wizara kwa ajili ya mpango wa mwaka utakaofuata kama tutawekewa fedha hizi basi tutajenga. Maana itategemea na uwezo wa upatikanaji wa fedha. (*Makofi*)

Na. 49

### **Ujenzi wa Barabara ya Mkiwa – Itigi – Rungwa – Makongorosi**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mkiwa - Itigi - Rungwa - Makongorosi kwa kiwango cha lami ulishafanyika:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kujenga barabara ya lami kuanzia Mkiwa - Itigi - Rungwa -

Makongorosi – Chunya – Mbeya yenyе urefu wa kilometa 528 kuunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya na Mikoa mengine ya ukanda wa kati na ukanda wa Kusini ili kufungua fursa za kiuchumi katika Mikoa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa sehemu ya barabara ya Mkiwa – Itigi – Rungwa – Makongorosi yenyе urefu wa kilometa 413 ulishafanyika na kukamilika mwaka 2011 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.6 zikiwa ni fedha za ndani. Baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina wa barabara ya Mkiwa – Itigi – Rungwa – Makongorosi, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, barabara hii pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais katika majibu inasemekana kwamba fedha za ndani zinatafutwa ni muda mrefu.

Lakini ninachotaka kujua ni kwamba kumekuwa na alina mbili za barabara kwanza kuna ya kwanza ambayo inafadhiliwa na fedha za ndani halafu barabara zingine zinafadhiliwa na fedha kutoka nje. Napenda kujua ni vigezo gani vinavyotumika katika kutoa *discretion* kwamba barabara hii zitumike fedha za ndani na barabara zingine zitumike fedha za nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kabla ya uchaguzi katika barabaa hii inayotarajiwa kujengwa nyumba nyingi ziliwekewa alama za kuvunjwa. Kuanzia Rungwa mpaka Mkiwa takribani vijiji 20 na miji midogo miwili. Sasa napenda kujua Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia hawa watu wanaostahili kulipwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza anaulizia vigezo vya kufadhili barabara kwa fedha za ndani au kwa kutumia wafadhili. Kusema kweli ni kwamba kama tumeshindwa kupata mfadhili wa kutusaidia au kukopa tunatumia fedha zetu za ndani na barabara hii kama unavyosema Rais ameagiza ni kwamba kama hatutapata mfadhili tutatumia fedha zetu za ndani kujenga barabara hii na nikuhakikishie kwamba lengo la Serikali barabara hii ijengwe kabwa ya 2015.

Kuhusu swali la pili, suala la kulipa fidia kwa wale wanaostahili tutalitekeleza pale tunapoona kwamba sasa tupo tayari kuanza ujenzi kwa sababu tuna miradi mingi ambayo inaendelea na hatuwezi ku-*commit* fedha za kulipa fidia halafu tukakosa fedha za kulipa makandarasi ambao wapo tayari wanafanya kazi. Kwa hiyo, tutakopoanza na kupata fedha za uhakika za kujenga barabara hii ndiyo tutaanza kulipa fidia.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwenye llani ya CCM ya mwaka 2010 -2015 tuliahidi kuanza upembuzi yakinifu wa barabara ya Kagongwa – Bukene hadi Tabora, barabara ya Kahama

Bulyanhulu – Geita na barabara ya Kahama – Kaliua hadi Mpanda.

Hivi sasa miaka miwili ya fedha imekwishapita na hakuna kitu chochote kinachoendelea kwa macho ya wananchi wa kawaida. Nataka kusikia upande wa Serikali kwamba kuna hakikisho gani kwamba mwaka ujao wa fedha 2013/2014 kazi ya walau ya upembuzi yakinifu itaweza kuanza ili baadaye ikiwezekana ujenzi kuanza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwenye llani ya uchaguzi tumeahidi maeneo mengi kwamba tutafanya upembuzi yakinifu.

Lakini upembuzi yakinifu tutaufanya kulingana na upatikanaji wa fedha. Nikuhakikishie tu kwamba kwa sababu tutatoa ratiba ya utekelezaji wa ahadi za Rais na za llani ya Uchaguzi tutaleta hapa Bungeni na mtaona ratiba ni lini barabara hiyo itaanza kufanyiwa upembuzi yakinifu.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Kwa kuwa barabara ya kutoka Tabora kwenda Mpanda na kutoka Mpanda kwenda Kigoma zimeshafanyiwa upembuzi yakinifu ili zijengwe kwa kiwango cha lami na ujenzi huo haujaanza. Lakini barabara ya kutoka Mpanda kwenda Kigoma iko katika hali mbaya sana je, Serikali ina mpango gani wa haraka na wadharura ili kuifanya barabara hii iweze kupitika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Arfi, unataja barabara ya Tabora – Mpanda – Kigoma bila kutaja Urambo namna gani, mbona unaruka? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara aliyoitaja ya Tabora Mpanda Kigoma tumeshaikamisha usanifu na sasa tunatafuta fedha za kujenga barabara hiyo. Siwezi kusema lini tutaanza nasema tu pale tutakapopata fedha ndiyo tutaanza kujenga barabara hiyo.

Na. 50

### **Ubovu wa Njia ya Gari Moshi maeneo ya Msagali – Godegode**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Njia ya treni (gari moshi) eneo la Msagali – Godegode Wilayani Mpwapwa huharibika mara kwa mara hasa kipindi cha mvua nyingi na kusababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa njia ya reli.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza maeneo korofi ya njia ya reli kuwaondolea usumbufu watumiaji hasa katika kipindi cha masika na vuli?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kwa nyakati tofauti mafuriko yanayosababishwa na mvua

yamesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya reli hususan kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe na pia kati ya maeneo ya Msagali na Godegode.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hali hiyo, Serikali kupitia Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (*RAHCO*) imejielekeza kufanya matengenezo madogo na makubwa katika maeneo korofi na hivyo kuwezesha huduma ya usafiri wa reli kurejeshwa na kuendelea kutolewa.

Kazi kubwa ambazo zimefanyika katika maeneo 32 tofauti kati ya mwaka 2010 na 2013 ni pamoja na ujenzi wa madaraja mawili kati ya Kilosa na Gulwe (Km 298 na km 303); uimarishaji wa tuta la reli na urekebishaji wa mwelekeo wa mto Mkondoa kati ya Kilosa na Gulwe.

Kazi zinazokamilishwa ni ufungaji wa mafurushi ya mawe (*gabion*) katika maeneo ya Munisagali na Gulwe na uboreshaji wa mwelekeo wa Mto Mkondoa. Kati ya mwezi Desemba, 2009 na Januari, 2013 jumla ya shilingi bilioni 28.3 zimetumika kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi waishio maeneo ya jirani na reli kuhusu utunzaji wa mazingira. Lengo ni kuwaelimisha wananchi kuendelea na shughuli za uzalishaji mali bila kuathiri miundombinu ya reli.

Tarehe 14 Septemba, 2012, Wizara kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa ya Morogoro na Dodoma, Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wabunge na Makatibu Tarafa wa

maeneo ya Kilosa hadi Gulwe walishiriki mukutano wa hadhara uliofanyika Gulwe.

Maudhui ya mukutano huo yalikuwa ni kuwaelimisha wananchi juu ya athari zitokanazo na shughuli za kilimo na ufugaji zisizozingatia utunzaji wa mazingira na ukiukwaji wa Sheria ya Reli Na. 4 ya mwaka 2002 kuhusu uhifadhi wa eneo la reli (mita 30 kutoka katikati ya njia ya reli).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la uharibifu wa mara kwa mara wa miundombinu ya reli katika maeneo korofi ya Kilosa - Msagali -Godegode hadi Gulwe, Serikali iliajiri Mshauri Mwelekezi (Kampuni ya CPCS kutoka Canada) kwa ajili ya kufanya tathmini ya Mpango wa kufufua na kuboresha utendaji kazi wa Reli ya Kati (*Railway upgrading and performance improvement study of the central line*).

Taarifa ya tathmini hiyo inatarajiwa kuwasilishwa muda wowote kuanzia leo. Ni matumaini yetu kuwa taarifa hiyo itasaidia kubaini mwelekeo wa uimarishaji wa reli katika eneo husika. (*Makofii*)

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Lakini kabla sijaauliza maswali yangu naomba niwapongeze sana wafanyakazi wa reli kwa kuanzisha usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam.

Swali, reli ya kati ilijengwa takribani miaka 100 iliyopita na kwa kuwa teknolojia hubadilika kulingana na wakati

naomba kujua ni mkakati gani ambao umewekwa na Serikali kuwafundisha au kuwasomesha watumishi wa reli ambao wameonyesha uzalendo kwa kutengeneza mabewa na injini za treni na kuinusuru Serikali kuingia gharama kubwa ambayo ingelazimu mabehewa na injini zake zipelekwe nje ya nchi kwa matengenezo?

Je, Serikali inawaandaaje wafanyakazi hawa ili muda utakapofika wa teknolojia mpya kutumika katika njia ya reli wawe tayari kutumia teknolojia hiyo?

Swali la pili, ni takribani miaka minne treni au gari moshi haijatoka Dar es Salaam kwenda Mwanza na kurudi Dar es Salaam lakini kwa sasa treni inatumia siku mbili kwa wiki kwenda Mwanza na kurudi Dar es Salaam.

Je, ni lini treni itaanza safari ya kila siku kwenda Mwanza kutoka Dar es Salaam na kutoka Mwanza kurudi Dar es Salaam na pia Tabora Kigoma na kurudi?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli reli ya Kati ilijengwa kati ya mwaka 1905 mpaka 1926 na maeneo makubwa ya reli hii sasa yamechoka na yanahitaji kufanyiwa mabadiliko makubwa.

Lakini sambamba na hilo pia teknolojia ya uendeshaji wa mabehewa vichwa vya treni na kadhalika na yenye we inabadilika. Wizara kwa kuyatambua hayo kwa kuanzia tumefufua Chuo cha Reli Tabora na kwa kushirikiana na Chuo cha Usafirishaji na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanatengeneza mtaala mpya kwa ajili ya wanafunzi katika chuo hicho. (*Makofi*)

Bajeti inayoandaliwa na kampuni ya Reli Tanzania na Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli, fedha itatengwa kwa ajili ya kuwapa mafunzo nje ya nchi baadhi ya watumishi wa Mashirika hayo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ratiba ya treni kwenda Mwanza na Kigoma kutoka Dar es salaam kila siku, suala hili linategemea na namna tutakavyopata kwa haraka zaidi mabehewa na vichwa vya treni vya kutosha ili kuweza kumudu safari za kila siku kwenda Mwanza na Kigoma.

Tunao mpango sasa hivi tumefungua zabuni kwa ajili ya ununuzi wa vichwa vya treni vipyta, ukarabati unaendelea katika karakana zetu za Morogoro wa vichwa vya treni, ukarabati unaendelea wa mabehewa katika karakana zetu za Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, mchanganyiko wa jitihada zote hizi tunatumani kuwa utatufikisha katika kupeleka treni Tabora, Mwanza, Tabora na Kigoma kutoka Dar es salaam kila siku kama siyo mwishoni mwa mwaka huu basi, mapema mwaka kesho. (*Makofii*)

Na. 51

### **Ahadi ya Kupeleka Umeme Katika Kata za Jimbo la Nkenge**

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA** aliuliza:-

Kumekuwepo na ahadi ya muda mrefu ya kupeleka umeme katika Kata za Ruzinga, Bunyango, Kitobo, Ishozo, Gera, Ishunju, Mtukula na Nsunga:-

Je, Serikali inawaambia nini wananchi hao na hasa ikizingatiwa kuwa suala hilo ni moja ya ahadi za Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa Serikali iliahidi kupeleka umeme kwenye Kata hizo na ahadi hiyo iko mbioni kutimizwa. Kazi ya kupeleka umeme katika Kata za Ruzinga, Bunyango, Kitobo, Ishozi, Ishunju, Mtukula na Nsunga, inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovuti 33 urefu wa kilomita 70.4 njia ya umeme msongo wa kilovuti 0.4 urefu wa kilomita 31na ufungaji wa transfoma ishirini na tatu(23); kumi na mbili(12) za KvA 25, nane (80) za kVA 50, mbili (2) za kVA 100 na moja (1) ya KvA 200 ili kuunganisha wateja 1,856. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa shilingi za Kitanzania billioni tatu millioni mia nne themanini na moja, mia moja na themanini elfu tu(3,481,180,000/=).

Zabuni ya kupata wakandarasi kwa ajili ya kutekeleza kazi hii imetangazwa mwezi Desemba, 2012 kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na ujenzi wa miundombinu ya mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 24.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Gera tayari kina umeme lakini kwa vile eneo ni kubwa suala la kusambaza umeme zaidi ili kukidhi mahitaji lilizingatiwa na tayari limewekwa kwenye Bajeti ya mwaka 2012/2013 ya TANESCO.

Kazi ya kusambaza umemekatika Kijiji cha Gera itajumuisha ujenzi wa njia ya msongo wa kilovuti 0.4 urefu wa kilomita 2 ili kuwaunganishia wateja wapatao 70. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa shilingi za Kiatanzania Milioni Hamsini na Mbili mia nane na tisini elfu tu (52,890,000).

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ninapenda kuishukuru Serikali kwa kazi hiyo au kwa taarifa hii iliyotoa na ukiisoma inapendeza sana. (*Makof*)

Lakini niulize tu Mheshimkiwa Naibu Waziri. Je, yuko tayari kuandama na mimi kuja katika Jimbo la Nkenge niitishe Mkutano mkubwa halafu awaambie wananchi maneno haya aliyoyasema hapa Bungeni, maana sasa hivi Kata hizi alizozitaja hazimsikii wala hazimwoni ili waweze kujua kama ni kweli kuwa umeme utawekwa katika hiyo miezi 24 aliyotaja?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ninaomba nirudie tena kumwuliza Naibu Waziri , ni kweli fedha hizi pamoja na kutangaza hii tenda hizo fedha zipo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ni kwamba niko tayari kuandamana na yeye ninasema niko tayari lakini nitaomba pia na kaka yangu Mshama tuwe naye ili tuweze kwenda kwa usalama zaidi.

La pili, ni kuwa tunakuwa na changamoto ya fedha na mara zote fedha huwa siyo rahisi kutosha lakini tunashukuru wenzetu nchi marafiki wahisani wenzetu wa Norway wameonyesha nia ya kutusaidia na wako tayari na uhakika ni kuwa tunakamilisha utaratibu wa msaada huo. Lakini pia nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Tanzania tulikuwa tunatekeleza miradi ya MCC kipindi kilichopita cha takribani miaka zaidi ya mitano.

Kwa mara hii katika Afrika ni Tanzania na Morroco ndiyo tumebahatika kuvuka na kuingia kwenye MCC awamu ya pili. Kwa hiyo tutapata fedha zingine nyingi na sisi kama Wizara tumedhamiria fedha hizi zote zilizoletwa kwa ajili ya Nishati tuzipeleke kwa ajili ya umeme vijijini.

Lakini kwa kusema haya haina maana kuwa fedha hiyo itakuwa peke yake inatosha. Nichukue nafasi hii kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge kuendelea kufikiria vyanzo vingine vinavyoweza kuusadia mfuko wa *REA* ili kwenye Bajeti ijayo muweze kutujengea uwezo zaidi kwa ajili yakupeleka umeme vijiji maana umeme vijijini una msisimko mkubwa wa kijamii na kiuchumi. (*Makofii*)

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sipendi kuandamana na Mheshimiwa Naibu Waziri lakini Naibu Waziri anapita barabara ya Bonga kwenda

Babati na hizo Kata ambazo nitazitaja anazifahamu. Umeme umetoka Babati Mjini kwenda Kata ya Bonga lakini umeruka Kata ya Singe na Nangara na Naibu Waziri amekuwa akiahidi kuwa huo umeme utashushwa katika hizo ambazo umeme umepita juu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kufahamu hiyo ahadi itatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa nilipotembelea maeneo haya na kwa kuwa, nina mahusiano ya karibu na maeneo haya niliona kuwa kwenye Kata hizi mbili kumerukwa na *line* inapita tutajaribu kuona kuwa gharama zake zikoje. Maana kama umeme ni mkubwa gharama zake pia zitakuwa kubwa kwani itabidi kujenga *sub-station* lakini kama ni njia ndogo ni suala la transfoma tutajaribu kuangalia ninafikiri tuwasiliane baada ya hapa tupate habari kwa ukamilifu zaidi.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi hii kuuliza swali la nyongeza kwenye sekta ya umeme, mwaka jana niliishauri Serikali kutumia ziada ya umeme ya megawati 5 ambayo inabaki pale Kigoma Mjini na tukakubaliana kuwa megawati 5 hizo zitasafirishwa kutoka Kigoma Mjini ili kusudi Vijiji vya Kalenge, Kazulamimba, Kandaga, Kidea, Uvinza mpaka Lugufu ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya vipate umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu ya mwisho mwaka jana nilifahamishwa kuwa tayari tenda ya kujenga

transfoma kutoka Kigoma Mjini kufikia Vijiji hivyo imekwisha tangazwa, ningependa kupata majibu mpaka sasa ni hatua gani kwa maana ya kuwa ujenzi wa hizo transfoma unaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunafahamu kuwa ziko megawati 5 ambazo zinabakia pale Kigoma Mjini na ni rahisi kufikiria kwamba haina gharama kubwa kuanza kusafirisha ule umeme. Kwa hiyo tulikubaliana na tumeweke katika Bajeti ya mwaka uliopita na sasa hivi ninavyosema tenda hizi zimetangazwa na wananchi wa Kigoma na Jimbo la Mheshimiwa Mbunge watambue kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi itafanya kazi hii na tutai kamilisha kazi hii wakati wowote ndani ya miezi 24. (*Makofi*)

Na. 52

### **Viuatilifu vya Zao la Pamba**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakuja na suluhisho la kuwapatia wakulima wa zao la la pamba dawa madhubuti ya kuua wadudu wanaoshambulia zao hilo ikizingatiwa kwamba dawa ya maji iliyosambazwa msimu huu imeshindwa kuua wadudu hao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wadudu wanaoshambulia zao la pamba ambao wanajulikana na watafiti wa Tanzania ni funza wa vitumba( *American Ball warm*). Wadudu hawa wamekuwa wakidhibitiwa na madawa ambayo yamethibitishwa na utafiti wa kitaalam, kwa misingi ya kiwango cha dawa inayotumika, muda na ubora wa dawa hiyo kulingana na vigezo vya kisayansi vilivyothibitika. Hivyo basi viatilifu ni vile ambavyo vimeridhiwa na kupidishwa na taasisi husika stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa kilimo wa 2011/2011, mfuko wa wakfu wa kuendeleza zao la pamba (*cdtf*) ulipokea malalamiko kutoka kwa wakulima kuhusu utendaji kazi wa baadhi ya viuatilifu vilivyosambazwa hususan ZETABETOX katika Wilaya za Nzega na Uyui, Bamethrin katika Wilaya ya za Meatu, Maswa, Kishapu, Shinyanga Vijini, Kahama na KARATE 5EC katika Wilaya ya Bukombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliwaagiza wataalamu wa *TPR* kufuatilia suala hilo. Wataalam hao baada ya ufuatiliaji wa uchunguzi wa sampuli walizochukua katika maeneo hayo walibaini kuwa viuatilifu hivyo vilikuwa na ubora unaokubalika (*active Ingredient – within manufacturers specifications*).

Kwa kutambua hilo Wizara itaendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu kwa wakulima ili kuleta ufanisi katika udhibiti wa usumbufu wa uzalishaji wa pamba. Hii ni pamoja na uchanganyaji, utumiaji wa vinyunyizi na unyunyiziaji na hivyo wakulima wanashauriwa kuendelea kutumia viuatilifu kwa kufuata maelekezo sahihi ya kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha utaratibu wa kuhakiki na kuridhia kwa vigezo vyta kitaalam viuatilifu vinavyoingizwa na kusambazwa kwa wakulima nchini kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vyta zao la pamba utaendelea kuimariswa. (*Makofi*)

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa zao la pamba wamekuwa na matatizo mbalimbali ikiwemo kuuziwa viuatilifu bandia pamoja na uchakachuaji wa mizani ya kununulia zao la pamba pamoja na bei kuwa haieleweki.

Ninataka kujuu, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuwakomboa hawa wakulima wa zao la pamba?

Kwa kuwa Vyama Vya Ushirika vimekuwa na udhaifu mkubwa katia Kuimarishe zao hili la pamba, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuvifufua ili viweze kufanya kazi na kusaidia ubora wa zao la pamba?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili la wakulima wa zao la pamba na kwamba wana matatizo makubwa ameliweka kwa sura tatu la viuatilifu bandia, la mizani na tatizo la bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijielekeze kwa hili la viuatilifu bandia kama swali lilivyokuwa kwa maana hili la mizani na tatizo la bei lina sura kubwa zaidi lakini ni sehemu ya kupatia ufumbuzi tatizo hili kwa upana zaidi, ambalo Wabunge wahusika wote ndugu zangu Wanyamwezi na Wasukuma na sisi tumekuwa tukijaribu kulifanyia kazi pamoja na Serikali kupata ufumbuzi wa muda mrefu. Hili la viuatilifu bandia ninaomba uniruhusu nilisemee kwasababu lina sura ngumu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara hii ya viuatilifu bandia tunasema kuwa *TPRI* kwa maana ya kwamba ndiyo taasisi ya Serikali inayoshughulika kuhakikisha kuwa vitu hivi viko sawaswa inafanya kazi yake, inawezekana kuwa huko wanakokwenda wafanyabiashara hawa kile wanacholeta kuhakikiwa na kile wanachopeleka kwa wakulima ni tofauti. Kwa hiyo, tunapenda kusema kuwa hapa pana kazi kubwa ya elimu, elimu ya matumizi ya viuatilifu vile lakini pia elimu ya kujua kuwa pale ambapo viuatilifu vinapofika na vinapokuwa vinaonekana vina matatizo. (*Makof*)

Tafadhali mhifadhi baadhi ya viuatilifu vile ili kwa wakati wowote ule *TPRI* na wenzake waweze kuja kufanya uchunguzi yaani *spot checking* ya ubora wa viuatilifu hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu wa fedha Wizara ya Kilimo imepanga kuomba fedha kidogo za ziada kwa Serikali ili tupate fedha ya kufanya *spot checking* kwenye maeneo yote kwa viuatilifu vinapokwenda, kwasababu inawezekana kabisa kuwa mfanyabiashara akaleta dawa moja ambayo ni safi lakini akipeleka kwa

mkulima anapeleka dawa ambayo imechakachuliwa na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili la viuutilifu ninawaomba sana wakulima wa pamba wazingatie kuwa kwenye *control mechanism* zile kuna *biological controls*, *cultural controls* na kuna *chemical control* hizi ambazo tunafanya, ninaomba tuzingatie ushauri wa kitaalam wanaotoa ili tujue matumizi na tupate matokeo bora katika matumizi ya viuutilifu pamoja na dawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linalofuata la Vyama vya Ushirika na udhaifu wake nimelisema juzi, tatizo la Vyama Vya Ushirika haliko kwenye Vyama Vya Ushirika vya pamba tu, vyama vya msingi na Vyama Vikuu hapana. Tulisema kuna tatizo katika mfumo mzima wa vyama vya Ushirika, tatizo hilo limefanyiwa kazi, Sheria mpya ya Ushirika imeletwa Bungeni kwako imetajwa kwa mara ya kwanza juzi itakuja humu Bungeni, itakwenda kwa wadau wote na sisi Wabunge ni wadau wakuu wa Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sote kwa pamoja siyo wakulima wa pamba tu, lakini ni pamoja na wakulima wa korosho, wa tumbaku, wa kahawa wote tufanye mkakati wa kuangalia Sheria hii kwa makini ili tuweze kuiboresha zaidi na kuweza kuwawajibisha zaidi viongozi wa Vyama Vya Ushirika ili tupate matunda bora zaidi katika mfumo wa Ushirika na sekta ya kilimo. (*Makofi*)

**MHE. RACHEL R. MASHISHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na utaratibu wa mtu unapoumwa unaenda *dispensary* au hospitali ukiandikiwa dawa

unaelekezwa jinsi ya kutumia dawa hizo. Nilikuwa ninataka kujua Serikali itachukua hatua zippi kwa watendaji ambao wamegawa hizo dawa bila kuwafundisha wakulima jinsi ya kuzitumia? Kwasababu imeonekana kuwa baada ya madhara ndiyo wanaenda kutoa elimu, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema hapo awali kuwa katika kupata matumizi bora ya dawa ni lazima tupitie kwa wagani sasa mkakati wa sasa hivi ni kupitia kwa wagani na watendaji Kata na kadhalika. Lakini tunatenga pia kwamba wale wasambazaji wa ile dawa yenyewe nao ni lazima wabebe dhamana.

Tumeli- *introduce* kwenye zao la korosho kwa mwaka huu unaokuja kwa wale watakaoleta *sulpher* na tutalileta kwenye zao la pamba kwamba wale wanaoleta viuatilifu kwenye zao la pamba pamoja na wale wagani na watendaji Kata na wao wenyewe ambao wanafanya biashara ya ile dawa waweke kipande cha gharama za faida yao au sehemu ya faida yao katika kuboresha elimu kwa wakulima.

**MHE. SELEMANI SAIDI JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa zao la pamba hapa Tanzania limekumbana na changamoto kubwa sana hasa kuhusu suala zima la viuatilifu na kwa kuwa wazalishaji wengi wa pamba kwa vile tunatumia mbegu zetu za pamba kwa vile tunatumia mbegu zetu hizi zimekuwa zikishambuliwa sana na magonjwa na hali halisi wenzetu Duniani hivi wanatumia *Bt Cotton* ambayo ukiangalia *production* yake ni mara mbili ya pamba yetu ya sasa.

Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia wakulima wa Tanzania au inatoa kauli gani hapa Bungeni kwamba tutafanyaje kuingia katika *Bt Cotton*, tukilinganisha kuwa pamba siyo *edible crop?* Ahsante sana. (*Makof!*)

### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Selemani Jafo, kwa sababu tumekwenda Burkinafaso tumeona, Wakulima wale wadogo wa Burkinafaso kwa heka moja ambayo Mkulima wa Mwanza, wa Kwimba, na wa Bariadi anapata kilo mia tatu, mia nne kwa ekari, wakulima hao hao wanapata tani mbili, *two thousand kilos per hectare* kwa kutumia *BT Cotton*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *BT Cotton* ina kitu kimoja kwamba, kwa namna yake katika kuendelezwa kwake inahimili magonjwa zaidi, lakini unatumia dawa mara moja au mara mbili badala ya kutumia dawa mara tano au mara sita. Kwa hiyo, kwa kila tafiti iliyofanywa, wenzetu huko duniani kwa kujua kwamba *BT Cotton* siyo zao la kula, wameendelea na mfumo huo, sisi huku bado tupo kwenye mfumo wa majadiliano baina ya Wataalam, Serikali, Wadau na majadiliano haya yamekuwa yanaendelea sasa kwa muda wa miaka mitatu minne bila kufikia popote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani katika hili nakubaliana na Mheshimiwa Jafo, sisi tumekwenda tumeona jinsi Wakulima wadogo wa Burkinafaso wanavyobadilika kwa matumizi ya *BT Cotton*. Tuache mambo ya siasa na ubinafsi katika jambo hili na Wadau

wote; sisi Serikali, Wadau wa Pamba na Wataalam, tukae tupate ufumbuzi wa haraka ili tuweze kuendelea na matumizi ya *BT Cotton* au pamba ambayo ina ubora zaidi wa mbegu kuliko hizi mbegu tunazotumia sasa ambazo hazimpi tija Mkulima wa Tanzania.

## MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7), wakati Mheshimiwa Mkosamali akiuliza swali lake, alisema maneno kana kwamba Rais alisema uwongo wakati wa kampeni kuhusiana na barabara ili achaguliwe. Rais ni mwongo au Rais alikuwa mwongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka niwakumbushe tu kwamba, Kanuni ya 64(1)(d) inatukumbusha kwamba, Mbunge hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bado tunajifunza na vijana hawa bado wanajifunza, sikuwa na nia ya kumtaka achukue hatua yoyote, lakini nilitaka kumkumbusha. Pia ninakuomba tu kwa Mwongozo wangu kwamba; je, unaweza ukatumia Kanuni ya 72(1) ili angalau kumkumbusha huyu Mheshimiwa Mbunge Kijana ili aendelee kufuata utaratibu na kutukumbusha Wabunge wengine kwa mujibu wa Kanuni ya 72(1), tuendelee kujenga mshikamano na utengamano wa hapa Bungeni kwa kutumia lugha inayokubalika hapa Bungeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hiyo hoja na kukuomba angalau kwa wakati mwafaka uendelee kumkumbusha huyu Mheshimiwa ili atumie lugha inayokubalika Kibunge na pengine na Wabunge wengine wote kwa mujibu wa Kanuni ya 72(1).

## TAARIFA

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, niombe Waziri afute hiyo kauli yake kwamba kuna vijana humu ndani; humu ndani kuna Wabunge na kwa mujibu wa Kanuni hizi wanaitwa Waheshimiwa Wabunge; Mheshimiwa Mbunge Mkosamali au Mheshimiwa Mbunge Tundu Lissu, kuna Waheshimiwa Wabunge hakuna vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kama Waziri amemwelewa vibaya Mheshimiwa Mkosamali, ni bahati mbaya sana. Alichosema Mheshimiwa Mkosamali, alitaka kujuu kama ahadi aliyoitoa Rais kuhusu ujenzi wa barabara Kibondo ilikuwa ni ya uwongo au laa na alikuwa anataka kujuu kwa nini hiyo ahadi haijatekelezwa, ndiyo maana alisema sasa mnataka kusema Rais alisema uwongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kama nimemwelewa Mheshimiwa Mkosamali sawasawa; hakutaka kushawishi Bunge hili kuchukua hatua yoyote dhidi ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, hayo matumizi ya Kanuni ya 64 aliyoisoma Mheshimiwa Waziri, sidhani kama ni sahihi sana. Hakuna kosa lolote ambalo Mheshimiwa Mkosamali amelifanya, lakini kama nilivyoomba kwamba hiyo kauli ya hawa vijana ifutwe ili tuweze kuendelea. (*Makofii*)

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, nilitaka kutoa taarifa kwa Waziri na nilitaka kufanya hivi kwa makusudi kabisa kwa sababu pamekuwa na utaratibu wa mtu kuomba mwongozo kwa kupotosha taarifa ambayo imetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, alichokieleza Mheshimiwa Mkosamali ni kwamba, ahadi iliyotolewa mpaka leo haijatekelezwa na ahadi ile ni ya Mheshimiwa Rais, kwa hiyo alichokiuliza ni kutaka Serikali iseme kama ahadi hiyo ambayo illahidiwa na haijatekelezwa ilikuwa ya uwongo au laa. Kwa hiyo, kitendo cha Waziri kutaka kusema kwamba, Mheshimiwa Mkosamali, aliyekuwa anasema Rais ni mwongo ni kauli ya uchochezi. (*Makofii*)

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, aliyoyasema Mheshimiwa Tundu Lissu na taarifa ya Mheshimiwa Kafulila ni mambo sahihi, mimi sijamtukana Mheshimiwa Rais ila nimeeleza hali halisi ya barabara na kilichotolewa na Mheshimiwa Waziri kwenye majibu yake ni tofauti. Mheshimiwa Rais, aliahidi kujenga barabara hii kwenye Barabara za *TANROAD*, sasa anaponiagiza mimi niwe Karani wa Rais, niende kwenye Halmashauri, wakati Rais ana Makarani wake wa kufuatilia ahadi zake, hilo kwa kweli siwezi kukubaliana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilichokisema ni sahihi na ndiyo maana nikamwambia aeleze kama Mheshimiwa Rais alisema uwongo au hakusema uwongo kuhusu ujenzi wa barabara ile kama itajengwa au haijengwi; ndicho nilichokisema. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika haya ambayo yamezungumzwa asubuhi ya leo, mwongozo wangu ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge sote humu ndani, ni vizuri tukawa waangalifu kwenye kauli zetu, inatusaidia sana. Ndiyo maana kama alivyosema Mheshimiwa Tundu Lissu, sisi tunaitwa kwa kuanzia na neno Waheshimiwa, kwa hiyo, ukishaitwa Mheshimiwa matarajio ni kwamba, ustaarabu wako utaanzia na kauli zako. Kama kauli zinaenda kinyume na neno Mheshimiwa, basi hakuna sababu ya kuitwa Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sote tujitahidi sana kujisitiri katika namna ambavyo tunazungumza. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni ambao tunao humu ndani; katika Jukwaa la Spika tuna Mkuu wa Kanda wa Benki ya *NMB*, Ndugu Gbariel Ole Loibanguti, ambaye ameambatana na Maafisa wengine kutoka *NMB* ambao ni Nazareth Lebi na Arjan Molenkamp.

Karibuni sana Maafisa wa *NMB*, tunawashukuru sana na sisi hapa Bungeni tunashukuru sana kwa huduma ambazo mnatupatia, lakini Wabunge wanasesma bado hamjafunga ATM hapa ya *NMB*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wa Mheshimiwa Richard Ndassa, ambao ni Walimu 24 wa Shule ya Msingi ya Shamariwa iliyopo Igoma Mwanza, wakiongozwa na Afisa Elimu Taaluma, Ndugu Oscar Kapinga pamoja na Mwalimu Mkuu, Ndugu Joachim Kasonka. Wageni kutoka Mwanza, karibuni

sana walimu wote na niwahikishie Mwenyeji wenu Mheshimiwa Ndassa ambaye hapa ni Mbunge Seneta, anafanya kazi yake vizuri sana. Karibuni sana Dodoma. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, huwa nawakumbusha tu watu wa Mwanza kuwa mnapokuwa hapa magari ni mengi, kwa hiyo, muwe makini kidogo barabarani huko.

Wageni wa Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mbunge wa Mbulu ni Ndugu Gervas Sulle, Katibu wa CHADEMA Wilaya ya Mbulu, Ndugu Raphael Ami, *Mbulu Environmental Society* na Ndugu James Kaija. Karibuni sana wageni wa kutoka Mbulu, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, mwakilishi wenu, anafanya kazi nzuri hapa Bungeni. (*Makof*)

Kuna wageni wawili ambao ni Amina Shaban na Kelvin Kitali; karibuni.

Kuna wanafunzi 70 kutoka Shule ya *Aseki Business School* iliyopo Dodoma. Karibuni sana wanafunzi kutoka hapa Dodoma, tunawakaribisha sana hapa Bungeni na tunafurahi sana kuwa pamoja nanyi.

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Munde Tambwe, ambaye ni Ndugu Christina Malasusa; karibu sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo majina pekee ya wageni ambayo nimeletewa hapa mezani.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la Kikao cha Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama,

linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowasa, ambaye anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, wakutane leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa B.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba TV zetu za humu ndani hazioneishi siyo kwamba Ukumbi wa Spika ni *analogy* hapana; hii mitambo ni *digital* yote, ni matatizo tu ya kiufundi ambayo yatarekebishwa muda si mrefu leo. Ninawahakikisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, matangazo mengine yote yanaendelea kwenye runinga mbalimbali kama kawaida. Pia nitoe taarifa kuwa, nimepata malalamiko kutoka kwa Wabunge kadhaa kwamba, baadhi ya sehemu mbalimbali katika Ukumbi wetu panavuja; tunaomba radhi sana kwa hilo, Ofisi ya Bunge inashughulika sana na jambo hilo.

Tumekuwa tukiwashirikisha watu wa Shirika letu la Mambo ya Majengo (*TBA*), ambao ndiyo wahusika wakuu wa marekebisho ya Jengo letu hasa kwenye paa pale na tatizo lao kubwa ilikuwa ni kupata ngazi ya kuweza kufika pale juu na kurekebisha na namna ya kuiingiza hapa ndani na kwa urefu huo. Kwa kushirikiana na Wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tunaamini kabisa kwamba, ufumbuzi utapatikana haraka sana, ambao hivi sasa wapo hapa Dodoma kuona nini cha kufanya. Kwa hiyo, tunaomba subira kwa upande wenu, tuvumiliane jambo hilo linashughulikiwa.

Katibu hatua inayofuata.

## HOJA BINAFSI ZA WABUNGE

## **Hoja ya Mheshimiwa James F. Mbatia Kuhusu Udhaifu Ulioko Katika Sekta ya Elimu Nchini**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Hoja Binafsi ya Mheshimiwa James Mbatia, ambayo inazungumzia udhaifu uliopo katika Sekta ya Elimu Nchini ambapo majadiliano yanaendelea. Mheshimiwa Waziri wa Elimu atafuatiwa na Mtoa Hoja, Mheshimiwa James Mbatia.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii binafsi ya Mheshimiwa James Mbatia. Kwanza kabisa, nitangulize kumshukuru Mheshimiwa James Mbatia, kwa kuleta hoja hii binafsi Bungeni. Hii inathibitisha kabisa uchungu wake katika Sekta hii ya Elimu, ambayo ni adhimu na muhimu kwa Maendeleo ya Taifa letu. Pia yeye ni kama kioo cha Wananchi wa Tanzania, kwa sababu najua Wananchi wa Tanzania wote kwa ujumla wao, wana hisia kali kuhusu maendeleo ya elimu ya watoto wao katika ngazi mbalimbali tangu msingi mpaka elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbatia, kwa kuleta hoja hii bila shaka amechangia harakati na nguvu ambayo tutaendelea kuiweka kuhakikisha kwamba, Mtanzania anafanikiwa kupata elimu bora katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba, katika ukurasa wa 12 wa Kitabu hiki cha Hoja, Mheshimiwa Mbatia, kwa umahiri sana ameleta

hoja yake, lakini amei-back up na utafiti na ningependa kunukuu maneno yake ambayo ameyasema kwamba: "Matokeo ya utafiti nilioufanya kwa takriban miaka 17 sasa na kwa miaka 17, nachukulia kwamba, tangu uhai wa Sera hii ya Elimu na Mafunzo ambayo imeanza mwaka 1995 mpaka mwaka 2012, maana yake ni miaka 17. Kwa hiyo, nasema matokeo niliyofanya kwa takriban miaka 17 sasa yanaonesha kwamba, udhaifu wa mfumo wetu rasmi wa elimu unatokana na mambo makuu matatu." Akayaorodhesha hapo chini:-

Kwanza, ni Sera ya Elimu ya Taifa ya tangu mwaka 1995. Pili, Mitaala ya Elimu ya Shule za Msingi na Sekondari. Tatu, mihtasari ya masomo na vitabu vinavyotumika katika Shule za Msingi na Sekondari. Akataja kwamba, matatizo yake yapo hapa katika maeneo haya makuu matatu na ameyafanya utafiti kwa miaka 17. Natafsiri kwamba, tangu mwaka 1995 mpaka mwaka 2012, ningesema kwa sababu matatizo yapo hapa na kurasa zingine zote zimeendelea kutaja sasa na kufafanua kuna matatizo gani kwenye maeneo haya matatu, basi bila shaka utatuzi wa mambo haya yamo katika kuyafanya kazi masuala hayo husika likitangulizwa namba moja kama alivyoorodhesha Sera ya Elimu ya tangu mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka Bunge lako Tukufu limefanya maamuzi mazuri kwamba hebu tukaiangalie hii Sera ya mwaka 1995 maana ndiyo imenorodhesha katika mambo matatu makuu ambayo yamemtatiza Mheshimiwa James Mbatia. Hili suala la Sera bila shaka ndiyo kubwa zaidi kuliko mengine yote, kwa sababu lile la pili la Mitaala

ya Elimu, Mitaala ya elimu inatokana na Sera ya Elimu. Mitaala inatengenezwa kufuatana na Sera mliyokuwa nayo, Sera inaelekeza nini kiwepo katika elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mihtasari na vitabu inaandaliwa baada ya kuwa na Mitaala ya Elimu. Kwa hiyo, kumbe kiini cha jambo lote hili ni Sera ya Elimu na mafunzo katika nchi yetu. Kwa hiyo, hapa nilikuwa nataka kusisitizia na kulishukuru Bunge Iako Tukufu, kufanya maamuzi kwamba, tuiangalie Sera; Sera ndiyo ambayo itatupa majibu katika matatizo haya ambayo ameyaainisha Mheshimiwa James Mbatia katika kitabu chake akianzia na kusema matatizo yapo wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, yale maelezo ambayo Mheshimiwa Mbatia ameyatoa katika hoja, mengine siyo sawa. Simlaumu kwa hilo, utafiti sehemu nyingine unaweza ukapata majibu mazuri na sehemu nyingine usipate majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ametamka kwamba, Sera hii haikukaa vizuri, lakini hii Sera ina miaka 17 sasa hivi, kwa hiyo, katika uhai wake ni lazima kwa namna moja au nyingine inaweza ikawa imepitwa na wakati, ndiyo maana tunahitaji kufanya mapitio katika Sera hiyo. Miaka 17 siyo midogo, mambo mengi yamebadilika katika miaka 17, lakini uzuri wa Sera hii ndiyo umetufanya leo sisi hapa nchini na Wananchi wa Tanzania wakajivunia maendeleo ya elimu katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja; hapa leo tunapokaa tuchukue Shule za Sekondari mwaka 1995 zilikuwa na jumla ya wanafunzi 196,375 wa Kidato cha Kwanza mpaka Kidato cha Sita, yaani ni tunu kupata nafasi katika elimu ya sekondari. Mwaka 2012 wanafunzi waliokuwa katika elimu ya sekondari walikuwa 1,884,272; wapi na wapi 196,375 na 1,884,272? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio ndani ya Sera hii ya Elimu ya Mwaka 1995 kwa Uongozi wa Serikali za Chama cha Mapinduzi kipindi chote hiki ni makubwa, Serikali za nchi nyingine zinashangaa nchi hii imefanyaje kuweza kupata mafanikio makubwa kama haya. Hata ile kuwa na Sera peke yake ni mafanikio. Nchi ya Bangladesh, Sera ya Elimu wameanza kuwa nayo mwaka jana; nikamwuliza Waziri, imekuwaje hivi? Sisi hatukuwa na Sera ya Elimu kwa mara ya kwanza mwaka jana, ya 1995 imeipokea Sera ya nyuma ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Sera hii imekuwa na mafanikio makubwa siyo tu kwa mfano huu mdogo nilioutoa wa idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari kwamba, sasa hivi siyo kitu adhimu, yaani kuwa sekondari imekuwa tunu, ukimwona unaona kama mungu mdogo huyu, amepataje nafasi ya kwenda sekondari. Hata katika Vyuo vyetu Vikuu, mwaka 1995 kulikuwa na idadi ya wanafunzi 9,042 tu mpaka mwaka jana wanafunzi waliokuwa katika Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki ni 166,488. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, 9,000 hata ungezidisha mara kumi ungefika 90,000. Tumepita kote huko tumeenda kwenye

166,448 na tunaenda mbele na katika MMEJ tumeamua kwamba, tutaongeza idadi ya wanafunzi katika elimu ya juu, tusimwache mtoto wa mkulima au wa mfanyakazi kufaidika na elimu ya juu katika nchi yetu hii. Hayo ndiyo matunda ya Sera hii ya Elimu ya Mwaka 1995 chini ya Uongozi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika awamu mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi katika elimu ya msingi hali kadhalika, mafanikio haya ni makubwa siyo madogo. Sera hii imetufikisha, hatuwezi tukasema ni Sera mbaya kabisa, sasa hivi Mwananchi yejote wa Tanzania atakuwa anacheka kwa mafanikio ambayo tumeyapata.

Wakati wowote ule muda unapopita miaka kumi ikafika 17, mabadiliko ni lazima yawepo. Kwa kazi kubwa kama hii ambayo imeifanya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kazi nzito, kubwa, ukafanya upanuzi wa Sekta ya Elimu kwa kiasi kikubwa mno. Upanuzi ambao kila wakati ulipokutana na Mawaziri wa Elimu, sehemu nyingine wameshindwa kuelewa tumefanyaje, ni lazima utapata athari hapa na pale. Hauwezi kufanya upanuzi wa elimu kiasi hicho halafu kusiwe na athari katika eneo moja au katika eneo lingine hata katika ubora wa elimu. Kwa maana upanuzi huo unataka kuendana pia na uwepo wa walimu, uwepo wa vitabu, uwepo wa maabara, uwepo wa maktaba, vitabu ndani ya maktaba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapopanua nafasi za elimu, ujue kwamba, utaathirika kwa kiasi fulani katika maeneo mbalimbali. Hata ubora wako wa elimu nao unaweza ukaathirika. Kwa hiyo, yale ambayo yametokea ni matatizo

ambayo yanatabirika kabisa katika watu ambao wamejipanga kikamilifu kuhakikisha kwamba, wanaleta maendeleo ya elimu katika nchi yao. South Korea, wamefanya hivyo hivyo; mwaka jana wametufanya semina maalum Mawaziri wote wa Afrika Nchini Burkinafaso katika Mji Mkuu wa Ouagadougou katika ADEA na wakatueleza walichofanya. Walisema tulikimbizana kwanza kupanua nafasi za elimu katika ngazi zote, hatukujali ubora, hatukujali kitu chochote; kwanza, kila mmoja awe shulen halafu ubora tutakuja kuuangalia wakati tuna nafasi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo hicho ambacho tumeanza kukifanya sasa kwamba, tumefika mahali pazuri, nafasi ziko nyingi za kutosha, lakini iangalie Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES – II). Hatutajenga tena Shule za Sekondari kama uyoga kama tulivyokuwa tunafanya miaka mitano hii. *Focus* yetu ni ubora wa elimu. Tunawekeza rasilimali watu na rasilimali fedha kuhakikisha kwamba, tunapata ubora katika elimu katika sekta zetu zote; msingi, sekondari na elimu ya juu; elimu ina gharama kubwa, lakini tumejipanga tuweze kumudu gharama hiyo. Tufanye kazi ambayo inaendana na mahitaji ya Watanzania na mahitaji ya nchi hii kufikia mwaka 2025 kuwa nchi yenye uchumi wa kati. Hatuwezi kuwa nchi yenye uchumi wa kati kama Wananchi wetu hawakuelimika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema hayo kwa sababu kiini ni Sera na kazi yoyote iliyokuwa inafanywa, inafanywa ndani ya Sera. Namshukuru Mheshimiwa Mtoe Hoja, ameleta na akaorodhesha mambo matatu; la juu kabisa

akaliweka Sera. Serikali hii imeshaanza kuifanyia kazi Sera hiyo, imeanza mwaka 2010, imewasilisha kwa Wabunge kwa mara ya kwanza Aprili, 2010 na kwa mara ya pili Novemba, 2011. Kwa sababu Sera ni jambo kubwa, ndiyo maana hata imerudishwa katika Bunge mara mbili. Kauli ya Wabunge, tumeisikia kwa sauti pana kwamba, irudi tena. Sasa mnasema kuwa imefikia mahali imekamilika, mnataka kuipeleka kwenye Baraza la Mawaziri ili iweze kuidhinishwa iwe Sera Rasmi ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kauli hiyo tumeisikia. Ninaahidi kwamba, tutafanya utaratibu kwa maelekezo ya Katibu wa Bunge, namna ambavyo tutaiingiza, lakini tutaingiza Rasimu ya Sera hii katika Bunge linalofuata mwezi wa nne, ikitoka hapa, ndiyo tuipeleke kwenye *Cabinet*. Hiyo tunaitoa kama ahadi na maelekezo ya namna ya kuiingiza tutayapata kutoka kwenye Ofisi ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile tumeanza kuifanyia kazi na Waheshimiwa Wabunge wote wameshiriki, wengi wao kama siyo wote wameshiriki kikamilifu kuikosoa na kuielekeza; ndio kusema kwamba, kumbe jambo hili tuliliona kabla hata haijatoka sauti yoyote kutoka Bungeni au kutoka mahali pengine na tukaanza kuifanyia kazi. Tumeifanyia kazi kwa muda mrefu kwa sababu ya umuhimu wake. Kwa hiyo, tutaendelea kulikamilisha jambo hili ili haya yote matatu kwa sababu kiini chake ni Sera kama Mtoa Hoja alivyoonesha, yawe yamekamilishwa na tuanze kwenda katika mustakabali ambao tunapata elimu ile ambayo nchi hii imeihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limezungumziwa kuhusu Taasisi ya Elimu ya Tanzania kwamba, Taasisi mbona inalegalega? Mbona imenyang'anywa majukumu? Mbona haifanyi kazi yake; haiandiki vitabu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilieleze tu Bunge lako Tukufu kwamba, Taasisi hii imeundwa kwa Sheria Namba 13 ya Mwaka 1977. Katika majukumu yake ni pamoja na kuunda Mitaala ya Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari na Elimu ya Ualimu. Jukumu la Mitaala ni la Taasisi, jukumu la Mihtasari ni la Taasisi na pia kuandaa vifaa vya kufundishia kama uandishi wa vitabu na Taasisi hii kazi hiyo inaifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtoa Hoja amesema hakuna Mitaala, Mitaala nimeionesa. Mtaala wa Elimu ya Sekondari 2005 ninao, Mtaala wa Elimu ya Sekondari A - Level 2009, huu hapa.

(Hapa Mheshimiwa Waziri alionesa Mitaala husika)

#### **WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, juu yake utaona umeandikwa *Tanzania Institute of Education* au Taasisi ya Elimu. Kazi hiyo wameifanya; 2005, 2009, 2010, nimeonesha mifano ya Mitaala mingine ambayo Taasisi imeandika, lakini haiishii hapo tu, Taasisi ikishatoa Mitaala ni dhima yao kuandika Mihtasari, kazi ambayo wanaifanya. Huu Muhtasari wa *Basic Mathematics*, umeandikwa *Basic Mathematics Syllabus for Secondary Schools* Mwaka 2010. Muhtasari huu ni wa Taasisi ya elimu. Muhtasari wa *Jiografia* huu hapa wa 2010. Muhtasari wa *Civics 2010, Teachers' Guide 2011*

*Civics*, ambayo imeandaliwa na Taasisi. Kazi hii Taasisi imeendelea kuifanya mwaka hadi mwaka kwa kutimiza majukumu ambayo imepewa na Taifa hili na wala Taasisi hii haijawekwa nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tuko katika mchakato baada ya Mheshimiwa Rais, kutoa maelekezo kwamba, kitabu cha kufundishia kwa somo moja kiwe ni kitabu kimoja cha kiada nchi nzima. Hatujafika hapo, tumechagua vitabu viwili kwa kila somo kwa kila darasa kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba, lakini tuko njiani kwa ajili ya kitabu kimoja cha kiada kwa kila somo. Taasisi imeshajipanga, imeshaanza kazi hiyo, ipo katika maandalizi na sisi tutawawezesha kifedha ili kazi hiyo waitimize kwa sababu ni maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hatuna namna nyingine ya kufanya zaidi ya kuhakikisha tunatimiza mustakabali ule wa kuhakikisha kwamba, nchi yetu inakuwa na elimu bora na Taifa hili litapiga maendeleo tu kwa kutegemea rasilimali watu yake. Rasilimali watu ambayo imeelimika, ina kisomo ambacho kinaendana na nia ya kuwa nchi hii iwe ni nchi yenye uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba, jambo hili siyo jepesi ni zito, kubwa, lina gharama, gharama yake ni kubwa mno na ni lazima Bunge hili lijpange kwa ajili ya kutoa *resources* kuruhusu Serikali iidhinishe kuweka mafungu makubwa zaidi katika Sekta ya Elimu. Haya yote hatuwezi kuyafanya kwa pesa ndogo ambayo tunaipata katika Sekta hii ya Elimu. Katika bilioni 384 ya OC ya Wizara ya Elimu, bilioni 326 ni mikopo ya wanafunzi na wala siyo wote ambao wanapata mikopo ya wanafunzi; hela haitoshi,

hamna namna ambayo tutaweza kuboresha tutakayoyaboresha bila ya kuwa na rasilimali fedha katika nchi yetu ama kutoka katika vyanzo vyetu wenyewe ama pesa ambazo tunaweza kuzipata kutoka kwa Wahisani.

Pesa ambazo tunazitumia sasa hivi katika Sekta ya Elimu, zinazofikia shilingi trillioni mbili kwa ujumla wake, maana tusiangalie tu zile ambazo zinakuja katika Wizara ya Elimu, tuangalie zinazokwenda TAMISEMI na katika Wizara nyingine ambazo nazo zinasimamia Taasisi za Elimu. Shilingi trillioni mbili bado hazitoshi kutufanya sisi tuweze kupata ubora huo ambao tunautaka. Bunge lijipange vizuri kubuni, ni rahisi kusema tuongeze ubora, lakini tunafanyaje; tunapata wapi hizi nyenzo? Mawazo ya Wabunge nayo yatasaidia; Serikali, ina jukumu hilo lakini mawazo ya Wabunge nayo kama Wawakilishi wa Wananchi, yatasaidia kusema pesa hizi tutazipata wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema niyafafanue haya ili tuelewe jukumu ambalo lipo mbele yetu na tuelewe tulikotoka na kule ambako tunaeleke. Tunaenda sehemu nzuri na Serikali hii ni imara na Serikali mahiri, inafanya mambo kufuatana na mahitaji na nina uhakika kwamba tutafika pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda wangu hautoshi ni mdogo, lakini niseme upande wa ukaguzi tunauthamini sana na tumeshaanza mchakato wa kufanya ukaguzi uwe wakala. Kwa hiyo, suala hili la ukaguzi kuwa *independent*, tayari Serikali imeidhinisha kwamba, iwe hivyo lakini namba mbili, tumeshaanza mchakato wa kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho ya maslahi ya Walimu; tunawajali sana Walimu, tunawathamini mno, hakuna elimu bila ya Walimu. Asibabaike Mwalimu yejote katika nchi hii kusema kwamba, Serikali hii haiwajali Walimu. Hivi sasa tuko katika majadiliano tayari ya kuangalia namna ambavyo tutaweza kuboresha maslahi yao. Wameleta mapendekezo, lakini nimelizungumzia suala la rasilimali fedha ambalo ni muhimu sana. Huwezi kuwa na motisha kubwa na mishahara mikubwa kama hela zenyewe huna. Kwa hiyo, tutakaa nao na tutaendelea kukaa nao ili tuwe wawazi kati yao na Serikali, kuwaonesha kipi kitawezekana na kipi hakiwezekani; hamna kitu cha kuficha hapa, lakini wajue kabisa kwamba, tunawathamini. Kwa sababu, tunathamini elimu, tunawathamini Walimu na tutahakikisha tunafanya kila linalowezekana kuondosha vikwazo na madhila kwa Walimu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EMAC* imelalamikiwa, tumeyasikia na ipo chini ya Waziri, tutachunguza madhila yote ambayo imefanya, tutachunguza mfumo wake na utendaji wake wa kazi. Ikithibitika matatizo makubwa ambayo Mheshimiwa Mtoa Hoja ameyatoa, nitaivunja *EMAC* na kuipanga upya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za rada tumezipokea.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana, nashukuru.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja iliyoko mbele yetu. Kabla sijafanya hivyo, ninaomba Mwongozo wako; kwa kuwa baadhi ya niliyoyasema kwenye hoja yangu, suala la Mitaala limeibuka na nikasema Mitaala Rasmi; na Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anajibu jana akasema Mitaala hiyo ipo. Nimemwandikia jana nikimwomba anipatie nakala mimi Mtoa Hoja sijaipata; leo nimekutana nae akaniambia atanipatia baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *Hansard* inarekodi, ningeomba alete kopi ya Mitaala aliyoitoa jana Mezani kwako ili niweze kupata kopi ya huo Mtaala nijiridhishe, niweze kuweka Kumbukumbu za Bunge sahihi niweze kuendelea na majumuisho ya hoja hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia, nimelipokea hilo, ninaendelea kulitafakari, wewe endelea kuhitimisha Hoja yako.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kiti chako kitende haki; mimi nimeshutumiwa kwamba, nimelidanganya Bunge kuwa Mitaala Rasmi haipo. Sasa kwa kuwa mimi nimesema uwongo hapa, ninataka nidhihirishiwe uwongo wangu. Naomba kama anayo Mitaala Rasmi ya Taifa hili, aniwekee Mezani niione ili niweze kuendelea; nijiridhishe, niweze aidha kuomba radhi au niseme vinginevyo kuhusu suala la Mitaala hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwa shida gani?

**NAIBU SPIKA:** Kwa hakika unanichanganya kabisa; uwongo wa kuhusu nini; yaani *I am completely out of place?* Kwa sababu, hii ni fursa yako kufuatana na Kanuni na Utaratibu tuliojiwekea humu ndani wa wewe kuhitimisha hoja yako na una saa nzima ya kufanya hivyo na mnajua katika ratiba ya leo tuna hoja nyingine inatakiwa kuingia tena.

Sasa unapoanza na kitu kingine ambacho ni tofauti tena, unanipa tabu sana. Wakati uwanja ni wa kwako na kwa michango ambayo Waheshimiwa Wabunge, wamekupatia tangu jana na ushirikiano mkubwa ambao umeupata, mimi ninaamini ni mchango tosha kabisa kwa wewe kuweza kuhitimisha hoja yako.

Kwa hiyo, kwa mara nyingine nakupa nafasi. (*Kicheko*)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali na Mheshimiwa Nassari na ningeomba asiongezeke mwingine ili baada ya hapo tuweze kuendelea.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulipatia Bunge lako taarifa kwamba, katika Bunge lililopita la mwezi Novemba, 2012 na tukirejea Taarifa za Bunge kwa maana ya *Hansard*, Naibu Waziri wa Elimu, aliahidi kwamba, watakuja kutupatia nakala za kitu

kinachoitwa Mitaala au Mtaala wa Elimu Nchini. Sasa leo inapokuja kujitokeza kunakuwa na hali ya Wizara kusita kutugawia nakala Wabunge na Mtoa Hoja ameomba apewe nakala hiyo, nafikiri haki haitendeki.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nakiomba Kiti chako kiiagize Serikali kupitia Waziri wa Elimu, watoe nakala hizo kama walivyoahidi; sijui kumetokea kigugumizi gani mpaka dakika hii!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi sipendi sana maneno ya kusema haki haitendeki na vitu vyatya namna hii kila wakati, siyo jambo jema sana kila wakati kuhisiana na kuona kama vile wako watu ambao wanapendelewa. Hoja yako Mheshimiwa haina kipengele hicho, kama ni kitu *specific*, hoja yako inaeleweka, kila mtu ana nakala ya ile hoja, sasa ni wakati wa kuhitimisha ile hoja siyo wakati wa kuzunguka na kitu kingine katikati tena kukiwekea masharti.

Pili, ameniomba mwongozo na Kanuni zetu zinasema Mwenyekiti au Spika atakayekuwa hapa, anaweza kutolea ufanuzi wakati huo huo au wakati mwingine atakaoona unafaa. Mimi nimesema nitatoa mwongozo wangu baadae, sasa kuoneana na nini kunatoka wapi! Haya Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kwa sababu ya muda na kwa ruhusa yako, naomba nisiisome ni Kanuni maarufu inafahamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyopo mbele yetu ya Mheshimiwa James Mbatia kuhusu udhaifu uliopo kwenye Sekta ya Elimu na mionganini mwa mambo ambayo aliyazungumzia Mheshimiwa James Mbatia jana, suala kubwa lilikuwa la Mitaala. Kama alivyozungumza Mbunge aliyetangulia, Mheshimiwa Moses Machali hapa kwamba, mwaka jana Serikali iliahidi kuleta nakala ya Mtaala wa elimu kwa Wabunge na wakasema kwamba, Mitaala ipo tangu mwaka 2005. Tunavyofahamu sisi au mimi binafsi na jana Mheshimiwa James Mbatia alilizungumza tena hapa na yeye kama Mbunge nafikiri anapenda liwekwe *clear* ili ajisafishe asije akaonekana kwamba yeye ni mwongo. Sasa, tunapaswa kujua nani mwongo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyofahamu ni kwamba, Mtaala wa elimu upo kwenye rasimu na umeandikwa Chapa ya Kwanza mwaka 2012 na huku tunaambiwa kwamba Mtaala wa elimu upo tangu mwaka 2005. Anachosisitiza Mheshimiwa James Mbatia hapa ni kwamba, sisi kama Wabunge au yeye ili aweze kuendelea na hoja yake, apewe nakala ya Mitaala ya elimu ya Tanzania, huo wa mwaka 2005 na Wabunge wote tulipo hapa tupewe nakala tuweze kuona ili aweze kuendelea na hoja yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassari, naona unarudia rudia, nimeshakuelewa.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Nikishasimama unakaa, ndiyo utaratibu. Naomba Mheshimiwa James Mbatia, urudie maneno yako, unataka Kiti kifanye nini *as such* na kwa kutumia Kanuni ipi ili nikuelewe?

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikitumia Kanuni ya 68(7) inasema, hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambao hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadiri atakavyoona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Kanuni ya 5 inasema kwamba, katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika lbara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazitakuwa na mwongozo, basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge, pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mwenye hoja ni mimi, nilisemea suala la Mitaala rasmi hakuna. Wadau mbalimbali wamesema hivyo. Tarehe 30 Novemba, 2012 nillleta swali Bungeni, naomba nirejee *Hansard* ya Bunge lako Tukufu wakati nauliza swali la nyongeza tarehe 30 Oktoba, naomba kunukuu kwa ruhusa yako.

"Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameliambia Bunge lako Tukufu kwamba, Mtaala unaotumika sasa ni ule wa mwaka 2005; na kwa kuwa kuna hisia kwenye jamii kwamba, Mitaala hii imekuwa ni jambo la siri wakati elimu siyo jambo la siri, siyo jambo la kuficha; je Mheshimiwa Waziri anaweza kuleta Mitaala hii kila Mbunge apate *copy* yake katika Mkutano huu wa Bunge ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufuatilia Mitaala hii kwa urahisi katika Shule za Sekondari na Shule za Msingi?"

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alijibu hivi; kwa ruhusa yako naomba ninukuu ile sehemu aliyojibu alisema: "Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge, anapenda kuliomba Bunge lako Tukufu liridhie Wizara ya Elimu isambaze Mitaala kwa kila Mbunge kwenye Bunge hili. Mimi sina matatizo na hilo, lakini basi niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, Bunge lijalo tutachapisha Mitaala hiyo ya elimu ya mwaka 2005, tutawagawia Wabunge waone kuna nini ndani yake (*Content*), halafu baadae tuje tuone namna walimu wanavyochukua Mitaala kwenda kwenye mihtasari (*Curriculum to Syllabus*), ndipo angalau tutaweza kuelewa jambo halisi."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo kwamba limeanza janam nimeliomba tangu tarehe 30 ya mwezi Oktoba, 2012 na isitoshe nina hoja hapa nimeandika naiomba na jana nimeoneshwa hapo sasa nikasema naomba nijiridhishe tu kwamba, Mitaala ipo nifute kauli yangu ambayo ipo kwenye hoja ili tuendelee mbele na nilitamka Mitaala rasmi; sasa tatizo liko wapi, kama anayo mwambie alete Mezani hapo huo ushahidi basi ili nifute kauli yangu na hata alipokuwa anaongea hapa

ameonesha Mitaala ipo, tuone sasa hiyo Mitaala rasmi ya mwaka 2005.

**NAIBU SPIKA:** Tukumbuke tu kwamba, tunaendelea na majumuisho yako, ndiyo *style* uliyoichagua ya majumuisho; kwa hiyo, ule muda wako unaendelea na Katibu tuendelee hivyo. Sasa hivi tumeshakula robo saa katika saa yako moja, ni njia ambayo umeichagua. Nilikuona Mheshimiwa Tundu Lissu, kabla sijasema chochote.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Hoja anayoitoa Mheshimiwa James Mbatia ni ya msingi sana; Bunge hili liliahidiwa mwaka jana kwamba, litaletewa nakala za Mitaala haijaletwa mpaka tunapozungumza hapa. Mheshimiwa James Mbatia, amezungumza jana kwamba, kwa vile Mitaala haijaletwa maana yake haipo. Waziri aliyeahidi kwamba mwaka jana angeleta Mitaala kwa Wabunge wote, ametuonesha vitu ambavyo anaviona yeye, Wabunge aliowaahidi atawaletea hajatuletea maana yake ni kwamba, *record* ya Bunge lako Tukufu itaonesha kwamba, Mitaala haijaletwa kwa Wabunge, haijagawiwa kwa Wabunge kama alivyoahidi Waziri na Waziri atekelze kile alichokiahidi ili Bunge lako Tukufu liweze kuamua kama Mheshimiwa James Mbatia amekosea Kanuni ya 64(1)(a) inayokataza Mbunge kutoa taarifa zisizokuwa na ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni neno la Mheshimiwa James Mbatia kwamba, hakuna Mitaala au neno la Mheshimiwa Waziri kwamba Mitaala ipo na mwenye kuthibitisha ni Waziri aache kutubabaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni Naibu Spika wa Bunge hili na kazi ya Bunge ni kuisimamia Serikali, naomba utusaidie Waziri alete Mitaala kama alivyoahidi waache kufanya Bunge kutupuuza sisi Wabunge. Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Sasa nikishasimama Mheshimiwa Wenje si tunakwenda kwa zamu jaman! Mheshimiwa James Mbatia, tatizo kubwa ulilonalo katika suala lako siyo *presentation* ya ulivyoliweka, tatizo ni njia ulivoitumia, umetumia njia ya Mwongozo wa Spika, lakini Mwongozo huu unanilazimisha mimi lazima nifanye unavyotaka na kwa wakati unaotaka wewe; hilo ndiyo tatizo liliopo.

Umetaka mwongozo kwangu na kanuni inaniambia nitatoa mwongozo ama papo hapo ama baadae kadiri nitakavyoona inafaa na ili nitoe mwongozo lazima niwe nimetafakari nimefikia mahali pa kusema sasa mwongozo unaofaa ni huu. Mimi nipo katika kutafakari wewe unanigomea unasema lazima wakati Kanuni haziko hivyo.

Pili, Waheshimiwa Wabunge hivi tangu lini utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni unazuia hoja za Bunge? Kwa hiyo, ninachokioomba Mheshimiwa Mbatia uniachie. Naona Mchungaji ameshasogea hapo nani, Mheshimiwa Moses Machali eeh, samahani Mchungaji samahani, nakuomba Mheshimiwa James Mbatia uhitimishe hoja yako. Hoja yako ni ya msingi, ni hoja muhimu kwa Taifa, uchukue muda huu na fursa hii kuhitimisha hoja yako ili baada ya hapo tuweze kuona tunaendelea vipi. Kwa mara nyingine tena, kwa mara ya tatu, nakuomba Mheshimiwa James Mbatia uhitimishe hoja yako.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni Watanzania na sisi chombo hiki tunakiita Bunge Tukufu, utukufu asubuhi ya leo kwa ruhusa yako ninaogopa sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize vizuri ndivyo anavyohitimisha hoja yake, ndiyo *style* anayoitumia. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu, atatuhukumu hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umesema Eee Mwenyezi Mungu, Mtukufu, Muumba Mbingu na Dunia, umeweke katika Dunia Serikali za Wanadamu na Mabunge ya Mataifa ili haki yako itendeke, twakuomba uibariki nchi yetu idumishe Uhuru, Umoja, Haki na Amani, umjalie Rais wetu hekima, afya njema na maisha marefu ili pamoja na wanaomshauri ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia, hiyo husomwa na Spika tu siyo mtu mwingine tena, sasa hapo unajibadilisha kuwa Spika, yaani leo unavua madaraka yangu yote Mheshimiwa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasoma Kanuni za Bunge lako Tukufu.

**NAIBU SPIKA:** Naomba uendelee lakini hiyo hebu iache.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumesema kwamba, utuongezee hekima na busara sisi

Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utupe uwezo wa kujadili kwa dhati mambo yatakayoletwa mbele yetu leo ili tufanye maamuzi sahihi, yenye manufaa kwa watu wote na ustawi wa nchi yetu; amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndivyo tulivyomwomba Mwenyezi Mungu siku ya leo asubuhi. Sasa nakuwa na moyo mzito na ninasema nakuwa na moyo mzito kwa sababu hili ni suala la Watendaji; nashindwa kuelewa kwa nini Viongozi Mawaziri walinde uovu wa Watendaji na ninapotamka Mitaala Rasmi ni kwa ajili ya Taifa hili la Tanzania siyo kwa ajili ya watoto wa James Mbatia. Suala la elimu mbele ya haki hakuna CCM, CHADEMA, CUF, tutaulizwa matendo yetu mema tuliyowafanyia Waja wa Mwenyezi Mungu tulipokuwa hapa Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoomba haki tu itendeke, hoja iliyoko mbele yetu ni Mitaala, humu Watanzania jana umewaambia hapana. Mheshimiwa James Mbatia, amesema hakuna Mitaala, Serikali imesema Mitaala ipo na bahati nzuri imeoneshwa Bungeni. Sasa mimi Mtoa Hoja naomba Mitaala hiyo inaonekana haitakiwi. Sawa, je, nitumie busara gani?

Nikijaribu kuangalia hekima gani nitumie nashindwa; je, busara inatawala nashindwa kuelewa na ni jambo la kiungwana tu na sikuanzia kwako, nilimwandikia Waziri tangu jana. Sasa kama Mbunge sipati huo Mtaala; je, Mtanzania gani atakayeona hiyo Mitaala?

Mheshimiwa Naibu Spika, ngumu kweli kweli na ninasema kwa moyo wa dhati na hili sikuanza leo wala juzi, tangu mwaka jana Mheshimiwa Waziri anajua nimeshafika kwenye ofisi yake na nimeshaomba Mitaala kwa Watendaji wake. Sasa hiyo Taasisi ya Wakuza Mitaala inafanya nini; kwa nini tunailinda? Kwa nini tunaendelea kulisha sumu watoto wetu wa Tanzania uozo huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumwogope Mwenyezi Mungu, kwa moyo wa uchungu kabisa acha nihukumiwe kwa matendo yangu na hili nalifanya *above political ideologies*, suala la elimu halina itikadi ya chama. Taifa hili linapoangamia, vurugu zinazotokea kila mahali na sikuanza kuyasema haya leo; Mheshimiwa Kabaka alipokuwa Naibu Waziri wa Elimu ya Juu, tuliyazungumza haya tarehe 14 Oktoba, 2006, Siku ya Jumamosi, kwenye Ukumbi wa Manispaa ya Kinonodoni na nilipotoa takwimu pale mkasema labda anafanya uchochezi; hapana na nikasema namna gani tuondoe tofauti hizi zilizopo za kielimu ndani ya Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008, tarehe 30 mwezi Novemba, Siku ya Jumamosi, nilitoa Kitabu nikisema tunataka kukumbatia giza au nuru sisi Watanzania kwa maslahi ya Watanzania wote. Mama yangu mzazi, marehemu, Mwenyezi amuweke mahali pema, aliniambia kichaka kilichokuhifadhi usikitie moto. Tanzania yetu hii ambayo tumekulia sote, mama yangu Philomena tusiitie moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Tanzania ni yetu sote, kwa nia njema elimu ndiyo itakayokuwa mkombozi wa Taifa la

Tanzania na elimu hii tunayoizungumzia lazima tuwe wa kweli, watoto wetu humu ndani hawapati elimu hii, watoto wetu wapo kwenye elimu nyingine tofauti na hawa tunaowazungumzia. Sasa hii Mitaala inayolishwa watoto wetu, jana sijalala nilikuwa ninachambua hoja za Wabunge, wameniandikia zaidi ya 36, Mwenyezi Mungu awabariki, nimepata *message* zaidi ya 167, kule Muleba Kusini kwa Mheshimiwa Anna Tibaijuka hali ni mbaya, watoto 70 wanasoma kitabu kimoja, nimeongea na Mwalimu Philemon.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ambayo inaendelea katika Taifa letu, tusilifanye Taifa letu lifikie mahali pa kuasi. Ninachoomba, sisi tulipo hapa tukiwa Wabunge, Ibara ya 63(2) ya Katiba inatutaka tushauri na kusimamia utendaji wa Serikali. Sasa Watanzania waliotutuma humu ndani hivi tunajisikiaje Mheshimiwa Rais wetu anaposimama anasema Mitaala yetu inatuongoza hivi na hivi, Mheshimiwa Rais tunampa heshima wakati hiyo Mitaala anayoitamka hatuioni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, anahitimisha mara kwa mara Mitaala yetu iko hivi na hivi; hiyo Mitaala hatuioni! Kuna Taasisi mbalimbali zinazokosoa Mitaala ya Tanzania, tunanuka huko nje ya nchi, wanapewa fedha nyingine hiyo Mitaala iko wapi? (*Makof*)

Mbunge nimetoa hoja jana hapa, nikaambiwa Mitaala hiyo ipo, sasa ninaiomba iko wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu, ningeomba nitoe mfano, Mitaala hiyo hiyo *syllabus*

aliyokuwa anaisema pale ya mwaka 2010 imeandikwa hii hapa. Hiyo Taasisi ya Elimu inayosifiwa hapa imeandikwa *Advanced Mathematics Syllabus for Advanced Level*, *Mathematics Syllabus for Advanced Level*. Hivyo vitabu anavyovisifia anaanza badala ya kuanza na *Mathematics Syllabus for Advanced Level*, anaanza na *Advanced Mathematics Syllabus for Advance Level*. (Makofi/Kicheko)

Ndiyo hii iliyokuwa inatetewa pale ya 2010, siyo ya kwangu jamani Waheshimiwa!

**MBUNGE FULANI:** *Shame.*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Kweli siyo ya kwangu ni ya Taasisi ya Elimu ya Tanzania hii hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ...

**NAIBU SPIKA:** Hicho ni kitu gani Mheshimiwa Mbatia?

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Ni muhtasari. *The United Republic of Tanzania, Ministry of Education and Vocational Training, Advanced Mathematics Syllabus for Advanced Level Secondary Education, Form Five to Form Six*. Ndiyo wanayolishwa watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyo vitabu sanduku zima hapa.

**NAIBU SPIKA:** Kuna shida gani katika hilo; sijaelewa hiyo *title* ina shida gani?

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Ninachosema, Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni msomi umesoma na nitaleta mbele yako na naamini unajua kimeandikwa *Advanced Mathematics Syllabus for Advanced Level*, hapa intakiwa iwe *Mathematics Syllabus for Advanced Level, advanced, advanced*, mara mbili hapa juu kwenye cover!

**NAIBU SPIKA:** Hatuwezi kubishana, sijui sana sina nakala, lakini wewe umesoma hesabu na mimi nimesoma, katika hesabu kuna advanced mathematics lakini kwa sababu ni muda wako wa kujadili hebu endelea tusichukue muda wako.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado nilikuwa naomba mwongozo sijaanza kujadili hoja.

**NAIBU SPIKA:** Jadili hoja, endelea Mheshimiwa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Sijaanza kujadili nilikuwa naomba Mitaala.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia, hujipangii, ninayepanga ni mimi, unajadili hoja endelea.

**WABUNGE FULANI:** Aah!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa unyenyekevu unitendee haki nahirishe hoja yangu mpaka nitakapopata Mitaala ndiyo niweze kutoa hoja yangu. (*Makofi*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nimewaona mmeunga mkono hoja, lakini kabla sijasema chochote ingawa hukusema Kanuni namba ngapi unaitumia katika kuahirisha hoja yako; Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbatia ananukuu Hansard ya Bunge liliopita kwamba, Serikali iliahidi kuleta kwa Waheshimiwa Wabunge nakala za Mitaala katika Bunge hili; na kwa kuwa Mkutano wako huu unaisha tarehe 8; kwa niaba ya Serikali nilikuwa nataka kukuhakikishia kwamba, ahadi hiyo iliyotolewa na Waziri wa Elimu kwa niaba ya Serikali, itatekelezwa kabla ya kukamilika Mkutano huu tarehe 8, maana leo mkutano haujaisha. (*Makofii*)

Kwa mujibu wa *Hansard* aliyoisoma, kama aliahidi kuileta Bunge hili, Bunge hili linaisha tarehe 8, Mtaala huu ameusoma jana, alikuja na kopi moja hazikutosha kwa Wabunge wote. Ninataka kusema kwamba, ahadi aliyoisema humu ndani ambayo imenukuliwa kwenye *Hansard*, itatekelezwa kama alivyokuwa ameahidi katika Mkutano huu. (*Makofii*)

Kwa kuwa nakumbuka jana Mheshimiwa Mbatia alisema nakala za Mitaala zikitolewa, yeye yuko tayari kujiuzulu, sisi hatutaki afkie kujiuzulu, hatupendi kufikia huko.

Ahadi yetu sisi tabia hii mpaka Bungeni, mtaani mpaka Bungeni, hatupendi tufikie huko lakini tunachosema tunataka kwa heshima kabisa, Mheshimiwa Mbatia ambaye ni muungwana sana, ahadi iliyotolewa na Waziri itatekelezwa kabla mukutano huu haujaisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kabla hatujaendelea, namwomba Mheshimiwa Mbatia ili nitende ile haki ambayo ameirudia sana na wenzake, anieleze tu kwamba ile hoja yake ya kuahirisha ameitoa kwa kutumia Kanuni gani ili vinginevyo basi tuachane nayo, maana hakutamka Kanuni yoyote ile. Ninakupa dakika chache sana unieleweshe katika hilo ili tufanye maamuzi. Kwa vile hata Kanuni yenyewe haijulikani, mimi naendelea na utaratibu uliokuwepo Mezani.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Nikishasimama wote mnakaa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia Kanuni ya 69...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia, nimesimama.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Si umenipa dakika tatu za kuangalia hii Kanuni sijaishia hata dakika moja haijaisha Naibu Spika. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Unatakiwa ujipange vizuri mzee, haya endelea.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, uliniambia dakika tatu hata moja ilikuwa haijaisha. Naomba kutumia Kanuni ya 69(1), Mbunge anayepanda mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja kwamba, mjadala sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisoma Kanuni ya 55(3)(b) inasema, hoja zifuatazo zinaweza kutolewa bila taarifa; kuahirisha Bunge au kuahirisha mjadala. Naomba vyote kwa pamoja, kwa sababu nilishatoa hoja hiyo na nilichokuwa naomba tangu mwanzoni, ningepata hata ile nakala ya jana basi nijiridhishe halafu Bunge liendelee, kwa sababu nimeshaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Kwa kuwa umeshanipa Kanuni, huo ndiyo utaratibu wetu Bungeni jamani wala siyo kwamba mtu anaonewa wala nini; unapozungumza jambo kama hilo, basi unatoa Kanuni.

Kanuni ya 69(1) ipo *in order* lakini ya pili inasema; kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja ni kinyume cha uendeshaji wa shughuli za Bunge, atakataa kutoa hoja hiyo ili iamuliwe vinginevyo, papo hapo

atawahoji Wabunge juu ya hoja hiyo kadiri atakavyoona inafaa. Kwa hiyo, ninachoona inafaa, ninaikataa hoja hiyo, kwa hiyo, tunaendelea na shughuli. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Shughuli inayoendelea ni hii ifuatayo; Waheshimiwa Wabunge, ninapokuwa nimesimama mnaongea, mbona mnapokuwa mnaongea ninyi mimi nakaa nawasikiliza!

Waheshimiwa Wabunge, kinachoendelea sasa ni kuwahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa James Francis Mbatia ya Udhafu Uliopo katika Sekta ya Elimu pamoja na mabadiliko yaliyofanyika jana.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Udhafu Uliopo Katika Sekta ya Elimu illafikiwa na Bunge pamoja na marekebisho yake)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo imeafikiwa. (*Makofi*)  
**Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangala ya Kuitaka Serikali Serikali ianzishe Mpango Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana kwa Kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana Wanaowekeza Kwenye Kilimo na Viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo**

**MBUNGE FULANI:** Utaratibu Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala, endelea na hoja yako hapa hapa ulipo.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Nakuomba Mheshimiwa Machali, sasa ni Mheshimiwa Kigwangala anaongea.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA:** Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Viumbe Vyote, aliyetujalia pumzi na kutupa afya safi, nguvu na uwezo wa kufika hapa siku hii ya leo na zaidi kuniwezesha mimi kupata fursa hii adhimu na adimu sana kuwasilisha hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Nakushukuru sana wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Makatibu, kwa msaada katika kuwezesha uwasilishaji murua wa hoja hii siku hii ya leo.

Kwa namna ya kipekee, namshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge na pia Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM, kwa ushauri na ushirikiano alionipa wakati nikiaandaa hoja hii. Pia bila kumsahau Mheshimiwa Hussein Mzee Mbunge na Mtunza Hazina wa Kamati ya Wabunge wa CCM na Watumishi wote wa Ofisi yetu ya Kamati ya Wabunge wa CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie fursa hii, kuwashukuru Wananchi wa Nzega, kwa kuendelea kuniunga mkono katika harakati zetu za kuleta Mapinduzi ya Kiuchumi na Kijamii katika Jimbo la Nzega. Wananzega ni mashahidi na wafaidika wakubwa wa Miradi ya Kilimo cha pamba, alizeti, miembe ya kisasa ya SUA na sasa tunaingia kwenye uzalishaji na ufugaji wa kuku.

(*Hapa Wabunge fulani walipiga kelele*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangala, endelea kutoa hoja yako kwa sababu muda wako unakwisha.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA:** Miradi ambayo ilibuniwa kwa ushirikiano baina ya Wananchi wa Nzega na Mbunge wao, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala, ambaye pia ni Mwenyekiti Mwazilishi wa Shirika la Maendeleo Nzega, yaani *Nzega Development Foundation*, kwa kutumia nadharia zinazofanana kwa ukaribu kabisa na mapendekezo yanayowasilishwa kwenye hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe wangu kwa Wananchi wa Nzega ni kwamba, nawaomba wasiteteleke.

**NAIBU SPIKA:** Nawaomba Wabunge mnaoondoka mwondoke taratibu na *Sergeant-at-Arms*, Mbunge yeoyote anayepiga kelele hebu mshughulikieni. Endelea Mheshimiwa Kigwangala.

**MHE. HAMISI A. KIGWANGALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe wangu kwa Wananchi wa Nzega ni kwamba, naomba wasitetereke, pamoja na jitihada za

Wapinzani wangu kisiasa kupotosha ukweli, jambo ambalo halijawahi kufanikiwa. Ni imani yangu kwamba, Wananzega wenyewe wanajua dawa ya hawa wasaliti ya maendeleo ya Nzega.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Ubunge ni ngumu sana, ina changamoto nyingi kubwa kwa Mbunge Kijana kama mimi ni muda wa kusoma, muda wa kuzaa, muda wa kulea na muda wa kutekeleza majukumu ya kiuwakilishi. Nitumie fursa hii, kumshukuru mke wangu, Dkt. Bayuni na pia nimpe pole kwa uchungu anaoupata huko *labor ward*, ambapo anategemea kujifungua mtoto wa kiume, ambaye nitampa jina la *HK Junior* na mabinti zangu Sheila na Hawa Kigwangala, kwa kuendelea kunivumilia kila siku ninapokuwa *busy* kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa na Kijimbo. Wote ninaomba wadumishe upendo na uelewa kwangu wakitambua kuwa ninawapenda na mara zote nawakumbuka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ama baada ya shukrani, naomba sasa nianze kuiwasilisha hoja yangu rasmi kama ifuatavyo:-

Kwamba, jampokuwa katika kipindi cha miaka 15 iliyopita, Tanzania imerekodi viwango vya juu sana vya kukua kwa uchumi, tuna mafanikio kidogo sana katika kupunguza umaskini wa kipato kwa wananchi. Pia ukuaji huu mkubwa wa uchumi umeshindwa kuzalisha ajira za kutosha kwendana na kasi za kuongezeka kwa idadi ya vijana kwa sababu za mpito za kidemografija, yaani *demographic transition*.

Ukuaji huu wa uchumi umeshindwa kwendana na ukuaji wa idadi ya vijana wanaotafuta kazi za kuajiriwa na pia kujajiri. Ukuaji huu wa uchumi unaopigiwa mfano kila kona ya dunia hii bado umeshindwa kwendana na kukua kwa kasi ya wahitimu kutoka kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu, ya Kati na hata Vyuo vya Ufundi na Ujuzi mbalimbali. Ukuaji huu umeshindwa kwendana na kukua kwa lazima kwa kasi ya uhitaji wa kilimo cha umwagiliaji kutokana na kupungua kwa ujazo wa mvua zinazonyesha na hivyo kupelekeea wakulima wadogo vijiji ni wanaotegemea mvua kupata mazao pungufu ya matarajio na jitihada zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchumi wa Tanzania umekuwa ukikua kwa wastani wa asilimia saba kwa kipindi cha kuanzia 2001 mpaka 2010, ulianguka kidogo mwaka 2009 ambapo ulishuka mpaka asilimia sita kwa sababu ya kuanguka kwa Uchumi wa Dunia, yaani *Financial Turmoil*, japokuwa uliruka juu tena na kurudi kwenye kiwango chake cha awali cha asilimia saba mnamo mwaka 2010.

Sekta zilizokua kwa kasi zaidi mwaka 2010 zilikuwa ni Mawasiliano ambayo ilikua kwa asilimia 22.1 ikifuatiwa na Ujenzi asilimia 10.2, Umeme na Gesi asilimia 10.2, Fedha asilimia 10.1 na Uzalishaji Viwandani asilimia 7.9. Kwa ujumla, kukua kwa Pato la Taifa kulichangiwa zaidi na biashara, yaani *trading*, huduma za marekebisho, kilimo, uzalishaji, biashara ya majengo kwa maana ya *real estate business* na huduma za kibiashara kwa maana ya *business services*. Mfano, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2001 mpaka 2007, Pato la Taifa lilikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 7.1, umaskini ulipungua, kama ukitumia kipimo cha *headcount index* kutoka kiwango cha asilimia 35.7

mpaka asilimia 33.6 tu. Hii inaonesha wazi kabisa kwamba, ukuaji wa uchumi haujawa mpana na haujawalenga wananchi maskini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takimwu za *Integrated Labor Force Survey* za Tanzania za Mwaka 2006, kiwango cha ujumla cha ukosefu wa ajira kilikuwa asilimia 12.9 kwa vijana, kiwango ni kikubwa zaidi ya hiki, ambapo ni asilimia 17 kwa Tanzania Bara na ni asilimia 20 kwa Zanzibar. Hii inaonesha kuwa, nguvu kazi kubwa zaidi ya Taifa letu haitumiki ipasavyo kwa maana kwamba ipo *underutilized*. Hata hivyo, viwango hivi bado ni vya chini ukilinganisha na ongezeko kubwa la vijana wanaohitimu masomo kutokana na wimbi kubwa la ongezeko la Vyuo Vikuu katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi sasa na pia hata wale ambao wanachukuliwa kama wameajiriwa kwenye Sekta Binafsi ama wameajiriwa kwenye biashara ndogo ndogo, kilimo, mifugo na uvuvi, kumekuwa hakuna tija ya kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakadiriwa kwamba, kila mwaka zaidi ya wahitimu milioni 1.2 kutoka kwenye ngazi mbalimbali za taaluma wanaingia kwenye soko la ajira, lakini soko hili lina uwezo wa kuhudumia wahitimu 200,000 tu. Tunatakiwa tufike mahali tujiulize, tutafakari na hatimaye tuchukue hatua. Takwimu hizi utaona wazi kuwa, kunyanyua juu kiwango cha ukuaji wa uchumi na hasa kwenye sekta zinazoshirikisha watu wengi zaidi, ni jambo lenye umuhimu wa kipekee, hivyo kuvutia na kuwezesha uwekezaji kwenye sekta ambazo zinaajiri watu maskini walio wengi ni jambo la lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, takriban miezi 13 iliyopita ndani ya siku moja, nilikutwa na wakati mgumu sana baada ya kupokea ujumbe kutoka kwa vijana mbalimbali sita waliohitimu masomo yao ya shahada mbalimbali wakinitaka niwasaidie kupata mahali pa kujishikiza kwenye mashirika ya marafiki zangu. Mtihani huu ulikuwa mgumu sana kwangu, nilijiuliza nitautatuaje. Imani yangu ni kwamba, siko peke yangu katika hili, Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni wahanga wa maswali magumu kama haya kutoka kwa vijana Majimboni kwetu. (*Makof*)

Matumaini ya vijana na ya Watanzania kwa ujumla yameweka rehani kwenye vichwa na mioyo ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi, nilibaki nikijiuliza, hivi marafiki zangu wanapewa nafasi za ajira kwenye mashirika yao? Maswali yangu yalinifanya nimfikirie upya kijana wa Kitanzania, nikapata muda wa kufikiri kwa mapana na kwa kina na kubaini kwa haraka tu na bila shida hata kidogo kwamba, kama Taifa tuna tatizo, tena tatizo kubwa kweli. Nilijiuliza sana hivi ni kwa nini vijana hawa hawakunijia na mawazo ya namna ya kujajiri na badala yake wanataka mahali pa kujishikiza? Nikajiuliza pia tunazalisha ajira ngapi kwa mwaka na wanaohitimu na wanaotafuta ajira kutoka kwenye utitiri wa Vyuo Vikuu kwa ujumla wao wapo wangapi? Wanaobaki bila ajira na ni wenye nguvu, nia ari na wasaa wa kufanya kazi ni wangapi? Na je, kama Taifa tunawatumiaje vijana hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kuna fursa za masoko kwenye za *SADC, European Union, AGOA* na Jumuiya ya

Afrika Mashariki. Leo ni vijana wangapi wa Kitanzania kwa mfano wamepata ajira Nchini Kenya ama kinyume chake ni vijana wangapi wa Kenya wanavamia soko la ajira la Tanzania na wanapewa nafasi za kipaumbele kwenye mashirika mbalimbali binafsi?

Kampuni ngapi za Vijana wa Tanzania zinauza bidhaa zake Nchini Kenya? Tunapofungua milango kwa kusaini na kuridhia mikata mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa, maana yake ni kwamba, tunawakaribisha wenzetu ndani ya soko letu. Je, sisi tunaingia kwenye masoko yao? Lazima tufanye jitihada za makusudi za kuwaandaa Vijana wa Tanzania kuwa washiriki mahiri na kuwa washindani wenyewe nguvu kwenye kunyakua fursa mbalimbali za kuza bidhaa Nchi za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema uchumi wetu umekua, tunatathmini kama kweli kukua huko kumetupa faida kiasi gani; tunapata faida gani kutokana na kuongezeka kwa Vuyo Vikuu, taasisi za kuzalisha fikra, yaani *think tanks* na kukua kwa idadi ya wasomi wetu, kwa maana ya *critical mass*? Je, tumejiandaa kiasi gani kukuza ajira kwa vijana wetu? Maswali haya na mengine mengi mengineyo ni magumu na hayajibiki kirahisi hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tuanzishe Mjadala Mahususi wa Kitaifa, utakaolitazama suala la ajira kwa vijana kwa mapana na marefu na kulipatia ufumbuzi. Vijana wazama hizi hawataki maneno wanataka vitendo. (*Makofii*)

Maneno na Mipango mizuri iliyoandikwa haitawasaidia sana, wanahitaji fursa nzuri kujiajiri waendeshe maisha yao. Mipango mgando na butu kama ule wa kuwawezesha vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kule kwenye Halmashauri zetu ama ule wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*), haujaleta mapinduzi yoyote mpaka sasa. Hakuna mtu mwenye akili timamu anayeweza kusimama hapa na kuipigia jaramba mikakati kama ile, maana vijana hawailewi na wala hawaajaona na kufaidi matunda yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa siku hizi hawako tayari kutumiwa na Wanasiasa wa Chama chochote kile cha Siasa, kwa faida za kisiasa. Vijana wanataka kuona mabadiliko, wanataka kuona Mapinduzi, sio yale ya kisiasa yasiyo na tija, wanataka kuona Mapinduzi ya Kiuchumi na wako tayari kushiriki katika harakati za kufikia Mapinduzi hayo.

Mheshimiwa Naibu Waziri, nimefanya tafakuri juu ya ufumbuzi wa tatizo la ajira kwa vijana na pia kukuza uchumi wa nchi na nimebaini kwamba, uwekezaji kwenye kilimo na viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo, ndiyo suluhu ya haraka na ukweli ya tatizo la ajira kwa vijana. Kwa namna yoyote ile, haimaanishi hata kidogo kuwa hoja hii ndiyo mwarobaini wa tatizo hili ambalo ni pana na linahitaji ufumbuzi mpana zaidi wa kila sekta na linahitaji ushiriki wa wadau wengi zaidi na kwamba si lazima kuwa vijana wote watataka kuwekeza kwenye *industries* ama sekta nilizozitaja hapa. Hii ni dira tu na ni mchango wangu mdogo kwenye kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili kabla halijawa janga la Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wenyewe nguvu wasipotumika vizuri, narudia tena wasipotumika vizuri, watatumiwa vibaya na watu wajanja wenyewe uchu na tamaa ya madaraka. Wao wenyewe wanaweza kujingiza kwenye vitendo visivyofaa kama kwenye mitandao ya biashara haramu za madawa ya kulevyo, mitandao ya madanguro ya ukahaba na hatimaye kuangamia wao wenyewe na wenzao wengi zaidi. Kama Taifa, tuna wajibu wa kuandaa mazingira wezeshi kwa ajili ya kizazi cha mbele yetu, swali lingine hapa linazalishwa. Je, tunaandaa mazingira hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio hili likitekelezwa, litawawezesha vijana wote; wasomi na wasiosoma na hapa ninarudia tena, azimio hili likitekelezwa, litawawezesha vijana wote, wasomi na wasiosoma bali wajasiriamali wenyewe ari, mshawasha, nia, tabia, fikra, hekima, utayari na pia nguvu za kuwa watengeneza ajira badala ya watafuta ajira, kwa maana ya job *creators instead of job seekers*; wajiunge kwenye vikundi na wafanye kazi za kujajiri kwanza wao wenyewe, lakini pia watakuwa waajiri wa wenzao.

Mbali na faida za kiuchumi zitakazopatikana, pia mpango huu utaamsha hali ya mabadiliko ya kifikra, yaani utasababisha *mind set change* kwamba, badala ya vijana kusoma huku wakitarajia ajira baada ya masomo kama ilivyo ada, watakuwa wakisoma huku wakifikiria kujajiri na kutajirika. Badala ya kuishi na kufikiria kuwa Serikali itawaleta maendeleo yao, vichwa vyao sasa vitafunguka, wataweza kufungulia *potential* zao nyingine, wataanza kuota kufika mbali zaidi katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale watakaofanikiwa, watakuwa mfano bora zaidi kwa wenzao na hapo tutajikuta tumejenga Taifa la watu makini, wawajibikaji na wenyetamaa ya mafanikio. Kwa maana ya *ambitious and responsible citizens* ile zana kwamba, utajiri siyo stahiki yao, ni ya watu wachache wenyetamaa ya asili hiyo, kwa hakika itatoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwekeza kwenye kilimo, vijana wataweza kujenga na kuendesha viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo kwa maana ya *backward linkage* na pia wengine wataanzisha Kampuni za Masoko (*Marketing and Trading Companies*); wengine za usafirishaji (*Logistic and Handling of Goods*); pia wataanzisha viwanda wenzeshi (*Associated Industries*) mfano vya *packaging materials*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wengine wakiendeleza Mashamba na Viwanda vyao, ajira zitajizalisha zaidi kwenye sekta nyingine kutokana na uwekezaji huu. Kwa maana ya *multiplier effect*; mfano, wakati wengine wanawekeza kwenye mashamba na kwenye viwanda vyao, wengine watakuwa wanawekeza kwenye kuanzisha makampuni ya kutoa ushauri kwa wakulima (*consulting firms*), wengine kwenye ugunduzi wa mbegu, kwenye uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora, wengine kwenye habari na mawasiliano; kwa mfano, kuboresha kilimo na upatikanaji wa masoko na taarifa za bei kwa kutumia njia za kisasa za mawasiliano kama vile ujumbe mfupi wa maneno, yaani *sms, internet* na wengine wakiwatengenezea wenzao tovuti, kwa maana ya *website* kwa ajili ya biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuongeza tija na ufanisi kwa maana ya *productivity and efficiency*, tutakuwa tumeongeza uzalishaji wa mazao na bidhaa zinazotokana na mazao; tutakuwa tumeleta uhakika wa masoko ya mazao ya wakulima karibu zaidi na wakulima; tutaongeza *market stability and sustainability* na hatutauza mazao ambayo hayajaongezewa thamani kutoka shambani; na tutakuwa tumeleta *value addition*. Matarajio yangu ni kwamba, tutakuwa tumetatua siyo tu tatizo la ajira kwa vijana, bali pia kwa kiasi kikubwa, tatizo la kiuchumi kwa kuongeza uzalishaji, kuongeza thamani ya mazao yetu, kuhakikisha masoko ya uhakika kwa wakulima na mwisho kupunguza kiwango cha mfumko wa bei, yaani *inflation rate* ya vitu na zaidi kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi na kupunguza manunuzi ya bidhaa kutoka nje ya Tanzania, jambo ambalo litachangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha akaunti yetu ya *balance of payments*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiuangalia Mpango huu vizuri, utagundua kwamba, kutakuwa na vijana wasomi, ambao watawezeshwa kuwekeza kwenye mashamba makubwa ya kibashara na viwanda. Wale ambao hawajasoma watawekeza kwenye kilimo cha mashamba ya saizi ya kati na hata yale madogo madogo na pia viwanda vidogo vidogo. Haya makundi yatabebana kwenye *model* hii. Hivyo, kila kundi litatoa ajira kwa watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kila kitu kikienda sawa, kibaiolojia tunawategemea vijana wataishi kwa muda mrefu zaidi huko mbele kuliko wazee. Tukiwatumia vijana kwa kuona mbele kuna nini, wakiwekeza leo na

wakifanikiwa kuendesha biashara zao kwa faida, maana yake ni kwamba, baada ya miaka 20, Tanzania itakuwa na watu wenyewe nguvu na wenyewe uchumi imara. Kwa kuwa sekta binafsi ni *engine* ya kukua kwa uchumi wa nchi, tutatoka kwenye kundi la nchi maskini zaidi Duniani. Pia ni rahisi sana kwa kijana kufanya jambo la kubahatisha ama kuthubutu, maana ya kubeba *risk* na kufanya kazi kwa bidii kufikia ndoto zake bila wasiwasi. Zaidi, kundi hili likipewa kipaumbele linaweza kuondoa utamaduni wa Tanzania kutoka kwenye kufanya mambo kwa mazoea, yaani *business as usual* na *laissez-faire* na kuwa nchi ya watu wenyewe kufanya kazi kwa ubunifu wa hali ya juu na *passion* ya ukweli. Mimi nalionna hili ndiyo kundi pekee liatakaloweza kuijenga Tanzania mpya, Tanzania ya miaka ishirini ijayo. Sina nia ya kuonekana ni mbaguzi kwa wazee wala simaanishi kuwa wazee hawahitajiki, la hasha; napenda kusema tu kuwa, Mpango huu ni mahususi kwa vijana tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuwe na ndoto na ni lazima tujipange kuzifikia ndoto zetu, hakuna ujanja mwingine. Hatuwezi kufanikiwa kwa kutumia mikakati ile ile iliyotufikisha hapa; ni jambo moja kuwa na ndoto na lingine kujipanga namna ya kuifikia. Ni jambo lisilo makini kupanda bangi na kujandaa kuvuna mchicha hatimaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kubadilika, tupande mbegu za kuandaa Uchumi wa Tanzania kesho. Tunahitaji mawazo mapya, tunahitaji njia mpya za utekelezaji na hapo ndiyo tutaona matokeo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, hoja yenyewe sasa inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1), (2) na (3) kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA** idadi kubwa ya Watanzania zaidi ya asilimia 60 ni vijana chini ya miaka 40;

**NA KWA KUWA** vijana hawa ni nguvu kazi ya kutegemewa katika nchi yetu, na kama kila kitu kitabaki sawa, kibaiolojia vijana hawa watakuwepo nchini kwa miaka mingi ijayo kulinganisha na wazee;

**NA KWA KUWA** vijana wanahangaika kutafuta ajira na kuna fursa nyingi za kutengeneza ajira nchini ambazo hazijafanyiwa kazi;

**NA KWA KUWA** vijana wengi nchini humu wamedhihirisha kuwa wana ari, nguvu, nia, elimu, ujuzi na vipaji vya kupigiwa mfano kwenye fani mbalimbali na wanakosa mitaji na mpango mahususi wa uwezeshi, wanahitaji uongozi, yaani *leadership, mentorship and guidance* ili kukamilisha ndoto zao;

**NA KWA KUWA** tuna malengo ya kuivusha nchi yetu kiuchumi kufikia mwaka 2025, kama uklangalia Dira ya Maendeleo ya 2025, kuelekea Nchi zenyе Uchumi wa Ngazi ya Kati (*Middle Income Countries*), wengi watakaokuwepo kibaiolojia watakuwa ni vijana na wanatakiwa kuwezeshwa ili wawe mhimili wa mwenendo wa Uchumi wa Tanzania ya kesho tunayoilenga na pia wakiwezeshwa leo, tunaamini ndiyo wataifikisha Tanzania huko tunapopataka kesho; ili kuzalisha ajira nyingi na kwa haraka, kilimo na viwanda

vyaneye uhusiano wa moja kwa moja, yaani *backward linkage* na kilimo, ndiyo jibu la msingi la nia hiyo;

**NA KWA KUWA** llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 88 hadi wa 95, kifungu cha 79, fasili ya (1), (2) na (3), Chama ambacho kinatawala nchi yetu kwa sasa, inatambua na kutoa maelekezo mazuri kabisa kwa Serikali kuhusiana na hoja hii ya kukuza ajira kwa vijana na pia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano tulioupitisha hapa Bungeni, ukiangalia ukurasa wa 92, kifungu cha 5(2)((iv) na MKUKUTA II, vinatambua umuhimu wa kutekeleza haya;

**NA KWA KUWA** pia Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwenye maelezo yake ya utangulizi mwanzo wa Mpango huo anasema na ninamnukuu hapa kwamba: "*Employment creation, particularly for the youth is also a critical cross-cutting target of this Plan.*" Inatafsirika Kiswahili kuwa: "Kutengeneza ajira hususan kwa vijana ni lengo mtambuka la Mpango huu." Kinachotakiwa sasa si kingine bali ni kufanya jitihada za utekelezaji tu, maana barabara zote zinaelekea huko. Hivyo basi, Bunge linaazimia kuitaka Serikali yetu ifanye yafuatayo:-

Moja, ianzishe Mpango Maalum wa Kukuza Ajira za Vijana kwa kuanzisha Mfuko wa Mkopo wa Vijana wanaowekeza kwenye kilimo na viwanda vyaneye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo, yaani (*backward linkage*). Mfuko huu hapo baadaye utaendelezwa na kuwa Benki ya Maendeleo ya Vijana Tanzania (*Tanzanian Youth Development Bank*). Kwamba, uanzishwe Mfuko Maalumu wa Kutoa Mikopo ya Uwekezaji kwa Vijana wa Tanzania

utakaoitwa *Tanzania Youth Enterprise Challenge Fund* na iwekeze katika Mfuko huu. Mtaji usiopungua shilingi bilioni mia mbili za Kitanzania kwa mwaka wa kwanza na bilioni mia moja kila mwaka wa fedha utakaofuata. Mfuko huu uwalenge vijana utakaowekezwa kwenye Sekta ambazo tutazichangia sana, tuweke kipaumbele kwenye Sekta za Kilimo na Viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo ili kuzalisha ajira nyingi kwa vijana.

Vijana hawa waingizwe kwenye mashindano ya kuandika maandiko ya Miradi na ile itakayoshinda kwenye mchakato huu, ndiyo pekee itakayochaguliwa. Mchakato huu katika hatua fulani, kama itabidi iwe hivyo, uwashirikishe wananchi kwa njia ya kupigia kura Miradi wanayoona inafaa na ushindi katika hatua hii iwe ni kigezo kimojawapo cha kuwapata watakaoshinda na kwamba, mikopo itakayotolewa katika mchakato huu, itakuwa ni yenye masharti nafuu kama ifuatavyo:-

Itakuwa na riba asilimia sita kushuka chini. Itakuwa na kipindi kirefu cha kurudisha (*pay back period*) cha takriban miaka 15 hadi 20. Itakuwa na kipindi kirefu cha kutoanza kurudisha mkopo kwa maana ya (*grace period*) kati ya miaka miwili hadi mitatu. Isiwe na masharti ya dhamana, yaani *security* za mali, maana vijana hatuwategemei wawe na mali zozote zile, bali iwe na dhamana maalum kama Cheti cha Elimu au Ujuzi kwenye fani husika. Ardhi ya shamba iliyorasimishwa kwa utaratibu unaokubalika na iwe kwenye usimamizi wa Kitengo Maalum cha Mfuko huo. Mpango huu uendane na kuweka utaratibu mzuri na rahisi wa kusajili mashamba na ardhi.

Kwamba, itenye Maeneo Maalumu ya Kuwekeza, yaani (*Special Economic Zones*), ichague maeneo maalum kwa mazao na viwanda maalum kwenye Wilaya mahususi za nchi yetu. Vijana waelekezwe na kusimamiwa kuwekeza kwenye Sekta zilizochaguliwa na wawezeshwe kupata mitaji hiyo. Uwanzishwaji wa Miradi hii uendane na kuwepo kwa sharti la kuwataka vijana kuhamasisha kilimo cha kisasa na kusaidia wakulima kwenye maeneo yanayowazunguka kwa njia ya Mkataba Maalum, yaani (*Contract Farming*) wa kukopesha pembejeo za kilimo, mbegu bora za kilimo, zana za kilimo ama kuwalimia na kuwavunia kwa mashine na kutengeneza mifumo ya umwagiliaji. Hii itasaidia kuongeza tija na ufanisi kwa wakulima vijiji.

Mwisho ni kwamba, Serikali iamue kuchagua Sekta, zitakazohusika kwenye Mpango huu Maalum kwa ajili ya vijana. Baadhi ya Sekta za kuandaliwa ni pamoja na kilimo kikubwa cha kibashara cha umwagiliaji, kila mradi ni lazima uwe na mpango wa kuwafikia wakulima wadogo wanaozunguka shamba husika, (*Satellite Outgrower Schemes*), ujenzi wa viwanda kama vya kuchambua Pamba (*Ginneries*) na kusokota Nyuzi (*Skimming*), kukoboa na kusaga unga, chakula ama chakula cha mifugo. Kukamua na kusafisha mafuta ya kula, pia kutengeneza sabuni, kusindika *juice* na kadhalika utafanyika maeneo ya karibu na mashamba haya. Kila eneo la Mradi litengwe likiwa na uwezekano wa kufanya utanazi kwenye sector hiyo ili kukamilisha mnyororo wa thamani kwenye eneo moja (*value change*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala, hoja imetolewa na imeungwa mkono, nakushukuru sana kwa hoja yako.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gudentia Kabaka.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, Mbunge wa Nzega, ambaye ameleta hoja ya kuliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Azimio la Kuanzisha Mpango Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana kwa Kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana Wanaowekeza kwenye Kilimo na Viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, amefanya utafiti na ninampongeza kwa utafiti huo, lakini pia kwa mtazamo wake chanya kuhusu suala la ajira kwa vijana hasa mtazamo wake wa vijana kuanza kuangalia suala la kujajiri na kuajiri wenzao.

Hata hivyo, naomba nifanye masahihisho kidogo tu kwamba, takwimu alizotumia za 2006 za ukosefu wa ajira, yaani *unemployment rate* za 2006, katika utafiti wa

nguvukazi ilioneshaa kwamba, *unemployment rate* ilikuwa asilimia 11.7 badala ya 12.9, ilikuwa imepungua kidogo.

Kimsingi, maelezo ya Mheshimiwa Mbunge katika hoja yake hayatofautiani sana na juhudii za Serikali ya Awamu hii ya Nne inayoongozwa na llani ya Chama cha Mapinduzi ya 2005 - 2010 na 2010 - 2015. Ni kweli kwamba, uchumi ulio rasmi hauwezi kupokea vijana wote wanaomaliza shule kwa nyakati mbalimbali katika kuwaingiza kwenye ajira rasmi. Kwa hiyo, suala la mikopo haliwezi kukwepeka, japo tunasema sana kwamba mikopo siyo mitaji pekee katika suala la ajira kwa vijana, bali tunahitaji pia kuwa na elimu kwa vijana kwa ajili ya kuwafundisha ujasiriamali ili wawe na *study* hizo, lakini pia wawe na *study* za kazi, pamoja na mtazamo chanya kuhusu masuala ya elimu, vyote ni muhimu sana katika upatikanaji wa ajira.

Serikali hii ya Awamu ya Nne kwa kweli imejitahidi kwa suala la mikopo kwa kutumia fursa mbalimbali. Fursa hizi ziko katika ukurasa wa pili. Nafikiri mkipewa mtazisoma kwa ajili ya *ku-save* muda nisizisome zote. Lakini naomba niende moja kwa moja katika suala la mfuko wa vijana, unaitwa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Huu ni Mfuko ambao unasihamiwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na unalenga kuwawezesha vijana wa Vijiji na Mijini kwa kuwapatia mikopo vijana wenyewe yenye masharti nafuu kupitia SACCOS.

Aidha, Serikali kwa sasa hivi tunavyoongea, kwa kupitia Wizara hiyo hiyo, imeshaanza mchakato wa kuanzisha Benki ya Vijana, kwa madhumuni ya kuwakopesha vijana na kuboresha mitaji yao ya ujasiriamali.

Suala la kutenga maeneo kwa vijana kama alivyolizungumza Mheshimiwa mtoa hoja, pia linafanyiwa kazi na Wizara, lakini tunashirikisha Mikoa na Halmashauri ambako ndiko kuna vijana. Nitoe mfano tu wa Mikoa ambayo imekwenda mbele sana katika hili; mfano ni Mkoa wa Pwani ambao mwaka 2012 ulishirikisha wadau na kuzindua Mkakati wa Kubainisha Fursa za Ajira kwa Vijana kwa kuanzisha kambi maalum ya maarifa ya vijana au Pwani *Youth's Center of Excellence*. Kambi hii iliendesha mafunzo ya muda mfupi ambayo yaliwaandaa vijana kupata stadi za maisha, stadi za kazi, stadi za ujasiri amali na biashara na msisitizo mkubwa ukiwa katika uzalishaji na usindikaji wa mazao kwa kutumia mnyororo wa thamani au *vaul* *added chain* na kuimarisha ubia kati ya Sekta za Umma na sekta binafsi.

Pia Mkoa huu una matarajio sasa ya kutengeneza kitu kinaitwa *technological park* ambako eneo la ekari 4,500 limekwishapatikana katika kijiji cha Milo, Wilaya ya Bagamoyo. Lakini Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Igunga, jirani na Mheshimiwa mtoa hoja, umewahamasisha vijana wasomi kujeunga na kuanzisha kikundi cha ujasiri amali, hususan kwa ajili ya uzalishaji wa asali, mipango mahsus iyo ya kukiwezesha zaidi kikundi hiki ili kupanua shughuli zake ili kuwezesha kujajiri.

Mkoa wa Singida kama mnavyofahamu, umeweeka mikakati katika kuhamasisha na kuwawezesha vijana wasomi na wasio wasomi kujikita zaidi katika uzalishaji wa alizeti na asali na takriban Mikoa yote sasa hivi imeshaibua mikakati hiyo na kuwaunganisha vijana kwenye vikundi

mbalimbali vya uzalishaji mali na biashara kulingana na vipaumbele na pia kutumia fursa zilizopo katika mazingira yao.

Sasa hivi tunawasiliana kwa karibu sana na Mikoa hii na Mikoa yote wameshaanza kutuletea taarifa ya vikundi hivi na jinsi wanavyotenga maeneo hayo. Wizara ya Kazi na Ajira, tunayo *program* ambayo tumeshirikiana na watalaamu wa Chuo Kikuu Dar es Salaam ambayo inalenga upatikanaji wa ajira kwa vijana wa kike na wakiume. *Program* hii ina-components tatu:-

*Component* ya kwanza ni kutoa mafunzo na stadi za kazi kwa vijana ili kuwawezesha kujajiri na kuajiriwa au *skills training for enhancing youth employability*. Lakini kuna sehemu ya pili ni kuhamasisha na kuwaelekeza vijana kutambua fursa za ajira ili kujajiri na waweze kuajirika na pia kuajiri wengine katika sekta mbalimbali ambazo vijana wanaonyesha kupenda na kuweza kumudu. Kwa sababu huwezi ukawalazimisha vijana wote kwenda katika kilimo, vijana wanafursa zao wenyewe, wana matashi yao wenyewe, lakini pia wana stadi na vijapaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vidogo vidogo vya uzalishaji na kusindika mazao ya kilimo, ufugaji, uvuvi biashara na bidhaa mbalimbali na huduma mbalimbali za sekta kama ya utalii, mawasiliano, sayansi na teknolojia, teknohama, huduma na usafirishaji ni moja ya mambo ambayo *program* hii itazingatia kama alivyoeleza mtoa hoja. Lakini pia katika hii *program* tunataka vijana wawe na Kampuni zao ndogo ndogo za ujenzi, utunzaji na ukarabati wa barabara, majengo na miundombinu mbalimbali kama

walivyo vijana wa Pwani, sasa hivi wanatumika na Halmashauri katika kujenga madarasa. Kwa hiyo, wamekuwa na utaalamu, wanakuwa wanatumiwa kama *tenderers* kuainisha Mfuko maalumu wa kuwawezesha vijana walengwa kupata mitaji au mikopo ya kuanzisha na kuimarisha miradi yao ya kiuchumi. Hiyo ndiyo *program* tuliyoanzisha na inatarajia kutekelezwa kwenye Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi tunapoongea, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo, Shirika la Chakula Duniani na Shirika la Wafanyakazi Duniani (*ILO*), tuko pamoja kuandaa *programs* hizi kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeendelea kutaja juhudini yingine za ki-sekta ambazo zinatekelezwa, naomba mjisome ukurasa wa sita, lakini pia ukurasa wa saba nimeeleza mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 na 2015/2016 vibali vilivyoandikwa na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuisaini ambayo inasema, kwa kweli suala la ukuzaji wa ajira ni mtambuka.

Vile vile kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla na umuhimu wa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu, elekezo hili ni kwa kila mdau kuzingatia malengo ya kukuza ajira kuwa ni kipaumbele. Mpango huu wa miaka mitano umeelekeza bayana kwa Wizara zote ziwe Waratibu wa Mipango ya ki-sekta, Idara na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Serikali za Mitaa, wote walipatie suala la ajira hasa la vijana kipaumbele na kulitolea taarifa kuhusu utekelezaji wake wakiwasilisha

Wizara ya Kazi na Ajira takwimu za ajira zitakazozalishwa kutokana na mipango na *programs* za maendeleo ya kila sekta. Sekta zile zimetajwa katika mpango ule, Nishati na Madini, Miundombinu hasa ujenzi wa barabara, Uchukuzi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo juhudhi za wabia mbalimbali, *ILO* ina mpango wa kazi nje nje. Nafikiri mtakuwa mmeshauona huko huko! Ulianizia katika Wilaya 10 za Mbeya Mjini, Kibaha, Handeni, Mtwara Mjini, Singida Mjini, Bagamoyo, Urambo, Tabora Mjini, Magu na Lindi Mjini. Lakini sasa umesambaa katika Mikoa yote, uko kikanda, lakini unatoka kwenye kanda, unakwenda kwenye Mikoa ya Kanda hiyo na umeshahamasisha vijana 76,241 kuhusu masuala ya ujasiriamali na hawa ni vijana wa elimu mbalimbali.

Shirika la *FAO* nimelisema ukurasa wa tisa, mtaweza kusoma zaidi na kwa hiyo, upatikanaji wa ajira kwa vijana kama Sera yetu ya ajira ya mwaka 2008 inavyosema, kwa kweli ni suala mtambuka na hili lazima tushirikiane wadau wote. Sasa umuhimu tumeona pia kwamba katika Wizara, tunachokosa ni taarifa za ajira ili kuweza kuwaonyesha vijana kwamba katika soko la ajira ni taaluma zipi zinahitajika ili waweze kujipanga kwa fursa zile ambazo ni rasmi, lakini pia waweze kujipanga katika fursa ambazo siyo rasmi.

Hapo na Wizara yangu sasa hivi ninapoongoea nadhani watakuwa wanaongea na waandishi wa habari, kwa kushirikiana na Ofisi yetu ya Taifa ya Takwimu yaani *NBS*, tumetoa hali halisi ya ajira nchini kwa kipindi cha

mwaka 2010/2011 na taarifa hii italetwa kwa kitabu maalumu mtagawiwa Waheshimiwa Wabunge. Sasa baada ya kusema hayo, kutokana na maelezo hayo, namwomba Mheshimiwa Mbunge aridhike kuwa, mawazo na matakwa yaliyoainishwa kwenye hoja yake yalishaanza kufanyiwa kazi na Serikali.

Kwa kutumia Kanuni ya 57(1) ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la 2007, naomba kutoa hoja sasa ya kubadilisha maneno kadhaa kutoka kwenye vipengele vinne vya hoja yake ili kuondoa masuala yale yanaoyojrudia ambayo yanaenda kufanyiwa kazi Serikalini na kuweka kama ifuatavyo:-

Hoja yake ya kwanza amesema, Serikali ianzishe mpango maalumu wa kukuza ajira kwa vijana kwa kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana Wanaowekeza kwenye Kilimo na Viwanda vyenye Uhusiano wa Moja kwa Moja na Kilimo. Mfuko huu hapo baadaye utaendelezwa na kuwa Benki ya Maendeleo ya Vijana Tanzania, yaani *Youth Developments Bank*. Mimi nimeweka mawazo hayo hayo, lakini kwa kusema kwamba Serikali itekeleze mpango maalumu wa kukuza ajira kwa vijana ambao umetengenezwa na Wizara ya Kazi na Ajira ili vijana hawa waweze kujajiri na kuajiri wengine.

Ya pili inasema, Serikali ianzishe mfuko maalumu wa kutoa mikopo ya uwekezaji kwa vijana wa Tanzania utakaoitwa *Tanzania Youth Center Price Challenge Fund* na iwekeze katika mfuko huu mtaji usiopungua bilioni za Kitanzania 200 mwaka wa kwanza na bilioni 100 kila mwaka wa fedha utakaofuata. Mfuko huu uwalenge vijana

watakaowekeza kwenye Sekta ambazo tutazichagua, tuweke kipaumbele kwenye Sekta za Kilimo na viwanda zenyehusiano wa moja kwa moja na kilimo.

Pia vijana hao waingizwe kwenye mashindano ya kuandika maandiko ya miradi, *Project Proposals* na ile itakayoshinda kwenye mchakato huo ndiyo pekee itakayochaguliwa. Mchakato huu katika hatua fulani kama itabidi iwe hivyo, uwashirikishe wananchi kwa njia ya kupigia kura miradi waliyoiona inafaa na iliyoshinda katika hatua hiyo iwe ndiyo kigezo kimojawapo cha kuwapata watakaoshinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina tatizo na maudhui haya, lakini nilifikiri pamoja na yote aliyoyaeleza, naomba niya-*summarize* katika taarifa hii ambayo inafanana maudhui yake kwamba, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulioko chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, uboreshwe kwa kuongezewa fedha kutoka Serikali kuu na Halmashauri ili vijana wapate fedha ya kutosha ya kuchukua mikopo ya kuboresha mitaji yao ili kuzalisha ajira nyingi zaidi kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Halmashauri zibuni njia na vigezo vya kuwapatia mikopo, ikiwemo kuwashindanisha kwenye kuandika maandiko ya miradi na Ofisi za Halmashauri zitoe wataalamu kwa ajili ya shughuli hiyo na kwamba vijana watumie fursa nyingine zilizopo Serikalini na kwa wadau binafsi na kupata mikopo yenye masharti nafuu na riba ndogo.

Tatu, amesema, Serikali itenge maeneo maalum ya kuwekeza (*Special Economic Zones*). Chini ya mpango huu, ichague maeneo maalum kwa mazao na viwanda maalumu kwenye Wilaya mahsusini ya nchi yetu; vijana waelekezwe na kusimamiwa kuwekeza kwenye sekta zilizochaguliwa na wawezeshwe kupata mitaji hiyo. Uanzishaji wa mradi huu uendane na kuwepo kwa sharti la kuwataka vijana kuhamasisha kilimo cha kisasa na kusaidia wakulima kwenye maeneo yanayowazunguka kwa njia ya mikataba maalumu na kukopesha pembe jeo za kilimo, mbegu bora za mazao, zana za kilimo ama kuwalimia na kuwavunia kwa mashine, kutengeneze mifumo ya umwagiliaji, hii itasaidia kuongeza tija na ufanisi kwa wakulima.

Nimesema, hilo halina tatizo pia lakini *already* Mikoa inafanya kwa hiyo, iendelee kutenga maeneo maalumu ya uwekezaji, *EPZ* na *SEZ* kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ambao watatengeneza ajira kwa vijana, lakini pia Mikoa na Halmashauri ziendelee kutenga maeneo maalumu kwa ajiri ya vijana kufanya shughuli zao mbalimbali ikiwemo kilimo, ufugaji na aina nyingine za ujasiriamali. Mikoa iendelee kuhamasisha kuhusu vijana kuibua fursa za ajira na kuwatafutia vijana mikopo ikiwemo za pembejeo, mbegu bora, ili kuboresha na kuleta tija katika shughuli zao za ujasiriamali na kuwasaidia kupata masoka na bidhaa.

Maudhui ya nne, yanahusu suala la sekta ambazo zitahusika kwenye mpango huu maalumu wa vijana. Waliopendekeza baadhi ya sekta za kuangalia ni pamoja na Kilimo kikubwa cha kibiashara cha umwagilia. Kila mradi

lazima uwe na mpango wa kuwafikia wakulima wadogo wanaozunguka shamba husika.

Ametaja hapa kwamba ni kukoboa, kusaga unga, chakula cha mifugo, kukamua na kusafisha mafuta ya kula, pia kutengeneza sabuni, kusindika juisi, utafanyika kwenye maeneo ya karibu na mashamba yao. Kila eneo la mradi litengwe likiwa na uwezekano wa kufanya utanuzi kwenye sekta hiyo ili kukamilisha mnyororo wa thamani kwenye eneo.

Kimsingi, hapa anazungumzia masoko na mimi nimebadilisha kwa kusema, Serikali kupitia mpango wako wa maendeleo 2011/2016 iendelee kuhimiza Wizara, Mikoa, Halmashauri, kuibua fursa za ajira kupitia mipango yao ya maendeleo ya ki-sekta. Sekta hizo ni pamoja na kilimo kikubwa cha biashara na umwagiliaji, viwanda, nishati na madini, miundombinu, ujenzi wa barabara na maeneo mengine yote yaliyotajwa katika mpango huu na kuibua fursa za ajira kwa vijana, pamoja na kuwatafutia vijana masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa kweli naomba tena nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla - Mbunge wa Nzega, kwa hoja hii muhimu ambayo tunasema kwamba ni suala mtambuka na ameshatambua hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Hoja ya Mheshimiwa Waziri imeungwa mkono. Sasa imetolewa hoja ya marekebisho ya hoja kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Mtoa hoja Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla, una nini cha kusema kuhusu hoja hiyo kabla ya Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha marekebisho ya hoja yangu ya awali, lakini naomba tu niseme hapa katika hatua hii sikubaliani na marekebisho ya Serikali kwa sababu zifuatazo:-

Sababu ya kwanza, Serikali inaonekana kuwa *reluctant* kwenye suala hili na kuonekana wazi kwamba mapendekezo yote manne ambayo nimeyaleta katika hoja yangu, yamebadilishwa kwa kiasi kikubwa sana. Ni kweli Mheshimiwa Waziri analenga kubadili maneno, kuondoa maneno na kuweka maneno mengine, lakini anapoondoaa hayo maneno, amejikuta amefanya *radical changes* kwenye hoja yangu ya msingi ya awali na hivyo adhima nzima ya mimi kuleta hoja yangu sasa inapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, niseme tu baadhi ya maeneo ambayo sikubaliani nayo na nitoe sababu kwa nini sikubaliani naye. Moja ni hiyo, lakini nyingine ni kwamba, hoja yangu inalenga katika kupendekeza njia ambazo zitatuwezesha kutekeleza mikakati mbalimbali tulioipitisha kama Taifa. Inalenga kutoa mchango huo, kwa sababu wakati naiandaa hoja

hiyo, nimefanya utafiti wa kutosha na kubaini kwamba mikakati iliyopo leo hii, miradi mbalimbali iliyopo leo hii, mipango mbalimbali iliyopo leo hii, haijaleta tija yoyote ile katika kuongeza ajira.

Sasa mimi kama mtu ambaye mime-*graduate* kutoka kwenye ujana, maana yake sasa nina miaka 37, kwa Sheria za *UN* za *WHO* nimekuwa siyo kijana tena, nilishakuwa mtu mzima. Naona kabisa vijana niliowaacha huko kwenye ujana hawapewi fursa za kutosha za kuweza kuendesha maisha yao. Pia naona kwamba, vijana hawapewi fursa za kuendesha uchumi, hawapewi fursa za kuchangia kwenye uchumi wa nchi yao na ninaona kwamba vijana hawatumiki ipasavyo katika kukuza uchumi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana leo hii, chini ya miaka 40 ni zaidi ya asilimia 60 ya Taifa letu. Sasa unapokuwa hulitumii vizuri kundi la watu asilimia 60 na ndiyo wenyewe nguvu na wengi wao ndiyo wenyewe elimu hao, ndiyo wenyewe ujuzi na ndiyo wenyewe uwezo wa kufanya vurugu zote zile ambazo zinafanyika, nachelea kuona kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaingia kwenye janga kubwa sana la kusumbuliwa na kundi kubwa la vijana, kwa sababu hawana kazi ya kufanya; watadhani kwamba sisi ambao tuko hapa, hatuwatendei haki, hatujwajali na wala hatubuni mipango ya kuwasaidia. Huwezi ukafikia ile *economic trajectory* ambayo inaongelewa kwenye dira ya Taifa ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, katika maisha ya binadamu, mimi sitaki kuangalia tumetoka wapi, lakini katika maisha ya binadamu kuna siku tatu tu; jana, leo na

kesho. Siku ya jana imeshapita, *there is nothing much that you can change about it!* Huwezi kuibadili! Siku ya leo ndiyo hii tunaishi. Lakini siku ya leo inatuwezesha kuziona changamoto za leo, inatuwezesha kuangalia siku ya kesho tutafanya nini. Kwa kuwa yaliyopita yameshapita, mimi sitaki kuanza kufukua maiti hapa na kuangalia kama kuna nini ndani ya maiti ama la, lakini ninataka tuangalie huko mbele tunakoelekea, tunafanya nini leo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wa leo na viongozi hususan vijana kama mimi wa leo hii, tunatakiwa tuzi-meet changamoto za maisha ya baadaye, *20 years, 50 years to come.* Changamoto kubwa iliyopo mbele yetu ni changamoto ya kuhakikisha kuna *full security* katika Taifa, kwa maana wa usalama wa chakula. Ni changamoto ya kuangalia kuna mazingira bora ya kitaaluma, kuna mazingira mazuri ya kujiajiri na kutoa ajira. Sasa changamoto zote hizi, ninaona kama hazijafanyiwa kazi ipasavyo na ndiyo maana ninaleta hoja sasa ya kutia kasi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyopo na ninaleta mpango mpya ambao uta-coordinate hizi *efforts* zote ambazo zinafanywa na Serikali.

Kwa sababu leo hii ukisikiliza maelezo ya Mheshimiwa Waziri utaona kuna miradi ameieleza iko Pwani, wanaita *Technological Park*; kuna mradi upo Igunga, mradi tu wa vijana kikundi kimoja kimeweleshwa pale na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kufunga mizinga ya nyuki kwa ajili ya kuvuna asali; kuna miradi, hata mimi Nzega nina miradi, hata Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa naye alikuwa anaeleza miradi iliyopo jimboni kwake, sasa hii miradi ni

miradi midogo sana ambayo ipo katika maeneo mbalimbali.

Tunapoongea katika mpango huu, tunaongelea ku-*coordinate efforts*, kuziweka pamoja *efforts* zetu ili sasa tuweze ku-move kwa pamoja kama Taifa, lakini pia tunaongelea kulenga maeneo mahsus ya uchumi.

Kwa mfano, hapa tunaongelea kulenga Sekta ya Kilimo ambayo inaa jiri watu zaidi ya asilimia 70 ya nchi yetu, lakini pia ninaona kama vile Mheshimiwa Waziri, kwa niaba ya Serikali, pengine hajasoma llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ule ukurasa wa 93 kifungu cha 79. Hoja yangu imejikita pale na wala haijajikita kwingine.

Kwa hiyo, siyo kwamba mimi *I am trying to reinvent the wheel* hapa, hapana. Sigundai tairi jipya la gari, bali ninajaribu tu kuelezea tu kitu kilichopo, sema ninataka sasa tufanye jitihada za kuwekeza na tufanye jitihada mahsus za kuwekeza kwenye ajira kwa vijana wetu na kuwekeza kwenye uchumi ili tuweze kuja kuvuna baadaye. Wakati natoa maelezo ya hoja yangu nilisema kwamba huwezi kupanda bangi ukategemea kuvuna mchicha. Haiwezekani! Kwa hiyo, ni lazima leo hii tupande mbegu za mchicha ili tuweze kuvuna mchicha huko baadaye. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo mafupi niliyoyatoa, niseme tu kwamba sikubaliani kabisa na mabadiliko yaliyoletwa na Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali na sikubaliani kimsingi tu kwa sababu ninaipenda nchi yangu na kwa sababu leo hii mtoto wangu Khamis

Kigwangwalla *Junior* atazaliwa na kwa sababu nimepata fursa hii ya kuwepo katika Bunge hili Tukufu, natamani nichangie katika kuandaa mazingira mazuri ya ajira kwa *HK Junior* miaka 20 ijayo na hivyo sikubaliani na mapendelekezo ya Serikali. Natamani Tanzania wakati wengine wanatembea, ianze sasa kuruka. Hizi ni changamoto za *generation* yetu na sisi kama viongozi tuliomo ndani ya Bunge ni lazima tuzi-meet.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.  
*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Ole-Sendecka, kisha Mheshimiwa Ester Bulaya halafu nitarudi kwako Mheshimiwa Waziri.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Nimesimama kwa ajili ya hoja iliyokuwa imewasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Khamis Kigwangwalla, kwanza kuiunga mkono, lakini nimesimama kuishawishi Serikali ya Chama changu ikubaliane na mapendelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla. *(Makofi)*

Nataka kusema tu kwamba wote mnazungumza lugha moja, yaani ukiangalia ukurasa wa sita wa hoja ya Mheshimiwa Waziri kwamba anaondoa maneno aliyopendekeza Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla yanayosema kwamba ianzishe mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana kwa kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana Wanaowekeza kwenye Kilimo na Viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo na kuendelea.

Anaondoa hayo anaweka maneno itekeleze mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana ambayo imetengenezwa na Wizara ya Kazi na Ajira ili waweze kuajirika, kujajiri na kuwaajiri wengine. *Literally* mpango ni ule ule na kwa sababu hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla inasema, anataka Azimio la Bunge linaloanzisha mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana kwa kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana Wanaowekeza kwenye Kilimo na Viwanda vyenye Uhusiano wa Moja kwa Moja na Kilimo, sasa mimi ninachosema ni kwamba, kama anachotaka Dkt. Kigwangalla ni kuanzishwa kwa mpango maalum wa kukuza ajira na ndivyo ilivyo kwenye ilani ya Uchaguzi ya CCM, mimi sioni haya maneno mengine tu ambayo *literally* mnazungumza lugha moja.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu sana lieleweke ni kwamba ipo mipango mingi iliyozungumzwa, kwa maana nyingine ni kazi nje nje; nimesikia leo kwa mara ya kwanza; pia nimesikia kuna mpango mwengine wa fedha sijui kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni na Vijana inakuja huko, fedha hizo hazipo! Tuwe na mpango unaoratibiwa na *centre* moja, siyo nyingine Wizara ya Kazi na nyingine Wizara ya Habari, bali tuwe na mpango unaoeleweka.

Nataka niwaambie kwamba ni bahati mbaya sana katika Tanzania ya leo, na hili linatishia amani ya nchi hii huko tunakokwenda kuliko kitu kingine chochote kuliko kansa ya udini, kuliko kansa ya ukabila na kuliko kansa ya ueneo, nalo ni hili; mnapokuwa na Utumishi wa Umma usiokuwa na sura ya nchi kwa maana ya kuona unapoingia

Ofisi ya Umma unakuta taswira ya Tanzania nzima ya makabila 120 na ushehe, mkawa na Utumishi wa Umma unaokaliwa na kabile moja au makabila mawili katika Taifa moja na wakanufaika na keki ya nchi na kwa mgawo wa pato la Taifa ni 80% ni uendeshaji wa Serikali na 20% ndiyo inakwenda kwenye maendeleo.

Maana yake wenyе ajira zile kama Sendeka na wengine ndiyo watoto wao watakwenda kupata neema. Mnajenga Taifa ambalo halina umoja na mshikamano huko tuendako. Unaokoaje hili? Njia mojawapo ni kuhakikisha ajira inapatikana kwa uwiano ulio sawa kama ambavyo ajira inatakiwa pia ipatikane kwa uwiano ulio sawa kwa sura ya nchi.

Mapendekezo ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa sura hii itasaidia kutenga fedha fungu la kutosha kwa ajili ya kuleta mapinduzi ya kusaidia vijana hao ili waweze kujiajiri. Ninyi nyote ni mashahidi, kwenye *source* ya mapato yetu ya nchi ya mchango wetu wa Taifa, Sekta ya Madini inachangia na zipo sekta nyingine mbalimbali zinazochangia. Lakini sekta zinazochangia katika uchumi mkubwa wa nchi na zinazokua ni zile ambazo wamiliki wake sio Watanzania, kwa sehemu kubwa Watanzania wako kwenye Sekta ya Kilimo. Lakini niambie Sekta ya Kilimo inakua kwa asilimia ngapi? Inachangia kwa kiasi gani pato la Taifa? Lakini hao wanaotegemea kilimo ni asilimia ngapi ya Watanzania? Utakuta ni wengi sana na tunataka tufanye mapinduzi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema, Serikali ikubaliane na mapendekezo ya Mheshimiwa Dkt.

Kigwangalla kwa sababu ni mpango tu unatakiwa maalum kwa ajili ya kukuza ajira ya vijana. Uganisheni mipango yote mliyonayo, hiyo iliyopo Wizara ya Kazi na hata Wizara ya Habari, njooni tengenezeni mpango mmoja unaoendana na llani ya Uchaguzi na Mipango ya Maendeleo tuliyokwishajipangia, basi hapo mnakuwa mmekubaliana na Mheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sioni *complication* yoyote na sioni tatizo mtakalolipata kwa kukubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda hapo mbele zaidi ukurasa wa nane...

*(Hapa Kengele illilia Kuashiria Muda Umekwisha)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Ndiyo mwisho? Tayari!

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaheshimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaomba pendekezo la Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla liungwe mkono. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijaendelea, Mheshimiwa Sendeka aliomba asaidiwe kwamba Sekta ya Kilimo inachangia kwenye *DGP* 28.7% lakini vilevile Sekta ya Kilimo inatengeneza ajira kwa 74%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nimpongeze Mheshimiwa Kigwangalla kwa kuleta hoja yake ya msingi inayohusu idadi kubwa ya Watanzania ambao ni vijana na lakini wanapata tatizo kubwa sana la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anatakiwa ajue jambo moja kwamba wakati Mheshimiwa Kigwangalla analeta hii hoja, alikuwa anajua kuna mipango Serikalini. Alikuwa anajua kuna mifuko mbalimbali ambayo imeanzishwa, alikuwa anajua kuna 5% ambayo inakwenda katika mfuko wa vijana kwenye kila Halmashauri na 5% inakwenda kwa wanawake. Lakini alifanya utafiti wa kina akaona hii mifuko haikuleta *impact* yoyote katika kuweza kutatua tatizo la ajira kwa vijana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali yetu ituelewe kwamba tunapoomba uanzishwe mpango maalum, haina maana kwamba wao hawafanyi kazi, haina maana kwamba ile mipango haisaidii, lakini haturidhiki na kasi ambayo ile mipango inafanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sioni tatizo kabisa la Serikali kukubaliana na hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla na kuanzisha mifuko wakati kuna mipango mingine haijaanza leo. Nakumbuka Marehemu Waziri Mkuu - Mheshimiwa

Edward Moringe Sokoine katika kutaka kuhakikisha kuwawezesha watu waweze kujajiri wenyewe, alianzisha mfuko maalum na ulikuwa unaitwa Mfuko wa Rais wa Kujitegemea na lengo lake lilikuwa ni kutengeneza ajira nyingi. Lakini siyo kwamba Serikalini kulikuwa hakuna mipango, ilikuwepo. Sasa sioni kwa nini Mheshimiwa Waziri anakuwa na kigugumizi cha kushindwa kukubali hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi viongozi vijana ndio tunajua matatizo ya vijana wenzetu kwa sababu tunapotoka ndiyo tunakwenda vijiweni, wanatuambia *straight* kwamba tunakwenda kwenye Halmashauri, lakini mpaka sasa hivi nikitolea mfano tu Bunda, Halmashauri ya Bunda imeweza kutoa msaada kwa vikundi vyta vijana viwili, lakini kuna zaidi ya vikundi 50 katika Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu mkubwa na tunaomba asikilize mawazo yetu sisi viongozi vijana ambao tunawakilisha vijana wa Taifa hili wenyewe matatizo makubwa ya ajira, tukubaliane na hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla kuanzisha mpango maalum na ukiwa na mpango maalum haimaanishi ile mpango mingine inakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla moja kwa moja. Tunahitaji mpango maalum na tumegundua kwamba Sekta ya Kilimo inaweza angalau ikaondoa ama kupunguza tatizo hili la ajira na tuwe na mfuko maalum. Hakuna tatizo, hata kama kuna mifuko mingine, kama tatizo limezidi kuwa kubwa, kuna tatizo gani la kuendelea kuanzisha mifuko mingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa mara ya pili ili nijaribu *ku-respond*.

Kwanza, mimi nakubaliana na mtazamo wa pamoja kwamba ajira ni *issue* katika Taifa letu kama ilivyo katika dunia nzima, taarifa za *ILO* mmezikia. Hapo hakuna ubishi.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa tunachozungumzia hapa ni jinsi ya *ku-approach* suala zima la ukosefu wa ajira na hasa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, unaposema uanzishe mpango maalum ambao Serikali itaugengea Shilingi bilioni 200 kwa mara ya kwanza na kila mwaka Shilingi bilioni 100 na kuendelea. Swali linakuja kwamba: Je, hao vijana umeshawaandaa kupokea hizo Shilingi bilioni 200? Kwa sababu nimesema tatizo la ajira siyo mapesa, pesa zipo. Mtakumbuka mabilioni ya Kikwete yalitolewa tulipoanza tu awamu ya nne ya mwaka 2006 chini ya Baraza la Uwekezaji, lakini: Je, pesa zile vijana walizichukua na wakafanya biashara na ujasiriamali? Shilingi bilioni moja kila Mkoa! Kwa hiyo, tatizo kubwa tulilogundua sisi ambalo tumekaa na Wizara hii na Wizara ya Kazi, kuhusu vijana, kwanza ni mtazamo chanya au hasi kuhusiana na suala zima la ajira. Kijana haamini kwamba ajira pia ni katika

ujasiriamali hasa vijana wetu waliosoma. Mtazamo huu siyo kwa vijana tu, bali pia ni kwa sisi walezi tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge na wazazi. Ungependa mtoto akimaliza Chuo Kikuu apate kazi ofisini na siyo aende shambani na ndiyo maana vijana wana-move kutoka Vijiji kuja Mijini kwa ajili ya kuogopa kwamba kazi ya shamba siyo ajira tena.

Kwa hiyo, kabla hujaanzisha huu mpango, ni lazima kwanza uangalie mipango mingine iliyopo ambayo sasa hivi tumesema mipango hii sasa iwatambue vijana kuanzia kule kule waliko, yaani Mikoani na kwenye Halmashauri.

Nina mifano mingi hapa! Hapa Dodoma peke yake kuna vijana kule Chinangali wamelima ekari karibu 200 na zaidi na ninafikiri alianzisha Mheshimiwa Lukuvi alipokuwa Mkoo wa Mkoo hapa. Wamepata Shilingi bilioni 251. Wale vijana ukiwaambia watafute sijui mkopo mwengine mahali, hawakuelewi kwa sababu tayari wameshakuwa *mobilised* na Mkoo na wanatumia fursa zilizopo katika Mkoo wao. Uwaambie wakakope Dar es Salaam pesa, kwanza hiyo hali ya kwenda kukopa Dar es Salaam hawana.

Kwa hiyo, tunasema vijana kule walipo wawe *mobilized* kama sasa hivi inavyofanyika. Wakuu wa Mikoa wote wameshaitikia suala hili na kwa taarifa yenu tunapozungumza, Wizara yangu sasa hivi ipo Mikoani inajaribu kukusanya taarifa zile. Tumepata jumla ya tulivyoletewa, tumemaliza Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, zaidi ya vikundi 2,700 lazima tuvhakiki ili tujue kwamba kweli vipo na mahitaji yao ili sasa kutumia fursa hizi mbalimbali na kama mlivyomsikia Mheshimiwa Rais wakati

wa hotuba yake ya mwisho wa mwaka alisema kwamba kazi iliyobaki mpaka mwaka 2015 ni kuwawezesha vijana kwa kuwapa mikopo ili waendelee kujajiri na hatuwezi kuwawezesha bila kuwatambua.

Kwa hiyo, suala la kwanza ni hivi, ujiulize kwamba huu mpango umeshawatambua hawa vijana ni akina nani? Wako tayari kupokea mikopo? Wana elimu ya ujasiriamali? Wana mtazamo chanya kuhusu suala la Ujasiriamali kama sehemu ya ajira?

Kwa hiyo, mimi ndiyo maana nasema tuendeleze mipango iliyopo na tutumie fursa zilizopo ili twende tukijua kwamba tunakwenda pamoja na vijana wetu, na sera ya ajira ya mwaka 2008 ambayo hatuwezi kuikwepa, inasema, naomba noisome: "Dira na dhamira na malengo ya sera hii ni kuhakikisha kwamba tunajumuisha wabia wengi katika kutengeneza soko la ajira. Wabia hao ni pamoja na wawekezaji ambao tumewatengenezea EPZ na SEZ lakini ni pamoja na sekta nyingine binafsi na zile za umma."

Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba hatuwezi kuweka hili gudulia lote la mabilioni Serikali inatenga. Kwa hiyo, tunahakikisha kwamba watu sasa wapo *hands off*, hatuwahuishi watu wengine katika kutengeneza hizi ajira.

Kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwa kweli tuache kazi ambayo tayari imeshaanza kufanyika katika Mikoa ili tuboreshe mifuko ya maendeleo ya vijana ili ifanye kazi yake na *actually* Mikoa na Halmashauri zimeshaanza kutumia fedha zinazoitwa *on source* ili kuhakikisha kwamba

vijana wanajiajiri wenyewe. Sasa hivi vijana wanaomaliza hata *SUA*, hawa vijana wa Igunga ni wale vijana waliomaliza *SUA*, wameanza kuwa na mtazamo huo.

Kwa hiyo, tukianza tena ku-*duplicate* kazi ile ile inayofanyika, tutakuwa tumeharibu kazi nzuri ambayo imeanza. Labda mtutake tu Serikali kwa kweli hiyo Benki ya Vijana pia ianze ili vijana wapate dirisha la kuweza kukopa kwa urahisi zaidi kama wanawake sasa hivi wanavyopata urahisi wa kukopa na kufanya shughuli zao.

Kwa hiyo, kwa kweli naomba hoja yangu iendelee.

## TAARIFA

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba tukubaliane kwamba kwa kuwa muda wetu karibu unaishia kabisa, nimwombe Mwenyekiti wa Kamati, nadhani Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Waziri wa Kazi - Mheshimiwa Kabaka, Waziri wa Habari - Mheshimiwa Fenella, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Kigwangalla na wengine ambao wangependa kushiriki baada ya kuahirisha shughuli zetu, wakutane mahali ili kuliweka vizuri jambo hili ili tutakapofika jioni, basi tuweze kujua tunafanyaje, kama tunahojiana au tunafanyaje. Nitaomba mfanye hivyo katika wakati huu tutakapoahirisha.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninapokea agizo lako na ningeomba timu hiyo tukutane sasa hivi katika Ukumbi wa Pius Msekwa baada ya kulipokea agizo lako. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na ninakushukuru sana Mwenyekiti wa viwango. (*Makofi*)

Sasa niliahidi kwamba nitatoa mwongozo kuhusiana na lile suala ambalo Mheshimiwa James Mbatia alikuwa amelitoa wakati ule na mimi mwongozo wangu ni kwamba Serikali ilete miongozo tajwa kama alivyoahidi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu hapa Bungeni kuhusiana na masuala haya ya mitaala kabla ya kuahirishwa kwa Bunge tarehe 8 Februari, 2013 hapa Bungeni. Kwa hiyo, huu ndiyo mwongozo ambao ninautoa kwa jambo lile.

Waheshimiwa Wabunge, pia kuna tangazo moja. Mnaarifiwa kwamba ndege za Shirika la Ndege la ATC kati ya kesho tarehe 2 – 4 zinazoelekea Kigoma kutoka Dar es Salaam na kuelekea Dar es Salaam kutoka Kigoma zitakuwa zikitua hapa Dodoma. Ni kati ya tarehe 2 - 4 tu. Kwa hiyo, kwa wanaotaka kusafiri kuelekea Kigoma kuanzia Dodoma na wanaotaka kusafiri kuelekea Dar es Salaam kuanzia Dodoma usafiri wa ndege wa Shirika la Ndege la ATC upo wa uhakika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mwisho, naomba kuwakumbusha kuwa tukishamaliza hili la mabadiliko ya Serikali kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, tutakapoanza jioni yapo mabadiliko ya Mheshimiwa Hezekia Wenje kuhusiana na hoja hiyo hiyo. Kwa hiyo,

nitaomba vilevile myapitie kwa sababu tutapaswa vile vile tuyafanyie uamuzi wa namna ya kuenenda nayo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. Ahsante.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilitfungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kitil*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyotuelekeza Katibu hoja iliyopo mbele yetu ni hoja binafsi ilioletwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla ya kuitaka Serikali ianzishe mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana kwa kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana Wanaowekeza kwenye Kilimo na Viwanda vyenye Uhusiano wa Moja kwa Moja na Kilimo. Tuliishia asubuhi kwa kuwaomba Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Vijana, Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara tatu na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na mtoa hoja wakutane ili watusaidie namna ya kuenenda. Bahati nzuri wamekutana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Ester Bulaya ili tuweze kuendelea.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo unajua tatizo la ajira kwa vijana ni kubwa sana na limeendelea kupigiwa kelele na Wabunge wa rika zote, wazee wameona tatizo hilo, Serikalini wameona tatizo hilo, lakini pia mpaka kupelekeea Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla kuleta hoja binafsi ambayo kimsingi wengi wanaiafiki na tunaona itaweza kuhakikisha inapunguza au kumaliza kabisa tatizo zima la ajira kwa vijana. Sasa baada ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kusoma hoja yake, Mheshimiwa Waziri akawa ameleta mabadiliko fulani fulani na Waheshimiwa Wabunge tukachangia, lengo la kuchangia tumeona mipango mingi utekelezaji wake usingekuwa vile ambavyo sisi vijana tunahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotufanya tuone kuna haja ya hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kuwekewa mkwazo, vyanzo vya Mheshimiwa Waziri ni vile vile, mikakati ni ile ile, lakini kama tukiiboresha zaidi nina uhakika kabisa kutakuwa na vyanzo vya uhakika na huo mfuko wake kuweza kupatiwa fedha za kutosha na lengo letu lile ambalo sisi tunalitaka liweze kukamilika na vijana wa nchi hii waweze kuondokana na tatizo la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa ruhusa yako, naomba nisome mabadiliko ambayo nataka niyafanye katika hoja ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hoja iliyowasilishwa mapema leo hii, hapa Bungeni na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla - Mbunge wa Nzega, akilitaka Bunge lipitishe Azimio la Kuitaka Serikali ianzishe

Mpango Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana kwa kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana Wanaowekeza kwenye Kilimo na Viwanda vyenye Uhusiano wa Moja kwa Moja na Kilimo, kutokana na hoja hiyo Serikali kupitia Waziri wa Kazi na Ajira - Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, alileta mabadiliko ya hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe hoja ya mabadiliko ya hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira kwa mujibu wa Kanuni ya 57 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007 kabla ya kufanyiwa uamuzi na Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo:-

Kuondoa maneno, "Itekeleze Mpango Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana ambao Umetengenezwa na Wizara ya Kazi na Ajira ili Vijana Waweze Kuajirika, Kujajiri na Kuajiri Wengine," badala yake yawekwe maneno yafuatayo kwamba, "Serikali ianzishe Mpango Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana kwa Kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana Wanaowekeza kwenye Kilimo, Viwanda vyenye Uhusiano Moja kwa Moja na Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Sekta nyingine za Kiuchumi." (*Makofi*)

Naomba nirudie, "Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Sekta Nyingine za Kiuchumi." Mfuko huo, hapo baadaye utaendelezwa na kuwa Benki ya Maendeleo ya Vijana ya Tanzania (*Tanzania Youth Development Bank*). (*Makofi*)

Katika hoja ya pili iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri ambayo mimi naomba iondolewe, "Mfuko wa Maendeleo ya Vijana uliopo chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo uboreshwe kwa kuongezewa fedha

kutoka Serikali Kuu na Halmashauri ili vijana wapate fedha za kutosha za kuchukua mikopo ya kuboresha mitaji yao ili kuzalisha ajira nyingi zaidi kwa vijana. Halmashauri zibuni njia na vigezo vya kuwapatia mikopo ikiwemo kuwashindanisha kwenye kuandika maandiko ya miradi na Ofisi za Halmashauri zitoe wataalam kwa ajili ya shughuli hiyo na kwamba vijana watumie fursa nyingine zilizopo Serikalini, kwa wadau binafsi za kupata mikopo yenyé masharti nafuu na riba ndogo."

Sasa naomba iondolewe hii na yawekwe maneno yafuatayo kwamba, "Serikali itenge fedha kutoka kwenye bajeti yake na vyanzo vingine kwa ajili ya mfuko huu utakaotoa mkopo kwa vijana kwa riba ndogo na masharti nafuu".

Sasa naenda kwenye hoja ya tatu ambayo Mheshimiwa Waziri aliiota na mimi naomba iondolewe. "Mikoa iendelee kutenga maeneo maalum ya uwekezaji (EPZ na SEZ) kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ambao watatengeneza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mikoa na Halmashauri ziendelee kutenga maeneo maalum kwa ajili ya vijana kufanya shughuli zao mbalimbali ikiwemo kilimo, ufugaji na aina nyingine za ujasiriamali. Mikoa iendelee kuhamasisha vijana kuhusu kuibua fursa za ajira na kuwatafutia fursa za mikopo zikiwepo za pembejeo na mbegu bora ili kuboresha na kuleta tija katika shughuli zao za ujasiriamali na kuwasaidia kupata masoko ya bidhaa zao".

Sasa mimi napendekeza maneno yafuatayo yawekwe kwamba, "Serikali itenge maeneo maalum ya vijana kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi (*Special Youth Economic Zone*).” (Makofi)

Katika pendelezo la nne la Serikali napenda yaondolewe maneno yafuatayo kwamba, "Serikali kupitia mpango wake wa maendeleo wa mwaka 2011 – 2016 iendelee kuhimiza Wizara, Mikoa, Halmashauri kubuni fursa za ajira kupitia mipango yao ya maendeleo ya kisekta. Sekta hizo ni pamoja na kilimo kikubwa cha kibiashara cha umwagiliaji, viwanda, nishati na madini, miundombinu, ujenzi wa barabara na maeneo mengine yote yanayotajwa katika mpango huu na kuibua fursa za ajira kwa vijana."

Sasa mimi napendekeza maneno yafuatayo, "Serikali kupitia sekta zote za kiuchumi zinazohusika na mpango huu ihakikishe vijana wanafanikiwa kufikia malengo yao katika mnyororo wote wa thamani (*value chain*)."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala kwa kuleta hoja yake na kuanzisha mjadala huu mpana juu ya changamoto zinazotukumba vijana. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, kwa kuleta mabadiliko yake.

Naamini kabisa kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mbunge mwenzangu kijana, hilikuunga mkono katokana na hoja yako kwa sababu nina imani ya dhati, mabadiliko yangu hayapishani na ya kwako, na nina

imani kwa mujibu wa mabadiliko haya yatatoa fursa nzuri kwa vijana na yataleta mwelekeo mpya na matumaini mapya kwa vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya, nakushuru sana na tumekwishaipokea hoja hii. Natumaini Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, kwa kifupi sana sijui kama uko kinyume na hoja hii.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa mara nyingine tena kwa kunipa nafasi hii niweze kuyakubali ama kuyakataa mabadiliko ya mabadiliko ya hoja ya Mheshimiwa Waziri ambayo yamewasilishwa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

Kwa faida ya kuokoa muda, niseme tu kwamba kwa kiasi kikubwa mipango ya Serikali iliyokuwepo, kwa mfano Sera ya Taifa ya Ajira, Mkakati wa Taifa wa Kukuza Ajira, Programu ya Taifa ya Kukuza Ajira, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Mfuko wa Uvezeshaji kwa kiasi kikubwa haijaonesha kuleta ufumbuzi wa tatizo sugu la ajira ambalo tunalo katika Taifa letu. Kwa muktadha huo, ninakubaliana kwa kiasi kikubwa, karibu asilimia 90 na mapendelezo ambayo yameletwa mbele yetu na Mheshimiwa Ester Bulaya kwa sababu kwanza, yamebadilisha tu maneno katika hoja ya awali ambayo niliwasilisha hapa Bungeni asubuhi. (*Makofii*)

Pili, yamejitahidi sana kumwokoa Mheshimiwa Waziri kwa sababu kwa kweli nisingekubaliana na mabadiliko ya

Mheshimiwa Waziri hata kidogo kwa sababu alikuwa amefanya *radical changes* kwenye hoja yangu na ni kitu ambacho nilikuwa niko tayari kukipinga. Lakini mabadiliko haya ambayo yamewasilishwa hapa na Mheshimiwa Ester Bulaya, yanakwenda moja kwa moja kwenye kutekeleza yale yale ambayo mimi nilikuwa nimeyapandekeza, sema kwa lugha nyingine tu. (*Makof!*)

Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa nakubaliana naye, na kwa kuwa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Ukurasa wa 94 na ukirudi nyuma mpaka ule wa 88 inaelezea kuhusu uwepo wa mpango kabambe wa kutengeneza fursa za ajira kwa vijana hapa nchini kwetu, mimi nadhani kwa kuwa tayari tunaanza kuingia katika huu mfuko mpya ambao tunaupendekeza utengenezwe hapa, mpango huu kabambe ambao umeelezwa katika llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) utatekezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na niseme nakubaliana nayo. Nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge watakapopata fursa ya kuchangia, wazidi kuboresha zaidi ni namna gani tutaweza kutatua tatizo la ajira nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla. Sasa Waheshimiwa Wabunge ili kuyarasimisha mabadiliko hayo, naomba kuwahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki mabadiliko haya.  
(*Makofi*)

Sasa kwa hatua hii, yako mabadiliko mengine. Natumaini Waheshimiwa Wabunge mnazo nakala, ni mabadiliko ya Mheshimiwa Ezekia Wenje.

Mheshimiwa Ezekia Wenje sasa ni nafasi yako.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Lakini kwa kiasi kikubwa naona mapendekezo ninayoleta *all most* yamechukuliwa. Mapendekezo niliyokuwa natoa ni kufanya marekebisho kwenye Azimio la kwanza alilokuwa anapendekeza Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naweka maneno haya yafuatayo, hilo Azimio la kwanza lisomeke kwamba: "Serikali ianzishe Mpango Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana kwa Kuanzisha Mfuko wa Mikopo kwa Vijana ambao wataandika mchanganuo wa kibashara utakaoonekana una tija kwa sekta mbalimbali za kiuchumi."

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yangu ilikuwa ni kwamba kwa Azimio alilokuwa analeta Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ilikuwa *lina-confine Youth Development Fund* kama Serikali italianzisha kwenye biashara zinazohusu kilimo au zenye *direct backward linkange* na kilimo kama alivyoeleza Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa natoa hoja kwamba, tunapoanzisha *Youth Development Fund* kama Taifa, liwekwe huru kiasi kwamba kama kuna vijana wanaoweza kuwekeza katika *professional businesses*, kwa mfano, kuna vijana wanamaliza Chuo Kikuu labda wao wamesoma udaktari, kama wao wanaweza wakaji- *organise* vijana watano wanataka kuanzisha hospitali, basi wapewe fursa ya kupata mkopo kwenye hiyo *fund, provided* wataandika *business proposal* itakayoonekana kwamba biashara watakayoanzisha *after some time* kweli inao uwezo wa kurudisha huo mkopo ambao wamepewa.

Kama kuna vijana kwa mfano wako kwenye *IT* wanao uwezo wa kutengeneza *IT Company* na wakafanya kazi na ikaonekana kwamba *business proposal* waliyoandika inao uwezo wa kulipa mkopo ambao wamepewa kutoka kwenye *Youth Fund* iruhusiwe. Kama kuna vijana huko kanda ya Ziwa wanataka kuwekeza kwenye uvuvi, wanunue boti, mitego na waende wavue samaki, *at the end of the day* waje warudishe ule mkopo, waruhusiwe.

Kwa hiyo, mapendeleko ninayoleta ni kupanua hii *Youth Fund* isiwe *confined* tu kwenye mambo yanayohusu killimo. Fursa zipo nyingi, Sekta za Uwekezaji ni nyingi na biashara ziko nyingi, inategemeana tu na mtu atakavyofanya *analysis* na akaona hii biashara nikiwekeza hapa iko *viable* na nitakuwa na uwezo wa kulipa hizi fedha kutoka kwenye *Youth Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mapendeleko yangu ni kuipanua. Tunaweza tukaamua tukaipanua kweli, lakini katika utekelezaji sasa tukaenda kwa *sector by sector*,

labda tukaanza na hiyo ya kilimo, *then tunai-monitor, tunai-broaden*, lakini msingi wa hoja iwe ni kwamba iwe *fund itakayo-involve sectors* zote za uchumi na vijana kwenye aina au shughuli yoyote, watakaoweza kuandika mchanganuo mzuri wa kibiashara, waruhusiwe kupewa hiyo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo msingi wa mapendekezo ya marekebisho niliyoleta hapa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maana yake mwanzoni ulianza kusema kama vile Ester Bulaya amesha-cover mapendekezo yako yote au bado kuna ambayo yako *uncovered?* (*Makofi*)

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa sababu kama nilimpata Mheshimiwa Ester Bulaya vizuri, amesema kwenye marekebisho ya Serikali kwamba iruhusiwe iende kwenye Sekta zote za uchumi. Kwa hiyo, kimsingi na kwa kuwa Bunge tumeishakubali, ninaamini imekuwa *covered*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru. Kwa hiyo, umetoa hoja ya mabadiliko yako!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Sawa Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nashukuru. (*Makofi*)

Mezani hapa nilikuwa vilevile na hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja ya mabadiliko ya Mheshimiwa

Wenje iliyokuwa inaletwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka. Kwa kuwa Mheshimiwa Wenje ameitoa, sidhani tena kama kuna haja.

Mheshimiwa Ole-Sendeka!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE- SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Wenje kwa kuondoa maneno haya baada ya kuona kwamba Mheshimiwa Ester Bulaya amezingatia msingi mzima wa sekta mbalimbali za kiuchumi kama alivyojenga Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mimi naondoa ya kwangu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna marekebisho yangu niliyawasilisha sijayaona yakisambazwa, ningependa kujua tu nini kinaendelea?

**NAIBU SPIKA:** Kwenye hoja hii hii?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kwenye hoja ya Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

**NAIBU SPIKA:** Kwa kweli nina hakika kabisa Meza yangu haijayapata. Makatibu wangu!

**MAKATIBU MEZANI:** Hayajafika Mezani.

**NAIBU SPIKA:** Basi itakuwa bahati mbaya Mheshimiwa Mnyika kwa sababu yanapaswa kuwa Katibu ameyapata kabla. Vinginevyo, kwa hakika baada ya hapa lazima tungeyafanya kazi. Lakini sijapata kabisa nakala yoyote na Makatibu wangu wanasema hawajayapata.

Kwa hiyo, tunaendelea na uchangiaji wa kawaida. Kwenye uchangiaji kama utakuwa na neno, basi utaniambia.

Katika uchangiaji wetu, mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kimsingi siko mbali kabisa na hoja hii, naiunga mkono. Ni hoja ambayo ni ya msingi ukizingatia katika Bara zima la Afrika tatizo hili la vijana limekuwa ni kubwa sana na Tanzania ni mojawapo ya tatizo hili kwa vijana ambao hawana ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa mapendekezo yaliyobadilishwa kwa sababu mwanzoni hoja ilibana kidogo *as if* watu wote ni wakulima. Lakini pamoja na michango mizuri ambayo naamini Waheshimiwa Wabunge wengine wataichangia na mawazo mazuri ambayo Mheshimiwa Kigwangalla anayo ya kuunda hii *Tanzania Youth Development Bank*, nilitaka tu nitoe angalizo kwamba kama Taifa tusije tukawa na *quick fix* tukidhani tukimwaga tu fedha kwa vijana tatizo litakuwa limekwisha.

Kwa hiyo, kama Taifa ni vizuri wakati mwingine tuanza kutambua kwamba chanzo cha matatizo haya ni nini? Kwa sababu mwisho wa siku sio wote watakaopata hii mikopo na mimi ningependekeza au ningeshauri kama Taifa tutambue kwamba kama mabadiliko aliyoyatua Mheshimiwa Ester Bulaya tuna watu tofauti tofauti, na kwa bahati mbaya kama Taifa au Uongozi wa kisiasa tuwaaminisha vijana kwamba fursa zinakuja kwa vijana kwa pamoja. Mimi siamini kama kuna fursa za pamoja, kila mtu anapata fursa yake kutegemeana na weledi na *skills* alizonazo na ndiyo maana ninawashukuru hawa wengine waliopanua wigo kwamba tusiwaelekeze vijana kwenye kilimo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo langu kubwa ambalo naliogopa hapa ndiyo maana nimesema wakati mwingine tunadhani tukitumbukiza fedha tu tunakuwa tumetatua hili tatizo. Nilipokuwa Chuoni, nilijifunza kwamba nilipojaribu kuangalia tatizo lazima niangalie mambo manne. Kitu cha kwanza lazima nifanye *observation* na hiyo *observation* ninavyofanya ni lazima iwe ya kina, uwe na *information* za kutosha kujua tatizo ni nini? Ukisha *observe* unafanya *interpretation* kulingana na mazingira uliyonayo na baada ya ku-*interpret* unaanza kujua kwamba tatizo hili tulitatuue kwa namna gani, na utajua kipi cha kufanya ambayo ni *application*, mwisho utakwenda ku-*implement*.

Sasa tatizo kubwa ninaloliona ambalo vijana wengi ambao hawana hata ajira wanazidi kuzaliwa katika Taifa letu, bado narudi katika hoja ya jana ambayo tumeijadili, ni mfumo mzima wa elimu ambao tunazalisha vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, tuna mfumo wa elimu ambao tunazalisha vijana ambao wanapokwenda kwenye maisha halisi wanakuwa *irrelevant*, yaani ni sawa sasa hivi unamwingiza mtoto darasani, unamfundisha kutumia *typewriter* ambapo akienda ofisini hataikuta. Kwa hiyo, pamoja na kwamba tunataka tuanzishe Mfuko huu, kwa sababu wanafunzi wanaomaliza Vyuo Vikuu sasa hivi wanazidi kuongezeka, swali ambalo kama Taifa pamoja na kwamba tunaweza tukapata Mfuko huu: Je, hawa wanaozidi kuzaliwa tunawaunganishaje? Kwa sababu kama tatizo hili hatujalichambua kwa kina, pamoja na kwamba tutafungua Benki, tunaunganishaje kile tunachokifundisha kwenye jamii na wanapokwenda kwenye soko lililopo? Kwa sababu tuna vijana wengi ambao wanamaliza Vyuo Vikuu, wengine wanamaliza Diploma wanapokwenda kwenye soko hawatatui majibu ya matatizo yaliyopo kwenye soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nimezungumza hapa nimesema *education should be dynamic, education is not static*. Sasa tuna elimu ambayo changamoto tulizonazo sasa tunatoa elimu ambayo haijibu changamoto tulizonazo za wakati huu. Kwa hiyo, utakuta matatizo mengi ambayo vijana wanakutana nayo ni mara nyingi hawana *information* za kutosha kulingana na soko la ajira lililopo. Kwa hiyo, hata tukitoa fedha nyingi, tukafungua Benki nyingi, hawa vijana tutaendelea kuona kwamba wanakosa ajira kwa sababu hawa-*meet needs* za mahali pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nilikuwa nashauri, kama wanasiasa, kwa sababu tuna vijana wa aina

mbalimbali, tunao wengine wanapenda kulima, tunao wengine wanapenda kufanya biashara, amezungumza Mheshimiwa Ezekia Wenje hapa wengine wanataka kufanya useremala, wengine wanataka kufanya uvuvi, kule kwetu wanapasua mbao kule Mufindi, wengine wanalima mahindi kule Ismani kwa Mheshimiwa William Lukuvi. Sasa tuna vijana wa aina tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani kama Taifa na tukubaliane kabisa wote hapa kwamba mtu analipwa *you get paid for the value you bring at the market place*. Unalipwa kutegemeana na thamani unayoipeleka kwenye soko. Kwa hiyo, ni wakati wetu muafaka kama wanasiasa na Taifa kuhakikisha tunawa-*encourage* vijana kwamba hakuna fursa za vijana wote wakija kwa mfano, Mjiini Iringa wakija kwa pamoja hakuna fursa za pamoja, fursa zipo tofauti tofauti inategemeana na kijana mmoja mmoja anaboresha *vipi value* yake yeye mmoja.

Kwa hiyo, tunge-*encourage* hii elimu ya watu tofauti tofauti katika maeneo tofauti tofauti kusudi huu mfuko uweze ku-*accommodate* watu tofauti tofauti badala ya kuwaelekeza kama ilivyokuwa mwanzoni. Kwa sababu watu wana uwezo wa kufanya shughuli tofauti tofauti na tuwaelimishe vijana. Kwa sababu mara nyingi wanasiasa tukienda huko tuwaaminisha vijana kwamba tukipeleka fedha tutatatua matatizo na kumbe fedha siyo suluhisho, tuwaaminishe vijana kwamba wakikuza *skills* zao na bahati mbaya duniani kote, *people do not buy average*, watu wanataka kununua *the best*.

Kwa hiyo, huyu kijana kama akiwa Mhasibu, ili aingie kwenye soko la ushindani lazima awe *the best*. Huyu kijana kama ni mwimbaji, ili aingie kwenye soko la ushindani, *CD* yake inunuliwe, lazima iwe *the best*. Watu hawanunui *average*.

Kwa hiyo, badala ya kuwaaminisha vijana kwamba tukimwaga fedha nyingi matatizo yatakwisha, tutakuwa tunalidanganya Taifa hili. Kwa hiyo, ni wakati muafaka kwamba tuhakikishe tunatoa elimu ambayo ni muafaka katika sekta mbalimbali kwamba hawa vijana wanapokwenda kwenye soko waweze ku-*compete* na soko la ajira mahali wanapokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawiwa sana kwamba Tanzania siyo kwamba ajira hazipo isipokuwa mazingira yetu hatujayatengeneza vizuri. Kwa mfano, kama Taifa, tungeweza kukaa kuangalia tuna kitu gani? Kwa mfano, sasa hivi tunajadiliana tuna gesi, tuna *uranium*, tuna mbuga za wanyama. Lakini ni kwa kiwango gani kama Taifa tumeweka msisitizo wa kusomesha vijana wetu?

Kwa mfano, sasa hivi tunagombana mambo ya gesi, ni Watanzania wangapi wanaenda *deep sea* kule ambako gesi ipo? Ni Watanzania wangapi wana utaalamu wa mambo ya *uranium*? Ni Watanzania wangapi wana *skills* za mambo ya utalii ambao wakienda kwenye soko la Kimataifa wana-*compete*? Ni Watanzania wangapi wana *skills* za mambo ya *Hunting*? Sasa haya mambo kama Taifa tungelitakiwa kwenye maeneo hayo tuwekeze zaidi, tuwaelimishe na hawa watu wawe na uwezo wa kupambana na masoko ya kidunia badala ya kufikiria tu

kwamba tukimwaga fedha, tukifungua Benki, kwa hiyo, mambo yatakuwa safi. Kama Taifa, tutakuwa tunajidanganya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba wanasiasa wenzangu, hebu tusaidie kwa sababu *barrier* zinazowafanya watu wasiingie kwenye soko la ajira zipo nyingi sana. Kama nilivyosema wengine hawana *network*, hawajui *ku-connect*, ukiangalia dunia ya sasa hivi inakwenda kwa kasi sana. Kwa hiyo, kama sisi tunatembea na hatuwezi kuwaunganisha na jinsi ulimwengu unavyokwenda, siku zote hawa wenzetu wanaotaka ajira na wanakosa ajira watakuwa nyuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nihoji, pamoja na kwamba hoja ya jana ilikwisha, lakini chimbuko kubwa la matatizo la ajira zetu ni suala la aina ya elimu tunayowapa vijana wetu. Kama Taifa, ni wakati muafaka wa kukaa kuona ni Taifa la namna gani tunataka tulizalishe? Kwa hiyo, *we have a need* kama Taifa, lazima tukae, tuna tatizo la elimu tunayoitoa, inajibu changamoto tulizonazo? Kwa sababu elimu lazima ikabiliane na changamoto tulizonazo na mojawapo ya changamoto tuliyonayo ni *unemployment*. Swali ni kujiuliza, elimu tunayotoa ina-solve vipi tatizo la *unemployment* katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunatakiwa tukae kama Taifa, tunahitaji moja, mbili, tatu, nne na tunataka tuzalishe Taifa la namna gani? Tutoe elimu ya namna gani ili tuwe na kizazi kinachokuja cha namna gani? Kwa sababu *garbage in, garbage out*. Wakati mwingine tunagombana

sana hapa, lakini inategemeana na mtu amejaza nini kwenye ufahamu wake, ana falsafa ya aina gani inayoongoza maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vijana wengine tunawalaumu Mitaani ni kwa sababu falsafa waliyonayo kuhusu maisha, tumefika mahali kama Taifa tunawaaminisha vijana kwamba wakikaa tu, Mbunge atamwaga fedha, Benki zikija watakuwa wanakaa, hakuna kazi. Tunajidanganya wenyewe!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi siko mbali na hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla, naunga mkono sana, lakini tusipokwenda kwenye kiini cha tatizo, tutakuwa hatutatui tatizo kwa sababu mwakani tena wanakuja wengine wanamaliza Vyuo Vikuu. Mimi kama Mbunge pale ofisini kwangu, wanakuja vijana wengi waliomaliza Vyuo Vikuu, wanasema Msigwa tutafutie kazi. Lakini mimi ninawaambia ukweli, hakuna kazi. Bahati mbaya Serikali hamsemi ukweli kwamba *there is no jobs!* Hamsemi! Tunatakiwa tuwaambie! Kwa bahati mbaya, hata elimu tunayowapa wakienda kutafuta kazi, hazipo zinazolingana na elimu tunayotoa.

Kwa hiyo, kama Taifa ni wakati muafaka. Narudia tena, tukicheza na elimu ambayo tumekuwa tukizungumza hizi siku mbili zilizopita hapa, tunaliua Taifa letu, Taifa linakuwa halina *future*, linakuwa halina mwelekeo kwa sababu lazima tuamue tunataka kuli-*shape* Taifa liwe la namna gani. Tunataka kuli-*shape* Taifa la namna gani? Ni aina gani ya elimu tunayo *invest* kwa watoto wetu? Lazima tuamue *what type of education we want to invest to our*

*kids?* Tunataka baada ya miaka 10 tuwe na utaalalm wa aina gani? Kwa mfano, Mungu ametujalia, tuna gesi hiyo, baada ya miaka kumi tumeandaa tunataka tuzalishe wataalam wa gesi wangapi ili tupunguze tatizo hilo. Hatutalitoa, tutalipunguza kwa kiasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya miaka 20 tunataka tuwe na watu watakaoingia kwenye *hunting industrial*. Kwa mfano, Wizara ya Maliasili ndiyo inatoa pato la pili kwa madini. Katika Idara hii, tumepeleka watu wazuri kiasi gani ambao wakiingia kwenye soko wana-compete na watu wengine? Lakini mpango huu kama Taifa, hatuna. Kwa hiyo, tumekuwa tukigusa, tunaendeshwa na watu wengine kitu ambacho tusipokuwa waangalifu hata tungemwaga fedha nyingi sana, hili tatizo hatutaliondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu, ni lazima tuweke watu wenyewe weledi mkubwa katika masuala nyeti kama haya ya elimu, watu ambao sio wababaishaji, watu ambao wana uhakika na kile wanachokizungumza, watu ambao wanajua Taifa letu tunalipeleka wapi, maana hili ni bomu. Niliwahi kutoa methali moja ya kichina siku moja, Wachina wamepitia kwenye matatizo mengi sana, wana methali nyingi sana. Kuna mchima mmoja mpaka huwa anatucheka Watanzania, anasema nyle Watanzania mnaangalia hapa karibu sana, eti mna *vision* ya 2025, wenzenu tulijenga ile *the great wall more than six hundred years*, yaani wanazaliwa watu wanakufa, *vision* haijkwisha, wanazaliwa wanakufa *vision* haijkwisha. Anasema, mnaangalia hapa! Anasema *the Chinese great wall...*, kile Kiingereza cha Kichina, mnakijua!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema, kama tusipoangalia mbele kama Taifa, tusipoona kama Taifa, tunaua kizazi chetu. Naomba hebu tuwe wakweli, tuwatendee haki watoto wetu, tuwatendee haki kizazi chetu kwamba waone kuna watu katika Bunge la Kumi walioona tatizo hili wakalitatu.

Ningeomba wale wanaosimamia masuala nyeti, masuala haya ya elimu, masuala haya ya kutatua matatizo ya vijana, ambalo kimsingi ni bomu, na Wachina hii methali niliyosema wanasema *hivi*; "*It is not economical to go to bed early and save all the candles if the result is twins.*" Siyo jambo la kiuchumi kwenda kulala mapema ili mishumaa isiteketee, matokeo ya kulala mapema utazaa mapacha. Kwa sababu kuzaa mapacha ni gharama kubwa kulea kuliko kuteketeza mishumaa. Kwa hiyo, tuone kwamba hili bomu lazima tulitoe mapema, tusije baadaye tukazaa mapacha ikawa tatizo. Kwa sababu hawa jamaa wakikosa hela watakuwa kwenye mageti yetu, watavunja, hatutakuwa salama.

**NAIBU SPIKA:** Mchungaji, kuhusu utaratibu. (*Kicheko*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hata mimi ninao, watakuja kwenye mageti yetu, watavunja nyumba zetu kwa sababu watakuwa na njaa. Kwa hiyo, tulione hili tatizo la pamoja, lakini tutafute *solution* ambayo ni *permanent*. Hii ya Benki ya Fedha mimi naona ni *temporary*, lazima tuwa-*inspire* vijana, tuwa-*motivate* vijana wawe na *vision* wawe *inspired*, kila mtu ajione anaweza na abebe *log skills* zake aongeze *skills in the market place* kwa sababu *you get paid for the value, bring to the market*

*place. Siyo kwamba unakuja tu na mwisho watu hawanunui average, they buy the best.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

## TAARIFA

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tundu Lissu nimekuona.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kutoa taarifa tu kwamba Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ni baba wa mapacha, na mimi vilevile ni baba wa mapacha. Sasa ina maana yeye alizima mishumaa mapema na kwamba hao mapacha wake ni shida? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kwa kuwa ni Mchungaji, hatakiwi kujibu hiyo hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa James Mbatia nimekuona!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba Mwongozo wako Kanuni ya 68(7) inasema: "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu

jambo ambalo lilitokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hili linaloruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa."

Halafu naomba nirejee Kanuni ya 55(3)(f) kuhusu hoja zifuatazo zinazoweza kutolewa bila taarifa. (f) inasema: "Kuhusu jambo lolote linalohusiana na haki za Bunge."

Sasa naomba nisome haki ninazosemwa za Bunge, ni Kanuni (63) (1): "Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuathiri uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni, na kwa sababu hiyo, Mbunge yejote anapokuwa akisema Bungeni, ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au kubahatisha tu."

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumia kanuni hii kuomba Mwongozo wako kwa sababu leo asubuhi nilipoomba nakala ya Mitaala, nilisoma *Hansard* hii na maamuzi yako uliyoyatoa ni kuhusu *Hansard* hii. Pia niliomba Mheshimiwa Waziri Elimu alipokuwa anachangia hoja yangu alionyesha mitaala hapa na Watanzania wote waliiona na jana aliitoa vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mitaala hiyo ije Mezani kwako ili tuweke kumbukumbu sahihi za Bunge lako Tukufu, kwa kuwa jana nilitamka mwenyewe kwamba, kama ipo rasmi niko tayari kuondoka kwenye

nafasi yangu. Hii ya majadiliano ambayo iliombwa tangu mwaka 2012 Oktoba, Bunge hili halijamalizika na maamuzi yake kwamba iletwe wiki ijayo tunakubaliana nayo. Lakini niliomba mimi binafsi, mtoa hoja nakala aliyokuwanayo iwekwe Mezani ili kujiridhisha. Hata nilipomwandikia Mheshimiwa Kawambwa, "Naomba hiyo nakala yako kwa kujiaminisha, mitaala rasmi ya mwaka 2002. Natanguliza shukrani, J. Mbatia tarehe ya leo." Akanijibu, akaniambia: "Kopi yangu nimeichorachora, nimekuagizia nyingine, naamini utaipata leo."

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi hata hiyo kopi sijaipata, nilikuwa naomba ile ilioonyeshwa kwenye Bunge lako Tukufu leo asubuhi iweze, ikawekwe Mezani ili kujihakikishia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Nimekusikia Mheshimiwa James Mbatia na nitatoa Mwongozo wangu baadaye. Mheshimiwa Rikizi Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Msabaha.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nitoe shukrani za dhati na nimuunge mkono kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa hoja yake aliyoleta ambayo ni hoja nzuri yenyе mashiko na ambayo nina imani kuwa itawasaidia vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi ni Mkao ambao umewatoa vijana wengi kuja Dar es Salaam kutafuta mazingira mazuri ya maisha, na ndiyo maana tunasikia Lindi kuna Wamachinga, Wamachinga

wanapatikana Lindi lakini amekuja kule kutokana na mazingira yaliyompelekea kwenda Dar es Salaam na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii katika ukurasa wa sita, upatikanaji wa ardhi kwa vijana Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Mtwara ni baadhi ya Mikoa ambayo ina ardhi na ardhi yenyewe ni kubwa, lakini mpaka sasa hivi vijana hawana ardhi. Kama kijana hana ardhi, anategemea nini? Kwa vile Mkoa wa Lindi hauna viwanda angalau angepata kazi katika viwanda tulitegemea ardhi itakuwa mkombozi mkubwa kwa mwananchi na kijana wa Lindi.

Hivyo, angalizo Mkoa wa Lindi tayari tumeshapeleka vikundi vya kuhamasisha vijana wapate ardhi yao, na hivyo vikundi vinaitwa amsha. Nia na madhumuni ya kuamsha vijana wa Lindi na wazee na watu wengine kuhakikisha wanapata ardhi, na hii inatokana na kwamba ardhi sasa hivi inapokonywa na wageni na hii haina kificho. Kijana amezaliwa katika Kijiji, anahitaji yake angalau eka kumi ili na yeye aweze kujivunia katika ardhi yake, anayo eka kumi. Lakini upatikanaji wake umekuwa wenye bugudha.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii bahati nzuri tumefika katika hoja ambayo Mheshimiwa Kigwangalla ameileta hapa, italeta mwamko kwa kila kijana ajione ana ardhi katika mkono wake amekabidhiwa. Hii italeta changamoto kwa vijana kuacha kukimbilia Mijini na kukaa vijijini wakiendelea na ardhi yao na iwekewe mazingira ili ile aweze kuitumia ardhi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ardhi tuliyokuwanayo, ukimwuliza kijana atakwambia mimi niko katika shamba la baba yangu ambalo saa nyingine itakuwa ni ekari moja, mbili au nne. Ardhi ile haina hati, hivyo bahati mbaya ikipita barabara, yule mtu anasombwa na kuzolewa kana kwamba yeye pale hajazaliwa, hajaishi kwa miaka mingi na anachokipata hakitamtosheleza wala hakitamnufaisha katika miaka ya baadaye. Tunaona ni suala dogo, lakini ni suala ambalo limetufanya, kwa sasa hivi tujione kama sisi ni watu wa kwenda kuwasaidia, tuwe Mabalozi wa kwenda kuwapelekea wananchi wetu tuwatambue na wao wapate ardhi yao ili iwasaidie katika suala hili ambalo amelileta Mheshimiwa Kigwangalla ili liwasaidie katika maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano leo umempa ardhi mwananchi wa Matakwa, Kijiweni, Milola, lakini miundombinu ya kule hakuna barabara, maji na umeme na amelima amepata ufuta anashindwa kuupeleka sokoni ule ufuta wake. Hivyo, pamoja na wazo ni zuri lakini iendane na miundombinu ya barabara, maji na umeme. Kwa mfano, leo kuna Mikoa mingine hawapati taabu ya umeme, hawapati taabu ya maji na wala hawapati taabu ya barabara, itamsaidia kujiendeleza kuliko yule mwananchi aliyekuwa Kineng'ene. Bado mwananchi wa Kineng'ene, Nachingwea atakuwa anapata taabu kwa vile hana umeme, maji wala barabara. Hivyo, hii changamoto iwe changamoto ya kuhakikisha Serikali Mikoa ile ambayo iko nyuma hasa Lindi ipewe kipaumbele na ionewe huruma.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikwambie vitu ambavyo vinaniletea changamoto kila siku kuvihoji na kila siku utasikia kuna miradi ya maendeleo inapelekwa katika Mikoa mbalimbali. Nanukuu ukurasa wa nne: "Juhudi za Kisekta. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Shirika la Chakula (*FAO*) tayari ilishabuni miradi ya kupeleka maendeleo ya ajira ya vijana vijiji." Lakini katika miradi hiyo, Lindi haipo na wala Mtwara haipo. Kwa nini nazungumza hivi na kila siku nakuwa mlalamishi humu ndani? Imekuja *SAGCOT* (*Southern Agricultural Corridor of Tanzania*) Lindi na Mtwara haimo. Sasa unategemea watu wale waende wapi wakapate ajira? Ikiwa ardhi zipo kule Kusini, miradi ya kilimo haipelekwi, miradi ya kisekta haipelekwi, hawa wananchi wataishi ishije? Ni kero! Serikali kila siku inazungumza kwamba Mikoa ya pembezoni tunajaribu kuipa msaada. Hakuna! Bado watu wa Lindi tunahangaika kwa ajira ya vijana wetu, wako katika hali ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali sikivu iangalie kwa macho ya huruma, Lindi hakuna kiwanda hata kimoja, Mtwara hakuna kiwanda hata kimoja, wamekuja wawekezaji wababaishaji wamechukua viwanda vya korosho wamekaa navyo mfukoni. Leo unategemea mtu huyo atapata wapi kazi au atapata wapi ajira na akija Kariakoo huyu Mmachinga fukuza, anakimbia ovyo ovyo, na mitumba yake wananyang'anywa, wanafanywa kila aina ya kudhalilishwa. Tunaomba Serikali sikivu iangalie suala la Wamachinga, mkawawekee mazingira mazuri ili Wamachinga warudi kwao wakafanye kazi na wana uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kusini wa Mkoa wa Lindi na Mtwara tulipelekwa Trinidad & Tobago hapa ndiyo sehemu yake angalau kile kidogo tulichokuwa nacho mwone faida tulizokwenda kupata kule katika ile semina. Trinidad & Tobago wanaofaidika na uchumi wa Trinidad & Tobago siyo wana Trinidad. Wana-Trinidad wako pale wanasuka rasta tu, lakini wanaofaidika na ule uchumi ni wageni, wamehodhi ardhi yao, wao wamekuwa watu pale kama Wamachinga wa kupita, kukimbia kimbia na kufukuzwa fukuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali sikivu illione hili kwa ardhi, hii wanaopita kukimbia kimbia, watu wako maporini wanachukua ardhi ya Tanzania, itakuwa mwisho wake. Mtanzania hana ardhi. Sisi tunachukua ekari tatu, wao wanachukua ekari 10,000 baada ya muda mfupi ile ardhi itakuwa imekwisha, sisi wenyewe tutakuwa kama Wa-Trinidad tunasuka rasta.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kuna Vyuo vya VETA vimejengwa Lindi na Mtwara. Ningombaa Serikali iviangalie vile Vyuo itengeneze mitaala kwa ajili ya kuwasomesha vijana katika sekta hili ndogo ya petroli ili angalau litakapokuja suala la gesi wapate kazi ya kuajiriwa katika kazi ndogo ndogo.

Leo hii tuna Vyuo kama *D/T* mitaala ya *Petroleum Engineering* na sekta zake mpaka za chini zifunguliwe katika VETA zetu ili watoto wasome ili wakishamaliza kusoma wapate ajira. Matokeo yake tutakuwa na gesi, sisi itakuwa

kazi yetu ni kufagia na kutakuwa kuna gesi, sisi tunakwenda kuosha vyoo vya wawekezaji. Heshima iko wapi katika nchi yako? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipofika Trinidad & Tobago wametoa *offer* kwa Tanzania, baadhi ya Watanzania wakasome. Waganda wamechangamkia, Wa-Angola, Wa-Nigeria sisi ziko wapi hizo *documents* wananchi wetu, watoto wetu watakaokwenda kusoma wamewekwa wapi? Tunatoa makabrasha, watu wanayaweka mezanim lakini matokeo yake wenzetu, ukienda Angola kila mwaka Marais wa Angola wanakwenda kutoa vyeti kwa wanafunzi wao ambao wamepewa *offer* na wakatuambia tena msije Tanzania kwa vile tumejaribu kuwapeni *offer* hamzifanyii kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali mtuulize sisi na baadhi ya makabrasha tumepewa ya kuja kuwapeni mwone jinsi na sisi tunataka watoto wetu wapelekwe wakasome, wakirudi hapa na wao wafanye kazi zile ambazo zinastahili wafanye. Waandisi wetu waende kule wakasome waje wafanye kazi zetu na siyo hivi sasa tunafungua iwe ajira ya wageni.

Tumejenga Uwanja wa Taifa, tumeona mlipuko wa wageni walivyojaa nchi hii, wanakuja kuwekeza kwa kuuza karanga, wanakuja kuwekeza kwa kuuza maua, hawa vijana wetu wanapata kazi wapi? Kila mwekezaji anakuja Tanzania, lakini anakuja na ndugu yake na kabilia lao wanakuja kufanya kazi, tumbakia sisi hapa, tunawapa fursa ya kuzidi kuingiza wao wapate ajira, vijana wanahangaika. Tupate muafaka wa kuwasaidia vijana ili

hawa vijana isije baadaye wakaja kutulaumu mlitengeneza mipango gani ya kutusaidia sisi vijana ili tuweze kupata ajira? Sasa hivi tunaona ni suala dogo la vijana na Vyuo vinazidi kutoa vijana, ajira ziko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe angalizo. Katika Wizara ya Kazi, kuna watu wamewekeza katika ajira, lakini Watanzania hawamo. Kama yumo mfanyakazi wa Tanzania, kijana ana digrii, anapata Sh. 400,000/=.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Taarifa!

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Taarifa nimemwona Mheshimiwa Kessy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anayezungumza kwamba anataka kusema kama nchi hii kiwanda kikijengwa kwa mfano Rukwa, wana-Rukwa ndio wasome wapate kazi. Kiwanda kikijengwa Rukwa ni makabila 124 Watanzania wote na wenyе sifa za kufanya kazi. Imekuwa nongwa Kiwanda cha Gesi Mtwara, basi wao wasomeshe watu wa Mtwara, wafanye kazi watu wa Mtwara peke yao kila kitu watu wa Mtwara! Hiki ni Kiwanda cha Taifa zima kwa ajili ya wananchi wote na faida ya nchi nzima na anayeajiriwa pale ni mwenye ujuzi. Tutapeleka nchi kubaya!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lulida taarifa hiyo!

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijataja hata siku moja kama ni mtu wa Mtwara, nimesema

Watanzania na mimi napenda Watanzania wapate elimu. Sijataja watu wa Mtwara. Nimesema tumekwenda Trinidad & Tobago, nafasi hii ya kusoma iwasomeshe Watanzania, sijataja Mtwara na wala Lindi, ila mabadiliko na mapinduzi ya maendeleo Lindi ipewe huruma. Hilo ndio nimelizungumza. Hivyo, kama anataka kuchekesha watu hapa hatukuja kucheka hapa, tumekuja kufanya kazi kumsaidia na kumkomboa kijana, hatukuja kufanya masihara katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, namuunga mkono Mheshimiwa Kigwangalla kwa hoja yake nzito na nina imani Serikali itaifanyia kazi na vijana watapata ajira na watapata kazi katika mazingira mazuri yatakayowafikisha katika muafaka na nchi kwenda mbele. Mungu Ibariki Tanzania ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Lulida, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mariam Msabaha.

**MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante name kwa kunipa fursa hii kuchangia hoja hii iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi mkubwa nimeupata humu ndani na tunaposema vijana, vijana wako makundi mbalimbali. Kuna vijana wasomi, kuna vijana wamesoma vizuri tu, vijana ambao wamesoma mpaka Darasa la Saba, Kidato cha Nne, na kuna vijana ambao hawajui kusoma na wala kuandika. Lakini vijana hawa wanafanya biashara nzuri sana na wanafanya biashara

ambazo hata ukiona unaweza kusema ni kijana wa Chuo Kikuu anafanya biashara hizi.

Sasa mnavyosema mkopo huu wapewe wasomi wa Vyuo Vikuu, mimi hapa napata kigugumizi kikubwa sana. Tukiangalia leo Jiji la Dar es Salaam wamejaa vijana wengi wafanyabiashara ndogo ndogo na hata ukiangalia wale vijana ambao wanaendesha boda boda ni vijana ambao wengine ukienda mle ndani ni vijana wamesoma tu, lakini sasa vijana wale na vijana ambao hawajasoma tutawaweka katika kundi gani katika Mfuko huu? Tutenganishe tuangalie vijana wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie mfano kidogo tu wa mabilioni ya Kikwete. Mabilioni haya kwa Tanzania Bara yaliitwa mabilioni ya Kikwete kwa Tanzania Zanzibar yakaitwa mabilioni ya Mheshimiwa Amani Abeid Karume ambayo sasa hivi ni Rais Mstaafu. Tuangalie Mfuko huu uliwanufaisha akina nani? Pesa hizi zilikwenda wapi? Pesa hizi ziliwanufaisha watu ambao sio vijana, watu ambao sio wajasiriamali na leo hii ukisema kama Mfuko huu uende Vyuo Vikuu, mimi hilo nalikataa.

Lingine kuhusu huu Mfuko, pia napata kigugumizi. Sisi kama Tanzania upande wa Zanzibar, Mfuko huu tunahusika humu ndani au hii ni danganya toto tu? Mambo mengi yanaishia kwenye makabrasha. Hili pia tunataka tupate ufanuzi wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tuangalie kuna Mikoa mbalimbali ambayo inaongoza kwa matunda, kwa mfano Bagamoyo. Ukiangalia Bagamoyo kuna mananasi na

msimu wa mananasi, yanakuwa hata hayana mahali pa kwenda. Lakini kama tungekuwa tunajenga viwanda, Serikali kwenye Mfuko huu huu tukashirikiana na *SIDO* tukajenga viwanda vidogo vidogo kwenye Mikoa ambayo ni ya matunda tukapata viwanda vile vya kusindika matunda na vijana wengi wakaingia mle wakapata ajira na hili wimbi la vijana kukimbilia Mijini pia lingepungua. Lakini tunaangalia hapa, jamani na mimi kuna kitu nasema tuangalie msikumbatie sana mambo. Wasomi, wasomi! Wasomi wengine wanatupeleka pabaya. Hawa wasomi wengine ndio wanaiba Serikalini jamani! Hawa wasomi ndio wameifikisha Serikali hapa! Samaki akioza mmoja, ni wote wameoza!

### **WABUNGE FULANI:** Sema!

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Nasema hawa wasomi kila siku atakuja mtu ataandika hapa atatumia vijana, vijana; vijana hawanufaiki! Mchanganuo, mchanganuo; mchanganuo hauchanganuki! Tuangalie kabisa jamani vijana na wapiga kura wenu kwanza naanza kuwaambia wapiga kura wenu ni vijana, hao hao masikini, hao hao waendesha boda boda, hao hao Wamachinga wanaouza vichupi Dar es Salaam, ndio wapiga kura wenu! Ni kwa nini msiwawezeshe? Mnapopata fursa kama hizi zinakuja msiangalie tu vijana wa Vyuo Vikuu, mwangalie na wale wapiga kura wenu walivyopigika. Leo hii kila Mbunge ukimwangalia hapa ukienda Jimboni kwake ana takribani karibu hata vijana 100 hawana ajira, tena hao ni kidogo. Hawa nimetaja ni kidogo na ukiwaangalia vijana ni wale wale mnaowatumia!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu Mariam Msabaha tunaheshimiana naye sana na mchango wake ni mzuri. Inawezekana alikuwa hajaelewa dhana ya mabadiliko yangu.

Dhana ya mabadiliko yangu ni kugusa vijana wote na wanaofanya biashara zote. Kwa hiyo, itagusa pamoja na hao vijana ambao anawazungumzia walio wasomi, wasio wasomi na wanaofanya biashara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Taarifa ya Mheshimiwa Ester Bulaya, mdogo wangu, kwa sababu katika kusoma hapa, sijaona kabisa masuala mengine, sijayaona! Nazungumza kitu ambacho nina uhakika nacho na naikataa. Nina haki yangu kutetea walalahoi kwa sababu ni walalahoi ndio wamenifikisha hapa, sio kila kitu mchanganuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee. Jamani tunavyofanya kitu, tunavyoangalia, na niliuliza swali hapa nikauliza, jamani, mabilioni ya Kikwete yamekwenda wapi?

Haya mabilioni ya Kikwete yamemnufaisha nani? Lakini jibu hakuna! Leo tukianza kufuatilia, tutakuta zimeishia kwenye mifuko ya watu wachache. Tukiweka kitu tukiweke wazi wazi msiweke kwa kubanabana. Leo tuangalie

mambo ambayo yamepita asubuhi hii, yalikuwa ni masuala mazuri tu, masuala ya kuboresha elimu, masuala mazuri sana, lakini mmejikuta wengine mmejichafua humo humo ndani.

Sasa mtapata shida kweli kweli! Watanzania sasa hivi wameamka, sio vijana wale wa zamani. Kijana awe amesoma, awe amepata elimu, wote tunafuatilia masuala ya Tanzania yanavyokwenda kwa sasa hivi na kila mtu amepigika kwa upande wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu vingine vinavyokuja kwa kweli viwekwe wazi wazi kabisa na hata kama kuna maslahi, basi wote tuungane tuache itikadi ya Vyama vyta Siasa. Kwa sababu hapa tuko kitu kimoja tu. Wengine hapa ni baba zangu, wengine hapa ni mama zangu na wengine hapa ni dada zangu, kwa hiyo, tuko kitu kimoja. Msiseme hiki kitu mtu wa CHADEMA akisema ni kibaya, mtu wa CCM akisema kama kina manufaa pia tukikubali na mtu wa Upinzani akisema wa CUF wa CHADEMA kama kina maslahi na Watanzania tukikubali kwa sababu ni kitu kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nakiomba tuangalie kama mfano Rukwa, Rukwa pia wanalima mahindi sana, wanaongoza kwa kulima mahindi. Lakini sasa tukiangalia vijana wametengewa ardhi, ardhi gani waliyotengewa vijana? Hawajatengewa ardhi!

Kwa hiyo, Serikali itenye ardhi kwa ajili ya vijana, kama kuna matrekta wapewe, kuna zana na leo mkisema sijui mambo ya pesa; pesa ni shetani! Watu watauana na

hakuna kitu cha maana kitakachofanyika na ongezeko la vijana kukimbia Vijiji ni kukimbilia Mijini litaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie kama Rukwa kule kunaweza kukajengwa viwanda vidogo vidogo vya *SIDO* vya kukoboa mahindi na kusagisha kuliko mahindi yetu yakapelekwa Kenya na mahali pengine. Lakini ajira zinapatikana mle mle! Endapo Rukwa kutakuwa na sehemu viwanda vile vya kusagisha na kukoboa mahindi. Kwa hiyo, vijana watakuwa wamebaki Rukwa na mahindi watakuwa wanakoboa kule kule na vijana wanapata ajira mle mle. Kwa hiyo, tuangalie huu mfuko pia u-organise na viwanda vidogo vidogo vya *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia mambo mengi kwa kweli yanatia uchungu mkubwa sana. Kwa kweli hata tukisema hawa vijana ambao wamesoma elimu ya juu sio wote, wengine wanunuifa na hivi vitu ambavyo tunavipitisha humu Bungeni.

Vitu kama hivi vikishapita na vikishafanyiwa kazi, pia zile pesa kama zinatoka, zifuatiliwe. Kuna wengine wanakuwa wanababaisha mle ndani na vile vitu vinapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo machache. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mariam Msabaha kwa mchango wako mzuri sana. Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mada hii muhimu sana.

Kwanza nianze kumshukuru Dkt. Kigwangalla kwa kuleta hoja ya msingi sana. Tukitaka kuangalia uchumi wa nchi yoyote ile duniani, inategemea sana vijana. Ukisikia nchi yoyote imefanya mabadiliko, hata mabadiliko ya kisiasa, tunategemea sana vijana.

Nguzo kubwa ya nchi yoyote tunayosema nchi inajitegemea kiuchumi, lazima tutegemee vijana.

Sasa nimefurahi sana kuona kwamba hii hoja imekuja hapa Bungeni ili tuweze kujadili jinsi Taifa letu litakavyo-*handle* vijana wetu ili waweze kuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nakubalia kwamba vijana wengi sana katika Majimbo yetu hawana ajira na sisi Wabunge tunasumbuliwa sana na tumeona katika nchi yetu kuna viwanda vingi ambavyo vingine vinafanya kazi vingine havifanyi kazi na bahati nzuri nchi yetu imejikita katika wawekezaji ambao wanatoa ajira kwa vijana wetu lakini hawawezi kumudu kuajiri vijana wote. Sasa ni vizuri taifa letu liwe na mpango mzuri ambao unaweza ukahakikisha kwamba vijana hawa wanaweza kupata maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana katika kuhangaika wao wenyewe kwa kujitegemea wanaweza kubuni biashara mbalimbali. Nawea nikasema nawasifu sana vijana kwa kubuni biashara mbalimbali. Tumeona

Wamachinga Dar es Salaam na miji mingine wanafanya kazi ya machinga lakini vipato vyao ni vidogo sana. Sasa biashara yoyote ili ufanye vizuri ni lazima uwe na mtaji mzuri na njia mojawapo ya kupata mtaji lazima upate mtaji kwa kupidia mkopo; na bahati nzuri katika hoja hii inasema mfuko maalum ambao utawezesha vijana waweze kupata mtaji ambao ni mkopo. Mimi nashukuru sana na hatujasema kwamba vijana wapewe pesa bure, tumesema wanakopa kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba ile fedha watakayopewa inaweza ikawa inajizalisha na ikajizungusha kwa miaka mingi sana. Ndiyo maana tunapendekeza kwamba baadaye itakuwepo Benki ya Vijana ambayo itakuwa inawasaidia vijana kuwapa mitaji na vijana hawa kwa kupidia mitaji hii wanaweza kuanzisha biashara na zile biashara tumesema *related* na kilimo, ukiongelea kilimo kina uwanja mkubwa sana. Maana ukienda kwenye mifugo iko kwenye kilimo, ukienda kwenye uvuvi, ni kilimo na sehemu nyingine. Sasa hii nimeona kwamba ni msingi mkubwa sana kwa Taifa letu kuhakikisha kwamba vijana wale ambao wamesoma na wale ambao hawajasoma ili mradi wanafanya kazi ya kujiajiri wao wenyewe, hii itasaidia sana kuondokana na kero ya ajira katika Taifa letu ili vijana waweze kujitegemea. Vijana tunayo bahati nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja ambayo nimeiona asubuhi, inaonekana kama vikundi vyatvya vijana bado havijatambulika vizuri na tunasema katika Halmashauri zetu au Mikoa inajaribu kuangalia na kutatua hili tatizo kwa kutoa fedha kidogo sana na ule Mfuko wa Halmashauri, nakubaliana upo ambao unasaidia vijana

lakini ni fedha kidogo sana ambazo haziwezi kusaidia katika kutatua tatizo la vijana wetu. Sasa tukiwa na mpango maalum wa kukopesha hawa vijana, ni fungu linatengwa maalum hata kwenye bajeti yetu, kwa mfano, bajeti ya Bunge tukapitisha kwamba kila mwaka tunatenga fedha kadhaa kwa ajili ya kusaidia vijana, tutakuwa tumetatua tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia Tanzania sasa hivi, tuna ardhi kubwa sana na tunasema kwamba ardhi kubwa hatuwezi kuitumia ardhi yote na ndiyo maana kuna sehemu nyingine tunaamua hata kuwapa wawekezaji kwa sababu ardhi ni kubwa, haitumiki. Lakini nataka niseme kwamba hii ardhi sio kubwa ni kwa sababu hatuna mipango thabiti ambayo inahakikisha kwamba watu wote wanapewa maeneo ambayo wanaweza wakazalisha, wakafanya kazi na kuweka viwanda vidogovidogo kwenye ardhi hii, ingeweza kutumika vizuri sana. Ninajua kabisa kuna vijana wengine wapo wanaweza kufanya kazi vizuri lakini kwa sababu hawana ardhi ya kuwekeza, sasa wanashindwa kufanya kazi kwa sababu hawana ardhi lakini Serikali ikitengeneza mpango mzuri wa kuwaunganisha vijana wetu na ikatoa ardhi, badala ya kutoa ardhi kwa wawekezaji, ikatoa ardhi kwa vijana wetu ambao wapo mitaani na ikishatoa ardhi, ikawandaa walewale vijana, ikawapa fedha ambazo ni mtaji, wakaanzisha miradi ya kilimo, hawatakuwepo vijana ambao wanazurura mitaani, vijana watajikita katika kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nimeona vijana wengi wanatumika kwenye siasa kukimbiakimbia barabarani kwa sababu wanaonekana hawana kazi. Lakini

kijana yeote atakayejikita kwenye kazi, hutamwona anatembea barabarani hata ukisema akimbie barabarani hatakimbia kwa sababu atakuwa anatumia muda wake katika kuzalisha mali. Sasa hivi vijana hawatumiki kuzalisha mali na hawana kazi, kwa hiyo wakiona kuna vikundi fulani vinakimbiakimbia barabarani na wenyewe wanakwenda. Lakini wakiwa *busy* na kazi, Serikali ikatengeneza mpango mzuri wakawa *busy* na kazi watakuwa wamejikita katika uzalishaji mali na wanaweza kumudu maisha yao na vijana wengi sasa hivi wanashindwa kujenga nyumba. Vijana wengi sasa hivi wapo vijiweni kwa sababu hawana kazi ya kufanya lakini taifa hili lazima liangalie jinsi ya kuwakomboa hawa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina rasilimali nyingi sana na bahati nzuri katika hoja imelenga kwenye kilimo. Kwa mfano vijana wakianzisha vikundi, wakakopeshwa hata matrekti kwenye vikundi vyao, itawasaidia sana kuzalisha viwanda vya kilimo. Hawa vijana tukasema kwamba pamoja na ile miradi ambayo wataonyesha katika michanganuo na nakubaliana na hoja kwamba tukisema vijana wale watakaoandika michanganuo tu, maana yake tunalenga wale wasomi peke yao. Kuna vijana wengine wana vikundi lakini hawawezi kuandika michanganuo lakini wana-*idea* ya kufanya biashara na kufanya miradi fulani. Kwa mfano, ukienda llula, Ifunda ukienda na sehemu nyingine vijana wameanzisha bustani za kulima nyanya lakini wanalima nyanya mashamba madogo sana kwa sababu hawana mitaji mikubwa. Ukienda kule kwangu, kuna vijana wamejiunda na tayari wana vikundi lakini wanataka kuanzisha viwanda vidogovidogo kama viwanda vya upasuaji mbao lakini wanashindwa kununua

mashine kubwa kwa sababu hawana fedha. Lakini kukiwa kuna mkopo maalum ambao umetengwa kwa vijana, wale vijana wanaweza wakakopeshwa na wakaanzisha viwanda vikubwa vya mbao, wakaanzisha viwanda vidogovidogo kama *SIDO*, wanaweza wakafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi vijana wanaonekana wapo tu. Kwa mfano, tukiangalia wengine wanalima kilimo cha alizeti. Vijana wengi wanalima alizeti, wanapenda kununua mashine za kuchuja mafuta ya alizeti. Kwa mfano, ukienda kule kwangu lhowanza mpaka Idumavanu na vijiji vingine, wanataka kuweka mashine ya kuchuja alizeti lakini kwa vile hawana mtaji, wanashindwa kufanya kazi lakini Serikali ikiwa imetenga fungu kwenye bajeti na sisi Bunge tukapitisha tukasema kwamba lazima vijana wapewe fedha na ufuatiliaji uwepo, bahati nzuri tuna Idara ya Vijana, Idara hii lazima ifanye *monitoring and evaluation* kwa vijana. Kwa mfano, kama wamepwa fedha na wanafanya kazi katika Wilaya zetu, katika Majimbo yetu lazima kuwe kuna ufuatiliaji, je, zile fedha ambazo tumezitoa zinafanya kazi? Ndiyo maana tunasema hizi fedha ambazo zinaongelewa fedha za JK henzieleweki zimekwendaji kwa sababu hakuna ufuatiliaji! Lakini kila kitu kikiwekwa vizuri na kukiwa na ufuatiliaji wa kutosha, lazima utainua kipato cha vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nimeona tumejitahidi kwamba kama Taifa tutoe nafasi kwa vijana waende Jeshini, sio *solution*. Si lazima kijana aende jeshini. Kuna vijana wengine hawapendi Jeshi na Jeshi lazima lijkite katika kuzalisha. Kwa mfano, juzi hapa zimetoka nafasi za Jeshi, vijana wanakuja 200 nafasi zenyewe kwa mfano kule

kwangu zimetoka 28, wanashindwa pa kwenda. Sasa vijana wapo mitaani na sisi Wabunge sasa hivi tunatingwa sana na vijana, vijana wanakuja wamemaliza vyuo vikuu hawana kazi na wanashindwa kwa kutembelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mfano ukiangalia nafasi zimetangazwa kwenye gazeti unaweza ukaona nafasi sita lakini zinaita vijana 200, wanakwenda kwenye *interview*, wanachaguliwa vijana sita, wengine wanahangaika. Lakini Serikali kama imeandaa mpango maalum kama huu ambao Mbunge mwezetu amependekenza hapa, itakuwa hakuna haja ya kuita vijana kwenye *interview*. Wewe unaita vijana 200 au 600 wanarudi hawapati nafasi, sasa hii inakuwa lawama kwa taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu ambao umekuja na sisi Wabunge lazima tuangalie vizuri kabisa na mimi naunga mkono asilimia mia moja lazima na kwenye bajeti inayokuja tuijone, tuipangie bajeti ili kuwakomboa vijana wetu, ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza, nianze kwa kukubaliana na dhana za mapendekezo ya mtoa hoja Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, moja, kuhusu haja ya kuwa na mpango maalum wa masuala ya ajira kwa vijana na pili marekebisho ambayo yamewasilishwa na Mheshimiwa Ester Bulaya kuhusu maeneo mbalimbali ya kuboresha hoja ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa Kigwangalla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia na mimi niliwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya kuongeza maeneo ya

nyongeza manne ambayo naamini yana msingi sana na baadhi nitayarejea kidogo wakati wa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana sio tena bomu la wakati, ni bomu ambalo limeshaanza kulipuka kidogokidogo. Ukiangalia migogoro inayoendelea katika Taifa letu katikati ya vyanzo vyake, ukiondoa kukithiri kwa umaskini na hali ngumu ya maisha, ni pamoja na ongezeko kubwa sana la ukosefu wa ajira kwa vijana. Kwa hiyo, uamuzi wa kupitisha mpango, ni jambo la muhimu sana kwa mstakabali wa vijana nchi nzima. Lakini kupitisha mpango ni jambo moja, kutekeleza mpango ni jambo lingine na haya mambo mawili ni mambo tofauti kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii imewahikuwa na mpango wa ajira kwa vijana. Shirika la Kazi Duniani wakati ambapo dunia ilipoanza huu mfumo wa kuwa na mipango maalum ya ajira kwa vijana liliwahi kutoa fedha kwa nchi yetu na likatoa na mwongozo kwa nchi yetu kuandaa mpango kazi wa ajira kwa vijana na mpango huo ukaandaliwa mwaka 2007 ukiitwa *National Youth Employment Action Plan* ya mwaka 2007. Pendekeso langu mojawapo kati ya marekebisho ambayo nilitaka kuyafanya ni kwamba kabla hata ya kuingia kwenye utekelezaji wa mpango huu mpya, Serikali ilete taarifa Bungeni ya utekelezaji wa mpango ambao ultumia fedha za wahisani lakini miaka imepita lakini mpango ule haujatekelezwa ili tuweze kupata msingi wa kuweza kusonga mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi naunga mkono sana pendekeso la kuanzishwa kwa Benki ya Vijana. Pendekeso hili sio jipy, limekuwepo kwenye mipango ya toka mwaka

2007 niliyoizungumza. Mwaka 2011, katika Bunge hili hili Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Waziri Kivuli Mheshimiwa Joseph Mbilinyi alilisema pendekezo hili kwenye hotuba yake na mimi nilichangia na Waziri wa Masuala ya Vijana wakati huo akajibu hapa Bungeni akasema, Serikali inakubaliana na kuanzisha Benki ya Vijana na katika mwaka huu wa fedha utaratibu wa kuanzisha benki hiyo utaanza. Leo tunaona pendekezo la kupitisha Azimio la Bunge la kuanzisha benki badala ya Serikali kuja kutoa hapa taarifa Bungeni imefikia wapi katika mchakato wa kuanzisha benki. Naamini kwa sababu sasa inaenda kuwa Azimio la Bunge jambo hili litafanywa kwa vitendo na hayatakuwa maneno matupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya na jambo hili lisichukuliwe kiwepesiwepesi, tayari nchi yetu ina Benki ya Wanawake, *Tanzania Women Bank*, ni vizuri tukajiuliza ni kwa kiwango gani Benki ya Wanawake imeweza kuwakomboa wanawake Tanzania kutokana na ufinyu wa rasilimali ambao benki ile inapewa! Mimi binafsi wakati wa Siku ya Wanawake Duniani mwaka jana 2012 nilikwenda na vikundi vyatakinamama wa Jimbo la Ubungo kwenye Benki ya Wanawake ili waelimishwe na tukapata fursa ya kujua kinachojiri ndani ya benki ile. Tatizo kubwa la nchi yetu ni kutokutoa vipaumbele. Katika mwaka huu wa fedha peke yake pamoja na kwamba tulipitisha kwenye bajeti ya nchi kuipa benki ile pesa, miezi sita imepita ya kiutekelezaji mpaka sasa Benki ya Wanawake imepewa shilingi milioni 200/- peke yake kutoka Serikali Kuu kinyume kabisa na mipango. Sasa kama benki hii inapewa shilingi milioni 200/-, tujiulize kama kuanzishwa kwa Benki ya Vijana kutaenda sambamba na uamuzi wa kupeleka rasilimali za kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napendekeza, Bunge hili liliwahi kupitisha Mpango wa Kunusuru Uchumi wa Nchi mwaka 2008 na mwaka 2009 kikatengwa kiasi cha shilingi trilioni 1.7/- kwa ajili ya kunusuru uchumi wakati ule wa m dororo wa uchumi. Lakini kilichotokea baada ya hapo kwa mujibu wa Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kumetokea ujisadi kwenye matumizi ya fedha za mpango wa dharura kunusuru uchumi wa nchi. Taarifa ambayo Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwaka 2011, eneo moja tu ambalo hakuna vielelezo shilingi bilioni 48, yaani milioni 48,000/- zimekosa vielelezo kutokana na masuala ya ujisadi. Sasa utakumbuka kwamba nchi yetu ilikwishawahi kukumbwa na kashfa ya *EPA* na sehemu ya hizo fedha zilizorudishwa nyingine nyingi bado hazijarudishwa, shilingi bilioni 40 baada ya madai ya kupambana na ujisadi zilielekezwa kwenye Benki ya Rasilimali, shilingi bilioni 40 za Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tukawa na Azimio vilevile, nchi hii ikaamua kuchukua hatua za haraka za kufuatilia fedha zilizotolewa za m dororo wa uchumi, hizi shilingi bilioni 48 na tukaamua kuzichukua hizi shilingi bilioni 48/- zikirejeshwa kuzipeleka kwenye Benki ya Vijana ili tukawa na mtaji wa kutosha tofauti na hali ya sasa ambapo tuna Benki ya Wanawake lakini haifiki wanawake wengi kutokana na matatizo ya mtaji. Nazungumza kwa uzito huu kwa sababu tatizo hili pamoja na kuwa ni tatizo la nchi nzima, Dar es Salaam kwa mujibu wa takwimu na Mheshimiwa Waziri ametoa takwimu hapa za ukosefu wa ajira ambazo zinataka kuonyesha kama tatizo hili ni dogo, asilimia 11.7 na kadhalika jambo ambalo ni vizuri Waziri

atakapohitimisha hoja, kwanza atoe takwimu ambazo ni za karibuni maana hizi ni takwimu za mwaka 2006 lakini pili atoe maelezo ya ziada maana tatizo linatofautiana. Dar es Salaam ukienda Ubungo, ukienda Kawe, ukienda Kinondoni, ukienda Temeke, ukienda Kigamboni hali ya ukosefu wa ajira kwa vijana imefikia asilimia 30 ambapo ni tatizo kwelikweli na ni bomu la wakati limeshaanza kulipuka, inahitaji hatua za haraka. Kwa hiyo, ni vizuri tukapewa takwimu sahihi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aya inayofuata Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hizi hoja zote hazitofautiani na juhudzi za Serikali kuanzia 2005 mpaka 2015. Ni vizuri wakati Waziri anahitimisha hoja yake akatueleza kuhusu juhudzi hizi za Serikali. Kwa sababu Serikali iliahidi mwaka 2005 kwamba kila mwaka kutatolewa ajira milioni moja kwa vijana na ahadi hii ni ya Mheshimiwa Rais. Ni vizuri tukaeleza Bungeni ajira milioni moja toka mwaka 2005 zimetengenezwa kwa kiwango gani mpaka sasa ili tuone haya maazimio yatakayopitishwa leo kweli yatatekelezwa? Kwanza Dar es Salaam maana hapa pendekero ni kwamba Halmashauri ndiyo ziandae maeneo, kuna utofauti sana. Mazingira ya kupata maeneo Dar es Salaam kwa sababu ya matatizo ya mipango miji ni gharama kubwa sana. Wakati wa kampeni za uchaguzi za mwaka 2010, Serikali ya CCM iliahidi kujenga *Machinga Complex* kwenye kila Jimbo la Dar es Salaam kwa maana ya Kawe, Kinondoni, Ubungo na kwingineko. Nitaomba ufanuzi vilevile wa Serikali, kwa kuwa sasa kazi hii inakwenda kupelekwa kwenye Halmashauri ya kutenga maeneo, kuna tatizo kubwa la Wamachinga Dar es Salaam, ni lini sasa itatekeleza ahadi ya kujenga *Machinga Complex* ili wale vijana wanaohangaika pale Ubungo na

maeneo mengine ya Dar es Salaam wapate vilevile mazingira bora ya kufanyia kazi kwenye maeneo yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekazo la Mheshimiwa Ester Bulaya, ukurasa wa pili, limezungumza kuhusu kuanzisha maeneo yanayoitwa *Special Youth Economic Zones*; na mimi nakubaliana kabisa na pendekazo hili na mtakumbuka wakati wa mjadala wa *SEZ* kwa maana ya *Special Economic Zone* pamoja na *Exclusive Production Zone, (EPZ)* na (*SEZ*), nilipendekaza wakati ule kwamba kwenye maeneo haya maalum kutengwe maeneo kwa ajili ya wazalishaji wadogo na wafanyabiashara wadogo ili kupanua ajira. Kwa sababu pendekazo hili hatimaye linaelekea sasa kupita, ningependa kupata ufanuzi vilevile kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza swali hapa Bungeni, Dar es Salaam ina matatizo ya viwanda vingi vilivyobinafsishwa vimekufa. Ukienda Kawe, kuna *Tanganyika Packers*, ukienda Ubungo kuna viwanda vingi kwelikweli na nikapendekaza wakati ule kwamba kwa kuwa waliobinafsishiwa viwanda hivi wameshindwa kuviendeleza na hatimaye wamechangia tatizo la ukosefu wa ajira Dar es Salaam, nikapendekaza hapa Bungeni kwamba ile mikataba ibatilishwe ili maeneo haya ya viwanda yarudishwe. Wakati ule nikapendekaza kwamba eneo mojawapo litengwe kwa ajili ya eneo maalum la wenye viwanda vidogovidogo kwa ajili ya vijana ili kupanua ajira. Naomba kupata kauli kutoka kwa Waziri wa Viwanda na Biashara na Waziri wa Kazi katika kuhitimisha hoja kwa sababu jibu la Serikali lililotolewa ilisema inakubaliana na ushauri huo, inapeleka waraka kwenye Baraza la Mawaziri

na hii ilikuwa mwaka 2011 mapema sana kwa ajili ya mapitio ya hivyo viwanda. Kwa sababu muda umeshapita na hali ya viwanda inaendelea kuwa mbovu, vijana Dar es Salaam wanaendelea kukosa ajira, ningeomba kupata kauli ya Serikali. Kwa wazo hili je, Baraza la Mawaziri limekwishakaa? Je, Baraza la Mawaziri limekwishapitisha ili tuweze kuchukua hatua za mapema zaidi za kuweza kuhakikisha kuwa vijana wanapata ajira? Nilisema kuwa tatizo letu siyo mipango kwa sababu pamoja na mipango unaweza kusema mtu anaweza kupuuza utekelezaji wa mipango kwa sababu ni mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ina Sheria, Sheria mbili muhimu sana, leo tunatengeneza mpango lakini tayari mwaka 1999, Bunge hili Tukufu lilipitisha Sheria ya Huduma za Kuongeza Ajira, kwa maana ya *Employment Promotion Services Act*. Ile Sheria ukiisoma imeelekeza kipengele kwa kipengele namna mikakati kama hii inavyopaswa kutekelezwa. Ndiyo maana kwenye mapendekezo yangu nimependekeza vilevile Serikali ilete taarifa toka mwaka 1999 kwa vifungu vile vya Sheria ambavyo vinaelekeza kwenye kila Halmashauri kuundwe Kamati za Kuongeza Ajira, za kuibua miradi ya ajira na kadhalika, Sheria hii imetekelizwa kwa kiwango gani kwa ajili ya kuwanusuru vijana na tatizo hili kubwa la ukosefu wa ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ina Sheria nyingine, Sheria ya mwaka 2004, inaitwa *Economic Empowerment Act*, Sheria ya Uwezeshaji wa Kiuchumi. Haya mawazo yaliyoko kwenye pendelekezo la Azimio namba moja, pendelekezo la Azimio namba mbili, pendelekezo la Azimio namba tatu, pendelekezo la Azimio namba nne kuhusu *value*

*chain* yaani mnyororo mzima ule wa ongezeko la thamani kwenye miradi, kuwawezesha vijana kwenye mafunzo ya ujasiliamali, mambo yote haya tayari yako ndani ya Sheria. Kinachotakiwa ni kupata taarifa hapa Bungeni ili tujadili vizuri na tutimize matakwa ya Kikatiba ya kuisimamia Serikali. Ni kwa kiwango gani Serikali toka Sheria hizi zipite utekelezaji umefanyika? Kwa hiyo, mimi ninasisitiza kwamba Maazimio haya yawepo pamoja na mapendekezo ya marekebisho niliyoyawasilisha kwa Katibu tangu asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ili tukitoka hapa hili bomu la wakati hili ambalo limekwishaanza kulipuka kidogokidogo tuweze kuchukua hatua za haraka, tuanzie tulikotoka, tusianze safari mpya kwenda mbele wakati ambako kuna misingi iliyowekwa. Tatizo ni dhamira ya utekelezaji, kuondoa udhaifu uliokuwepo huko nyuma ili tuweze kusonga mbele kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano huu wa Bunge la mwezi wa Februari kwa mujibu wa Kanuni ya 94 ya Bunge lako Tukufu, ndiyo mkutano unapaswa kutengeneza mpango wa mwaka wa Serikali. Ni vizuri Wabunge wote kwa sababu jambo hili halina vyama, halina itikadi na halina mahali, kila mahali kuna vijana ambao wanahitaji ajira, Bunge lako Tukufu lijadili kwa kina Maazimio yote yatakayopitishwa siku ya leo yasibaki kuwa Maazimio peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maazimio haya yatengewe fedha za kutosha ili mwaka ujao tukiiingia kwenye bajeti na baada ya bajeti kuwe na tija tofauti na maeneo yaliyopita. Ninasema haya kwa nia njema sana kuwa jambo hili la

ukosefu wa ajira kwa vijana haliwezi kujibiwa kwa maneno ya Waziri tu kusema kuwa juhudini zimefanyika kutekeleza llani kama hakuna matendo na rasilimali za kutosha. Ninashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mnyika, ninakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nifafanue kuwa ninao wachangiaji kama thelathini ambao siyo rahisi kumalizika kwa jioni ya leo na katika wachangiaji hao hakuna wa kutoka Chama cha *TLP*, hakuna wa kutoka *UDP*, hakuna hata mmoja kutoka *CUF* aliyeomba, kuna mmoja tu wa *NCCR* ndiye aliyeomba karibu wote ni...

**WABUNGE FULANI:** *CUF* yupo!

**NAIBU SPIKA:** Oh! Kama *CUF* wameomba, nitamwona. Oh, yuko mmoja ameomba lakini ameleta sasa hivi. Baada ya hapo, nimwite mchangiaji kutoka *NCCR*, Mheshimiwa David Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimshukuru Mama yangu Mama Malecela kwa kuniachia nafasi yake ili niweze kuchangia.

**NAIBU SPIKA:** Atafuata Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Kafulila endelea.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ambayo kimsingi inahusu agenda kwa vijana kwa maana

ya ajira, kwa sababu unapozungumza tatizo la ajira duniani kote, kwa sehemu kubwa wahanga wa kwanza wa ajira hizo ni vijana. Ninashukuru kwamba sasa tunaweza tukaanza kuweka mipango japo tumechelewa sana. Ukikaa humu, ukasikiliza michango, utadhani uhuru tumepata mwaka jana, sasa tuko kwenye mwezi wa kwanza wa mwaka mpya tunaanza kupanga mipango, ni mambo ya aibu. Uhuru tumepata leo ni miaka 52. Nimewahi kuzungumza hapa Bungeni nikimwuliza Waziri wa Vijana, hivi mpaka sasa kuna vijana wangapi hawana ajira? Akanijibu hapa kuwa taarifa za uhakika hazijapatikana, unaweza kuona ni kwa namna gani ambavyo tuna Mawaziri, tuna Watendaji ambao wanalipwa mishahara na posho kwa kodi za wananchi lakini ufanisi wa kazi uko chini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango yote ambayo tumeizungumza hapa, ukweli ni kwamba ukisoma Mpango wa Miaka Mitano, haya tunayozungumza yamo. Ukisoma llani za Vyama vyote, haya mambo yapo. Ukisoma mikakati mbalimbali ya Wizara mbalimbali, haya mambo yapo lakini tuna ugonjwa sugu wa nani tumtume kusimamia haya mambo. Mfumo umeoza kuanzia juu mpaka kwenye kitongoji, watu hawajibiki na ufanisi uko chini sana. Leo hii tunazungumza hapa ndugu zangu kiasi cha vijana ambao wanaingia kwenye soko la ajira kila mwaka ni kati ya laki nane na milioni moja, wanaingia katika soko la ajira kila mwaka. Ukiangalia ni mkakati gani ambao upo kwa ajili ya kufyonza hayo mahitaji ya ajira na nani ambaye anasimamia, hatuoni! Leo tunazungumza na leo tunakubaliana kuwa kuna umuhimu wa kuanzisha mfuko kwa ajili ya mikopo kwa wanaohitaji mikopo hususani vijana,

ninakubaliana. Lakini tatizo ni zaidi ya mkopo, ni zaidi ya hela, tatizo la ajira ni mfumo mzima, namna gani ambavyo unaweza kutengenezwa kuwafanya hawa watu kweli waajirike lakini pia wakajiriwa waweze ku- *perform*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunazungumza kwenye sekta ya elimu, tunazungumza mabadiliko ya Mitaala, mabadiliko ya Muhtasari sijui, ndugu zangu kuna vitu ambavyo ni lazima tufikirie upya. Mwaka 1967 wakati wa utawala wa Mwalimu Nyerere, yeye alikuja na *Philosophy* ya *Education, Education for self reliance* kwamba ni elimu kwa ajili ya watu wajitegemee. Tukipita katikati tunabadilisha, tunafuta, tunabadilisha, tunafuta, tukaingia machakani kabisa baadaye watu wa Ulaya, Benki ya Dunia na Wahisani wetu wanakuja wana-introduce ujasiriamali kwamba jamani mnapaswa kufundisha ujasiriamali kuanzia shule ya msingi mpaka chuo kikuu kwa sababu bila elimu ya ujasiriamali watu hawawezi kujitegemea, sasa mlifuta nini mnarudi wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo haya ya ujasiriamali ambayo leo mmepewa na watu wa Ulaya yalikuwepo wakati wa Mzee Kawawa, Mzee Nyerere lakini kwa sababu ya ku-copy na ku-paste mipango ya Ulaya, matokeo yake mnakwenda machakani halafu baadaye wanarudi. Sasa miaka 50 mliyopoteza mnapiga safari ya kilomita nyingi kwenda porini kwa kupotea halafu baadaye unaambiwa hapana siyo huko rudi kulekule uanze mwanzo, halafu uanze kilomita ya kwanza kwenda kwenye mwelekeo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo sura ambayo tunaiona katika Taifa, tunahitaji kama Taifa kuzalisha vijana ambao wanaweza kuajirika. Miaka ya nyuma kulikuwa na vyuo vya kati vinatoa *diploma*, vinatoa vyeti vya kati na tukazalisha vijana wengi katikati ambao walikuwa na taaluma zao kiasi kwamba wanaweza kuzalisha katika nchi. Hapa karibuni tukaingia kwenye dhana nyingine tena kwamba pengine elimu ni mpaka mtu afike chuo kikuu, mmezalisha vyuo vikuu vingi vya kutosha mkasahau vyuo vya kati, matokeo yake tunakosa *labour force* ambayo inaweza ku-*drive* uchumi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kuwa mtu mwenye *degree* atakwenda kufanya kazi ya kupanga tofali na Mataifa yote ukisoma historia ya Singapore, soma historia ya Malaysia, ukisoma China wote walifanikiwa kwa kuanza kuwekeza kwenye elimu ya ufundi, teknolojia na sayansi, haya ndiyo maeneo ambayo tunapaswa kujielekeza. Kwa kuwekeza pale wakazalisha vijana wengi ambao wana uwezo wa kufanya kazi lakini kwa sababu tunaua kimoja baada ya kingine, tumeshaua elimu, tumeua maeneo mengine na ajira *is obvious* kuwa ukiua elimu huwezi kutengeneza maeneo mengine, haiwezekani, ukishaua elimu *is obvious* kuwa viwanda vitakufa na kilimo kitakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilikuwa Quebec Canada kwenye mjadala wa namna gani tatizo la ajira Duniani linaweza kupatiwa majibu. Mbunge mmoja wa Denmark akani- *challenge* akasema kuwa David huwezi kuzungumza ukosefu wa ajira kwenye nchi yako wakati kwenye nchi yako mna takribani hekta milioni ishirini na tisa na laki nne ambazo zinafaa kwa *irrigation*, achilia mbali

maeneo ambayo yanafaa kwa kilimo cha kawaida. Anasema kuwa kule kwao ukisema *unemployment* maana yake ni fursa zimejaa, sasa watu wamebaki nje. Nchi hii ina fursa za kutosha, tatizo ni nani atuongoze kuzitumia, tuna mito kumi na moja nani anatuelekeza tuitumie tuweze kuzalisha ajira kupitia mito hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna ardhi kubwa lakini ni kwa namna gani ardhi hiyo, ni nani anatuelekeza tuweze kuitumia ardhi hiyo iweze kuzalisha ajira? Ni aibu kwenye Taifa lenye neema kama hili kulia ajira, ni aibu! Lazima ifike mahali kwa kuwa mipango ipo, kwa kuwa sera zipo, nilikuwa ninawaambia kuwa Chama Tawala kwa kweli siyo maskini wa mipango, mnyonge mnyongeni, kwa mipango mnayo mingi sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni nani atekeleze? Nani atekeleze, hapo ndipo tunapopigiana kelele hapa, hakuna mtekelezaji hapa, watu wamechoka, watu hawana uwezo, ni Mawaziri wachache unaona kapewa Wizara na unaona inatoa matokeo, *very few* wengi ni mazoea tu. Tunahitaji mtu akipewa Wizara tuone kabisa kuwa kuna utofauti, ndani ya muda mfupi tuanze kuona tofauti, hii mambo ya kupewa Wizara na kuanza kufanya mambo ya kimazoea mwisho wake ni maswali kila siku lundo hakuna majibu au majibu ni yaleyale. Tunahitaji watu ambao wanaweza waka-*perform* na kama amechoka basi apishe watu wengine waingie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezakana usiujue umaskini kama uko kwenye AC, unakula vizuri, inawezekana usijue adha na karaha ya umaskini. Umaskini ni aibu,

unashusha heshima, unaweza kuwafanya watu watembee na mabakuli kuomba wakati wana miguu na mikono, unawadhalilisha kwa sababu ya mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii benki tutakubaliana kuwa ianzishwe lakini pamoja na kuanzishwa hiyo benki ni lazima tuone kuwa suala la ajira ni suala pana, tuwe na mkakati mpana wa kuweza kufanya watu hawa wawe na uwezo wa kuajirika. Hiyo benki kama benki ni lazima tuangalie ni kwa namna gani tuta *i-manage* iweze kutoa matokeo ambayo tunadhani ni matokeo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulikubaliana kuwa benki ya kilimo itaanzishwa. Benki ya kilimo mpaka leo haijaanzishwa. Tulikubaliana kuwa *TIB* wafungue dawati la mikopo kwa kilimo lakini *complication* ambazo ziko pale ili huyu mtu apate huu mkopo, ni afadhali kuacha. Hawa Watanzania siyo wavivu, hawa Watanzania wanahitaji kuwezeshwa tu na kupewa mwongozo lakini wana uwezo wa kufanya kazi. Jambo la msingi tunahitaji Serikali iwajibike, tutazunguka mambo yote mipango, mipango, mipango lakini kama Mawaziri wenyewe ni *design* hii, kama kikosi ni *design* hii, mtatafuta mchawi mwingine tu lakini kuna tatizo kubwa sana kwenye watendaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika Halmashauri ziko hoi halafu tunasema Halmashauri uelekeze huko, hivi mnajua Halmashauri zetu zilivyo? Halmashauri ziko taabani, majukumu yake ya kawaida mpaka sasa haiyawezi uongeze mizigo mingine tena. Hivi vitu tufike mahali tukubaliane kwamba kama tunaanzisha kitu basi tutafute mfumo ambao ni mfumo utakaojitegemea. Ni lazima

tutafute, tutafungua benki lakini iwe ni benki ambayo inaweza kusimama yenyewe kimfumo mwanzo mpaka mwisho. Ardhi tunayo na wataalamu wanasema ardhi tunaweza kuitumia pengine kama *collateral* lakini ukiuliza leo kwamba ardhi ni kiasi gani imepimwa mpaka sasa ni chini ya 10% ya ardhi yote iliyopimwa, miaka 50 ya uhuru mmepima asilimia 10% kupima tu acha kutumia, kupima tu na hiyo imepimwa *generally* lakini kwa maana ya ardhi kabisa watu wenyе hati ni 6% tu, 94% ya watu wana nyumba na hazina hati. Wanasema kuna mkopo kigezo ni hati ingekuwa ni utaratibu rahisi sana lakini hiyo hati anaipataje, kama *ku-process* mtu kupata hati tu mtu anaweza kuchukua mwaka mzima mpaka miaka miwili, akaamua kuchoka, nauli zimeisha, akaamua kurudi kijijini. Mimi niseme kuwa miongoni mwa vigezo ambavyo baadaye tusije kuvitumia kama njia ya kupata mkopo, ni pamoja na kuwasukuma watu kuwa wakiwa na hati watapata mikopo, kuna complications nyingi sana kwenye upatikanaji wa hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu mnaziweka hapa zinaonekana nyepesi lakini unapokwenda kwenye utekelezaji wa hizo taratibu, mna watu wa ajabu sana kwenye kusimamia taratibu hizi. Ni bahati mbaya sana ni kazi ngumu kumfukuza mfanyakazi Serikalini. Kama kuna kazi ngumu ya kufanya katika nchi hii ni kumfukuza mfanyakazi wa Serikali, kuna shida kweli. Watu wanaharibu lakini *complications* za kuwafukuza ni nyingi mno. Mnapaswa kupunguza urasimu ama sivyo tutabaki hapa tunalea watendaji ambao hawana uwezo, wanaumiza Taifa hili, wanatumiza vijana na mwisho wa siku yatakuja kutokea ambayo kimsingi nisingependa tuyaone yakinoteka.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana unaweza kuzungumza machafuko leo kwa urahisi kwa sababu hujayaona lakini ukishuhudia maeneo ambayo kuna machafuko, mmetoka Mtwara, watu wa Mtwara wanajua ni namna gani machafuko ya Mtwara yalikuwa mabaya. Sasa unaweza ku-*imagine* kuwa hivi nchi nzima ingekuwa kama Mtwara, leo hata Bungeni tusingekaa hapa maana tungekaa hapa vijana wa Dodoma hapa wangezunguka jengo hili asingekaa mtu hapa. Tunakaa hapa kwa ustaarabu kwa sababu kuna watu wamevumilia shida lakini uvumilivu una mwisho, kuna wakati watu watachoka na wataamua kuchukua hatua zingine. Kabla hawajachoka, ni lazima tukubaliane kuwa tuna-rescue hii *situation* kabla haijawa worse.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali katika mpango mpana, mpango mkubwa tujitahidi ikiwezekana vyuo vya kutoa taaluma visambazwe nchi nzima, watu wafundishwe ufundi, watu wafundishwe sayansi. Tutatengeneza vijana ambao wanaweza kuajiriwa kwa urahisi badala ya kusema kuwa mnasubiria mikopo.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ninakushukuru sana. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela atafuatiwa na Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia lakini pia

ni vigumu sana kuchangia baada ya Mheshimiwa Kafulila kumaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla, kwa kutuletea hoja na ameleta hoja hii wakati muafaka kabisa. Ninaomba niseme kuwa hoja hii ni hoja ya muhimu sana, ninaomba Serikali ichukue hii hoja kwa uzito wake lakini hata na sisi Wabunge tunapochangia tusitoke sana nje ya mstari tusimame kwenye hoja hii aliyoileta Dkt. Kigwangalla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, Jimbo la Vijana, kwa marekebisho yake aliyoyleta ambayo yameongeza ladha ya hoja ya Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nzega. Lakini mtu wa tatu wa kumpongeza ni Waziri kwa jinsi ambavyo amekuwa mstaarabu, akawa *flexible*, hakuendelea kung'ang'ania yale mabadiliko aliyoyleta mwanzoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongea tatizo la ajira kwa vijana, tukiwa wawakilishi wa wananchi, tukiwa tumechaguliwa na wananchi, twende tuangalie nchi kwanza. Tatizo la ajira kwa vijana si tatizo la nchi yetu tu, ni tatizo la ulimwengu mzima, lakini ni vema ikafahamika kwamba kila Serikali inajitahidi kutafuta njia muafaka ya kuondoa tatizo hili. Naomba nirudie kwamba ni tatizo la ulimwengu mzima lakini kila Serikali inajitahidi kutafuta ni mpango upi utatatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba leo nizungumze kwa kutoa mfano, nitoe hotuba yangu kwa kutoa mfano. Tarehe 5 Novemba, 2012, saa tisa asubuhi. Ilikuwa siku ya Jumatatu nilikuwa nasafiri kutoka Dubai kwenda London Heathrow na ndege ya Emirates, nikabahatika kukakaa kiti Na.1A.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumza na Serikali nikitoa mfano huu, baada ya kuingia kwenye ile ndege tu, mimi nimefanya kazi kwenye *Airline* miaka 14, kwa hiyo, nafahamu taratibu za *Airlines* vizuri. Ukiingia kwenye ndege yule anayeku-serve mwangalie kwanza jina lake ni nani ili umwite kwa jina. Yule msichana aliyekuja kunipokea tangu nilipoingia akanipeleka kwenye kiti changu Na.1A, niliona jina lake limeandikwa Felister. Nilipoona jina nikawa na wasiwasi huyu msichana atakuwa ni Mtanzania lakini nikanyamaza nikakaa kwenye kiti changu.

Mheshimiwa Naibu Spika, akajaakanisalimia vizuri, *accent* yake haikunionesha kwamba ni mtu wa Kenya wala ni wa wapi, *accent* ya Kiingereza ilikuwa ni nzuri sana. Akaniambia Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, akaniita kwa jina, mimi nitakuhudumia kutoka hapa mpaka London. Kwa sababu nimefanya kazi kwenye *Airline* nikamwuuliza masaa yako mawili unayopumzika ni saa ngapi? Akaniambia, nikamwambia naomba muda wote uje kukaa na mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikutaka acae na mimi ili nimwangalie, kuna kitu nilitaka kujifunza. Yule msichana kila dakika alikuwa na mimi nikaanza kujifunza na sasa naiambia Serikali. Nikamwuuliza Felister unatoka nchi gani?

Akaniambia natoka Tanzania. Nikamwuuliza *which part of Tanzania?* Akaniambia ni Arusha na mimi nilimwangalia nikajua yule msichana anatoka sehemu za Arusha, Mbulu au kitu kama hicho kulingana na alivyokuwa na umbile lake. Nikamwuuliza uliipataje kazi hii? Kwa sababu yupo *first class* na ana-serve mtu aliyekaa kiti Na.1A. Akaniambia nimeipata kwenye *internet*. Nikamwuuliza Watanzania mpo wangapi? Akaenda, akaleta *documents* zote akaniambia tupo tisa kwenye Emirates.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamwuuliza Emirates ina *Cabin Crew* wangapi? Akaniambia wapo elfu kumi na tano. Ndiyo! Ni *flight* kubwa! Niliandika kila kitu kwenye *notebook* yangu. Nikamwuuliza Wakenya wapo wangapi na Serikali naomba mnisikilize vizuri, mimi nilikuwa nafanya kazi kama Mbunge, natafuta *comparison*, akaniambia Wakenya walikuwa mia tano lakini sasa hivi baada ya kwenda kufanyiwa *interview* wapo mia nane. Nikamwuuliza wanapataje hizi nafasi? Akaniambia Serikali yao ina-*intervene*, Serikali yao inaingilia!

Mheshimiwa Naibu Spika, akaniletea na zile *document* akaniambia Mheshimiwa, ananifahamu si ni Mtanzania na ananiona kwenye Bunge, akaniambia zikitoka tu zile *employment* leo, Balozi anaondoka anakwenda kwao ndiyo maana wenzetu wapo mpaka mia nane sisi tupo tisa. Hiyo ni moja ambayo ipo ndani ya ndege, hiyo ni moja ambayo nimeiona ndani ya *Emirates* kwa wale ambao mnakwenda Dubai na Abudhabi, angalieni kwenye *five stars hotel* nani wapo kule, ni Wakenya! Lakini nendeni Zanzibar!

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa kuwa *aggressive*, kwa nini Wakenya ni mia nane, kwa nini Watanzania ni tisa? Tujiulize wenyewe jamani? Tupo hapa kwa ajili ya nchi yetu, hatukuingia hapa ndani kutembea hapa, tupo hapa kufanya kazi, kwa nini Watanzania ni tisa, kwa nini Wakenya wamefika *up to mia nane!* Ni Serikali yao. Serikali mnapaswa muwe *aggressive enough!* Ni lazima tuambizane ukweli, kwani wao wamepataje, wao wana nini cha zaidi, Felister nilimwona alivyokuwa, ni msichana wa Arusha alikuwa ana mwonekano mzuri, anaongea vizuri, ana elimu nzuri, wasichana wa Tanznaia wengi ni wasomi, wana mwonekano mzuri, wanaongea Kiingereza kizuri, tena hawana *accent*, lakini kwa nini hawaingii kwenye hizi kazi za Kimataifa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimependa kupanua wigo, niende mpaka nje ya Tanzania...

## TAARIFA

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninasimama kumpatia taarifa Mama yangu Anne Kilango Malecela kwamba, Kenya wamefikia hapo walipo kwa sababu walishakiondoa Chama Tawala nchini mwao. (*Kicheko*)

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa naifuta na siitaki kuisikia. Mimi kama Mbunge napaswa kuishauri Serikali, ndiyo kazi yangu. Nimeifuta hiyo taarifa wala sikuipokea. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hata kama mtu humpendi anapofanya jambo jema chukua mfano kwake. Mimi nimeona wivu kwa nini Wakenya 800, kwa nini Watanzania 9? Naiomba Serikali yangu ijiulize, naomba mchukue hili suala *in a very serious note*. Serikali naomba muwe aggressive haraka sana. Mwendo sasa hivi siyo huu wa kawaida, jamani ulimwengu unakwenda haraka, ni lazima uwe na wivu wa maendeleo!

*(Hapa Wabunge fulani walikuwa wakiongea)*

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Hebu nyamazeni huko na nyie! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutabaki tunalalamika lakini tunapaswa tufanyekazi kwa bidii sana. Vijana Watanzania narudia tena ni wasomi, wana uwezo lakini wanahitaji msaada. Huu mpango uliopita hapa leo, hoja aliyotuletea Mbunge wa Nzega, tunaomba Serikali mjue kwamba tutasimamia, hakuna kusema kama wanavyosema, aah, ni mpango wa makaratasi hakuna kitakachoteklezwa! Sisi Wabunge tupo wapi? Tutasimamia na tutahakikisha huu mpango unatekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge ni kazi yetu kusimamia na ninaiomba Serikali ijue kwamba katika hili la ajira kwa vijana tutasimamia na tutafanya kazi yetu na nyie fanyeni kazi yenu. Ninyi mkifanya kazi yenu na sisi tutafanya kazi yetu, tutawasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie tena, niseme naiomba Serikali sasa ijue mwendo wa ulimwengu wa sasa ni kwenda kwa haraka, kuiga yaliyo mazuri na kufanya kazi kwa bidii, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa mchango wako mzuri sana, Mheshimiwa Rukia Ahmed.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu jana nilikuwa nikisikiliza vizuri michango ya Wabunge wengi hapa, ilikuwa ni hoja ya kuanzisha mifuko, lakini mimi nashangaa tunataka kuanzisha mifuko, sikatai hoja waliyoleta watoa hoja kutaka kuanzisha mifuko lakini pia siwezi nikaunga mkono kwa sababu kila siku tunataka kuanzisha mifuko, mifuko hii pesa hizi tutapata wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mifuko mingi hapa imeanzishwa, kuna mifuko ya *UCAF*, kuna mifuko ya pensheni, kuna mifuko ya barabara na mifuko mingine mingi, lakini sasa mbona mifuko hii nahisi kama inavuja? Tatizo la nchi hii siyo kuanzisha mifuko, tatizo la nchi ni ajira, vijana hawana ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzisha mifuko tu bado tutakuwa hatujawasaidia vijana waliokosa ajira. Uchumi wa nchi kila siku zinavyokwenda unazidi kudidimia.

Hebu tujipangeni vizuri jamani namna ya kutumia rasilimali zetu ili vijana wetu waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanatoka kila pembe ya nchi hii, wanatoka Pemba, wanatoka Kigoma, wanatoka Newala, wanatoka Mtwara, wanatoka Lindi wanatoka Mbeya, wote wanakimbilia Dar es Salaam kwa sababu maendeleo yote yapo Dar es Salaam. Viwanda viro pale, kila kitu kipo pale, kama ingekuwa tunajipanga vizuri, tukajenga viwanda katika sehemu za Mikoa yetu, tukajenga Mbeya kiwanda cha kusindika matunda, kule kuna mazao mengi, tukajenga Morogoro kiwanda cha kusindika mazao, pale pana mazao mengi sana, tukajenga Mtwara, tukajenga Lindi, tukajenga Pemba, tukajenga kila mahali, hivi vijana wangekuja Dar es Salaam kutafuta ajira? Wasingekuja hata siku moja kwa sababu nia ya vijana hawa ni kupata ajira lakini mimi nashangaa sisi tunataka tuanzishe mifuko, mifuko hii mpaka lini na tutakuwa na mifuko mingapi? Kwanza pesa za kuanzisha mifuko hii tutazipata wapi ikiwa bajeti ya Serikali haikamiliki. Tunapitisha bajeti hapa ni mali kauli tu, hatuna pesa! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii twendeni katika Wizara, sote hapa Wabunge tuna Kamati, tunakwenda na tunaona. Katika hizi Wizara tukizungumza na Watendaji unaambiwa pengine bajeti tumeipitisha mpaka inafika bajeti ya mwaka mwingine hata asilimia 30 ya pesa hawajapewa katika Wizara, lakini bado tunang'ang'ania tuanzishe mifuko, mifuko gani hii jamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tujipange vizuri, tutumie rasilimali zetu, vijana wetu wapate ajira. Vijana jamani wanachanganyikiwa, vijana wanafika mahali wanatumia madawa ya kulevyo, vijana wanafanya mambo ya ajabu ajabu, vijana wanakuwa wezi, kwa sababu hawana ajira, wafanye kazi gani, wanakaa vijiweni halafu wanafanya mambo ya ajabu ajabu!

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge tuna jukumu la kuhakikisha vijana wetu wanapata ajira, lakini siyo tung'ang'anie mifuko. Huu mfuko tukiuanzisha hebu tuseme watapata ajira vijana wangapi kwa mfuko huu? Mara tunafungua Benki ya Wanawake, kesho tutasema tunafungua benki ya wakongwe, kesho kutwa benki ya wajane, mpaka lini? Pesa zenyewe hatuna halafu tunadai tunaanzisha mifuko, jamani mifuko ina tundu inavuja! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuachenii kukaa hapa tukajadili mifuko tu, tutafute ni namna gani tutatumia rasilimali zetu, vijana wetu wapate ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, hapa Mheshimiwa Mnyaa aliwasilisha hoja akasema kuna wafanyakazi wa kigeni katika mahoteli ambao siyo raia wa nchi hii wameajiriwa, sasa nafasi zile ingekuwa tunazifanyia kazi, aliwasilisha hoteli moja tu ina wafanyakazi 29 ambao ni wa kigeni. Sasa hebu tuangalieni ikiwa hoteli moja ina wafanyakazi wa kigeni 29, nchi hii ina hoteli ngapi? Je, nafasi hizi tungezifuatilia wakapewa Watanzania vijana wetu wasingepata ajira? Lakini tunaacha namna ya kuwatafutia vijana ajira, tunakuja hapa Bungeni tunaanza

kuhimiza mifuko tu, jamani tuachaneni na mifuko! Tujipange vizuri, tuendeleze rasilimali zetu, tuzitumie ili vijana wapate ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii mifuko kwa kiasi fulani inanufaisha upande mmoja tu wa Jamhuri hii ya Muungano. Je, ule upande mwengine vijana wao wapate ajira gani au kutakuwa na mfuko gani kule? Kwa sababu hawa watoa hoja hawakumaanisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ni muungano wa Tanzania ambayo inajumuisha Zanzibar pamoja na Bara. Sasa, je, huu mfuko watoa hoja hawakutuambia ni kwa ajili ya Bara tu, wale kule wengine wavute bangi, wawe hawana kazi au watumaanishie mfuko huu ni kwa ajili ya Watanzania wote?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siungi mkono hoja hii ya kuanzisha mfuko. Nasema tujipangeni tuwatafutie vijana ajira na kwanza tuanze na kupitia mahoteli yote, tuangalie vijana waliopo kule wanastahili wageni wale kupewa ajira zile? Tuwatafutie watu wetu ajira tusikae hapa tuki-deal na mifuko kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Rukia kwa mchango wako. Sasa nitamwita Waziri Kivuli, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa pia *Happy New Year*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza, naomba niunge alipoishia Mheshimiwa Rukia kuhusiana na suala la mifuko. Naunga mkono mikakati yoyote ile ya kuendeleza masuala ya ajira kwa vijana wa Tanzania na niko mstari wa mbele, lakini kwenye suala la mifuko hata mimi kidogo nina-*doubt* kwa sababu mifuko imekuwa mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ripoti ya Waziri hapa kuna Mfuko wa Dhamana, kuna Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji, kuna Mfuko wa Wajasiriamali Wadogo, mimi nafikiri tungekuja na hoja ya kupunguza mifuko ili tuwe na mfuko mmoja wenyewe nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Rukia na zaidi niseme tu kwamba nakubaliana na suala la uanzishwaji wa Benki ya Vijana ambayo itakuwa na maslahi kwa vijana wote. Lakini hii mifuko itakuja kuwa na Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Ma-VX, Makatibu, sijui *Chief Accountant*, kitu ambacho kinazidi kutawanya rasilimali ndogo ambayo ingekusanywa kwa pamoja vizuri ingeweza kwenda kutimiza malengo kama vile inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la jira kwa kweli ndugu zangu tunatakiwa watu tuwe *serious* zaidi. Kila mtu alisema alikosafiri, Mheshimiwa Kafulila alienda Canada, mimi mwaka jana pia nilisafiri na Waziri nilienda Geneva kwenye Mkutano wa *ILO* kuhusu masuala ya kazi, nikakutana na jamaa kutoka Indonesia ambao wao kwa ajili ya mkakati wa kazi tu kwa vijana walitenga miaka kumi, ambapo sisi mpango wa maendeleo kwa ujumla tuna miaka mitano

ambayo ni midogo sana. Wao kwa ajili ya mikakati tu ya kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya ajira walitenga miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi kwa mama yangu pale Mheshimiwa Anne Kilango ameshangaa kukutana na *Air Hostess*, mimi nilishangaa kwenda Geneva tumekuja kupokelewa na gari la Ubalozi wa Tanzania dereva ni Mkenya. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani *no heart feeling* kwa yule jamaa, labda kaoa Mtanzania, *I do not know!* Lakini nilishangaa na nikauliza eeh bwana, hii inakuwaje? Wakasema *ooh*, Watanzania hawajui Kifaransa! Hawajui Kifaransa, mimi naenda *Alliance François* kila siku nawakuta vijana wanasoma Kifaransa na kuna programu za kifaransa pale! Kwa hiyo, tunarudi palepale suala la mipango. Yule mtu aliyekuwa kule aliyemwajiri yule kijana wa Kenya alichukua hatua gani kuhakikisha kwamba anatoa fursa kwa vijana wa Tanzania wenyе sifa kama zile ili wakafanye kazi ile. Nina uhakika hilo halikutokea na kuna namna ilitokea na ndiyo maana yule mtu akabaki kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasema tuanzishe mfuko, Mheshimiwa Kigwangalla anasema tuanzishe mfuko tujikite kwenye kilimo, kilimo tumefeli nchi hii, kilimo kiko *ICU*. Tunasema kila siku sasa hivi tumeishia tu kuonesha mafanikio ya kilimo kwenye *television*. Ukiangalia *ITV* unasikia mipango ya Awamu ya Nne, mafanikio katika kilimo, unaona mashamba mazuri pale ya wawekezaji, malori makubwa, helkopta za kumwagilia, tunachukua kama ndiyo mafanikio yetu katika kilimo, wakati mkulima halisi wa nchi hii

amepigika, ana matatizo hawezi kupata hata mbolea. Mkulima ana hekari tatu, anapewa mbolea ya nusu heka au robo heka, sasa huyu mkulima atatoka vipi kwenye umaskini halafu leo hii unasema kwamba uwapeleke vijana kwenye kilimo, *they will not believe you!* Hawatakuamini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama tutafanikiwa kusukuma kilimo na tukaendelea, kadiri kilimo kinavyoendelea na kuwa cha kisasa ndivyo nguvukazi yake inapungua. Utakuta kijana mmoja ana trekta lake analima ekari 200 kwa hiyo, hakuna tena vijana 100 pale wa kushika majembe kulima. Kwa hiyo, wale watatakiwa tena warudi viwandani; viwanda ambavyo kimsingi tumeviuwa. Sasa hapo ndipo tulipo. Kwa hiyo, hizi habari za kusema sijui Mifuko, habari za kusema sijui nini, hizi hazitatusaidia kitu chochote, tujikite kwa dhati katika kutafakari na kujitafakari kwamba, tunatakiwa tufanye nini ili kuondoa tatizo halisi la ajira kwa vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa nchi hii tukirudi, kwa sababu Mheshimiwa Kigwangalla hakutangaza *interest* kwamba yeye amehusika na kilimo, mimi ninatangaza *interest* kwamba, ninahusika na masuala ya usanii, ni msanii. Lakini angalia ni ajira ngapi zimetoka kwenye eneo la wasanii na Serikali tumechukua miaka mingapi kupigana nayo ili kutambua tu kwamba kuna ile shughuli? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tumeleta hoja ya *sticker* za *TRA*, wakati ule Mheshimiwa Nchimbi yupo, Mheshimiwa Nchimbi akakubali, tukashirikiana vizuri. Watu walipoona kwamba lile jambo limekaa kisiasa, wamelidaka

juu kwa juu, mara unalionna kwenye *TV*, sijui kuanzia leo *TRA* wasanii wa nyumbani, hautakiwi kuweka *sticker* kwa wasanii wa nyumbani peke yake; weka *sticker* kwa kazi zote za sanaa kwa sababu, ukiweka *sticker* kwa kazi za wasanii wa nyumbani peke yake ukawaacha akina Dbanji wa Nigeria, akina Fally Ipupa, watu watachagua kule ambako wataendelea kununua *CD* kwa 500/=, 1,000/=, wataacha hizi *CD* zenye *sticker*. Kwa hiyo, hii ni namna ambavyo tunafanya mambo yetu kuhusiana na vijana, kisasa, tunaangalia *political mileages*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninaomba tufike mahali, sasa vijana wameshtuka; sijui ni nani yule alisema, Mheshimiwa Mkosamali, sijui nani alisema, vijana sasa hivi wameshashtuka, wanajua kila hatua. Haitusaidii kwenda kuwadanganya na *Viboda-boda*, sijui eti unaenda unakutana na vijana, nitawapa *Boda-boda* moja, nitawapa *Boda-boda* mbili, vijana wanataka zaidi ya hapo; vijana wanataka fursa zaidi ya hapo, sasa sisi tumekaa tu tunasema mifuko, tuanzishe mifuko, sijui tuanzishe nini? Hayo hayatatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu katika masuala ya kutatua matatizo ya ajira ya vijana, tunatakiwa kuwa *serious* zaidi kuliko hizi slasa tunazopiga humu kwa ajili ya kutafuta *mileage*.

## TAARIFA

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, lakini Taarifa dakika ya mwisho. Haya, mwenye Taarifa yake, Mheshimiwa Kangi Lugola!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Mbilinyi anashangaa kukuta dereva kwenye Ubalozi wa Tanzania ni Mkenya, napenda nimpe Taarifa kwamba, hata madereva wa ng'ombe tunaowachunga kule nyumbani ni Wanyarwanda. Hata ukienda kwenye nyumba nyingine, utakuta hata wanaofanya kazi za ndani nao pia wanatoka nchi nyingine. Kwa hiyo, kuna tatizo kubwa sana la kuajiri watu katika nchi hii.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Aah, jamani, sasa mnaleta fujo; haiwezi kuwa Taarifa juu ya Taarifa, malizia.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilichotaka kumpa Taarifa ni kwamba, suala la ajira, turudi pale ambapo siku moja Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwahi kusema kwamba, ajira nyingine wanachukua watu wengine kwa sababu, Watanzania kufanya kazi hawataki na wanabagua ajira nyingine. Kwa hiyo, suala la mfuko kweli linaweza likawa na matatizo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Hiyo haina haja ya Mheshimiwa Mbilinyi kuijibu kwa sababu alikuwa amezungumzia mfano halisi kwamba alimkuta dereva, ni kitu halisi; kwa hiyo, haina haja ya kuleta ubishi.

Mheshimiwa Tundu Lissu, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma maelezo ya Mheshimiwa Dokta Hamisi Kigwangalla, kuhusiana na hoja hii pamoja na maelezo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba, hoja inaonekana nzuri sana machoni. Inasikika nzuri sana masikioni na pengine kwa sababu tunaelekea mwaka 2015, inawezekana ikawa ina malengo yasiyokuwa ya ajira ya vijana *as such*, ila ina malengo ya 2015 ya kujipendezesha kwa wapigakura na vitu kama hivyo. Nachotaka kusema ni kwamba, hoja hii haina tafakuri ya kutosha. Hoja hii haina fikra za kutosha. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mikopo kwa kundi lolote lile la kijamii sio suala geni katika nchi hii. Si la leo, si la jana, wala si la juzi, ni mambo yanayojirudiarudia. Tuna-recycle the same old lies.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006, wakati Mheshimiwa Rais anaanza awamu yake ya kwanza, ilikuja habari ya mabilioni, yaliitwa "Mabilioni ya JK", mikopo kwa akina mama; zikatoka fedha za umma mabilioni. Leo nani anayeweza kusimama hapa akatuangalia machoni,

akawaangalia Watanzania machoni, akawaeleza hiyo ajenda ya mikopo kwa akina mama iliishia wapi? Mabilioni ya JK, yalimsaidia mwanamke yupi? Ni wangapi waliokombolewa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, mwaka juzi, mwaka 2011, iliamuliwa ianzishwe Benki ya Vijana ili itoe mikopo kwa vijana wajajiri; leo mwaka umepita, hakuna kitu. Benki ya akinamama ipo, imetoa mikopo kwa wanawake laki ngapi wa Tanzania? Imewakwamua wangapi? Inawapa akina nani mikopo? Ni nani anayeweza kuwaambia wanawake wa Tanzania leo, wa Jimbo langu la Singida Mashariki kwamba, kuna Benki yenu inayotakiwa iwape mikopo? Hii sio Singida Mashariki tu, hata kwa Mheshimiwa Dokta Mary Nagu, Hanang, nani, nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna habari inaitwa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu, ni vita. Kuna maelfu ya wanafunzi ambao wako majumbani sasa hivi tunavyozungumza, hawawezi kusoma, wazazi wao hawana hela, walihidiwa mikopo, hawajapata mikopo kwa sababu, sungura ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia miaka nendarudi, zamani nilikuwa Mtafiti wa Masuala ya Madini, miaka ya 1990, ukiangalia Sera zote za Madini, ukiangalia hotuba zote za Mawaziri wa Madini, tutatoa mikopo kwa wachimbaji wadogowadogo ili wajajiri. Tumewapa wangapi? Tumempa nani? Tunamdanganya nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kwa wakulima, mikopo kwa wamachinga, mikopo kwa wavuvi; ni nani ambaye amepata? Kama hiyo sio lugha ya kutongozea kura za 2015, ni ya nini? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hakuna tafakuri ya kutosha. Hakuna fikra kwenye hoja hii, ni mambo ya kuokotezaokoteza tu. Katika nchi zote zilizoendelea, zote, zote ambako tunapenda kwenda kujifunza kutoka kwao na tunatembea kweli, niambieni Marekani, Jumuiya ya Ulaya, Japan, wapi kuna Benki ya Vijana, inayotoa mikopo kwa vijana wajajiri? Au Afrika ya Kusini, majirani zetu? Haya mambo ni ya ubabaishaji wa Kitanzania yenyе lengo la kudanganya watu tu *and we are sick and tired of being lied to.* (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu ambao wanahangaika kujitafutia ajira, wanahangaika bila msaada wowote. Nchi hii machinga wanahangaika ili wasiwe wezi, kwa sababu, hatujawasaidia hata kimoja. Badala ya kuwaacha angalau waendelee na hiyo ajira waliyojitalfutia, tunawapelekea Askari wa Jiji kila mahali, kila mahali! Wale hatujawasaidia, wanahangaika, hawataki kuwa wezi, tunawalipisha ushuru, tukishawalipisha ushuru, tunawapelekea Askari wa Jiji wanawatandika, wanawanyang'anya vitu vyao. Akina mama-ntilie hivyo hivyo, wakishalipa ushuru ndio tunajua kwamba ni wachafu, wanauza kipindupindu, tunawanyang'anya vyombo vyao vyaa mapishi, tunawaharibia ajira walizozitengeneza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2001, miaka 12 iliyopita, kuna Wataalamu wa Tanzania humuhumu na wenzao wa Kimarekani, waliandika utafiti juu ya kitu walichokiita Umuhimu wa Kiuchumi wa Uchimbaji wa Madini unaofanywa na wachimbaji tunaowaita wadogowadogo. Kwenye *study* yao wakasema kwamba, hakuna sekta nyingine yoyote ya kiuchumi katika kipindi cha miaka ya 90 ambayo ilitengeneza ajira kuliko hii ajira ya wachimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati hiyo *study* inachapishwa mwaka 2001, tulishawanyang'anya wachimbaji wadogowadogo wa Kitanzania maeneo karibu yote, tukawakabidhi wageni ili watengeneze ajira. Ukisoma takwimu za Wizara ya Nishati na Madini, makampuni yote ya madini hayajafikisha ajira 12,000. Tumeharibu ajira mamilioni, kufuatana na hiyo *study* ya *Economics of Mining*, ili kutengeneza ajira elfu kumi na ngapi, hazifiki 12,000. Kwa hiyo, pale wanapojaribu, wao hawajasaidiwa, tunaenda tunawaharibia, halafu tunakaa tunaanzisha vitu vinaonekana sexy-sexy hivi, ni ubabaishaji mtupu; hii ni lugha ya 2015. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa kwamba, hiyo Benki ya Vijana, ambayo mimi sijawahi kuisikia kwingineko ninaisikia hapa, itoe mikopo bila kudai *security*. Maana yake ni kwamba, fedha za umma, fedha za walipa kodi, zigawiwe kwa watu bure, wakizila hakuna namna ya kuzirudisha; hii ndio hoja ya kuleta Bungeni kama sio lugha ya kutongozea kura za 2015 ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba tu nipayendekeze haya yafuatayo; tunachohitaji, sikatai kwamba tuna tatizo kubwa sana la ajira, tunachohitaji ndugu zangu ni '*a marshal plan*', tunahitaji mpango mkubwa wa kufufua uchumi. Tunahitaji *massive investment* katika maeneo ya kiuchumi yatakayotengeneza ajira. Kwa mfano, tunahitaji kuwekeza *massively* katika viwanda vya pamba, vya nguo, ili hii pamba ambayo inauzwa marobota leo, itengenezwe nguo leo. Tunahitaji *massive investment* kwenye *infrastructure*, kwenye miundombinu, kwenye barabara, kwenye maji, kwenye miundombinu ya kila aina; ukianzisha ujenzi wa barabara unatengeneza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kuwekeza *heavily* katika sekta za kiuchumi ambazo ni *labour intensive*. Ukianzisha *investment* ya aina hiyo, ni lazima unatengeneza ajira bila benki hii inayozungumzwa kwenye hoja hii. Hii ni hoja ambayo ni *poorly thoughtout, ina-appear sexy but it is nothing*. (*Kicheko/Makofi*)

## KUHUSU UTARATIBU

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Kuhusu Utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu Utaratibu. Mheshimiwa Ole-Medeye, Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1)(g).

inasema kwamba: “*Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.*” (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji anayeendelea ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ametumia maneno kadhaa ya kuudhi katika mchango wake. Kwanza kusema kwamba hoja imeletwa kwa ajili ya kutongozea kura maana yake ni kwamba, sisi tunatumia hoja kwenda kutongoza wapigakura, hiyo si lugha inayokubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, lugha ya kusema kwamba, hii ni hoja ambayo iko *poorly*, iko *sexiest*, naomba Mwongozo wako.

## TAARIFA

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa, naomba nimpe Taarifa Mzee wangu Goodluck Ole-Medeye, Naibu Waziri, kwamba, neno ‘Kutongoza’, kwa tafsiri rahisi ni ‘Kushawishi’. Kwa hiyo, hatuoni ubaya wa neno hili. Nafikiri akasome Kamusi na tumwombe Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, atatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, neno 'Kutongoza' na mimi nimesoma Kiswahili tu kwa kiwango kizuri, ni 'Kushawishi'. Sasa sijui ubaya wake uko wapi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakataa Taarifa yake na nimwambie tu kwamba, mimi ni Mtaalamu wa Kiswahili, nimefundisha Kiswahili katika ngazi mbalimbali na kwa hiyo, lugha yoyote inategemea *context* ambayo inatumika, katika *context* hii, lugha hiyo haikubaliki. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Niliyeombwa utaratibu ni mimi na muda wangu ni mdogo sana, nahitaji angalau kupata wachangiaji wawili wengine. Mheshimiwa Jenista Mhagama!

**WABUNGE FULANI:** Bado hajamaliza!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista Mhagama!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**WABUNGE FULANI:** Hajamaliza!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa bado sijamaliza.

**MBUNGE FULANI:** Hajamaliza!

**NAIBU SPIKA:** Ulikuwa umeshamaliza, Mheshimiwa Jenista!

**MBUNGE FULANI:** Hajamaliza bado.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamaliza bado.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Tundu, hajamaliza!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamaliza!

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**NAIBU SPIKA:** Wakati gani ulikuwa umebakiza Mheshimiwa Tundu Lissu tena?

**MBUNGE FULANI:** Bado hajamaliza.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipaza  
sauti kusitiza kwamba Mhe. Tundu A.M. Lissu  
alikuwa hajamaliza muda wake)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamaliza, kengele haijalia.

**NAIBU SPIKA:** Haya, malizia basi kwa dakika hiyo moja.  
*(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane na sio vizuri sana kila wakati tukageuza Bunge kuwa ni shule ya sekondari, mahali pa vijana ambao hawajabalehe hivi, eeh.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**NAIBU SPIKA:** Itakuwa ni jambo ambalo si sawasawa hata kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa dakika moja. Tupate wachangiaji wengine wawili kwa harakaharaka.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili vijana watakaopewa mikopo kweli waitumie mikopo kwa uzalishaji mali, kuna kitu kinaitwa kuwafundisha namna ya *ku-manage* fedha. Kuna watu wamezaliwa mjini hawajawahi kushika jembe, unawapelekaje shambani na milioni tano za mkopo ukawaambia limeni, unawaambiaje, wanaenda kufanya nini? Tumewafundisha *financial management*, tumewafundisha kilimo, tumewafundisha *skills*, hii hoja inasema yote hayo au tunagawa mahela tu, *what is this?* Ndiyo maana ninasema hii hoja haina tafakuri, haina fikra, ni hoja ya kutongozea wapiga kura. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista Mhagama!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu*)

## **NAIBU SPIKA:** *Order, order!*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii. Nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kukubali marekebisho yaliyoletwa na Mheshimiwa Ester Bulaya akimuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla lakini nampongeza Mheshimiwa Ezekia Wenje aliyeunga mkono mabadiliko haya kwa maana hoja hii ni hoja yenye msingi katika kipengele alicholeta cha mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu niseme kidogo, haiingii katika akili yangu leo katika Taifa hili la Watanzania na sisi Waheshimiwa Wabunge tunaotambua kwamba nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la ajira kwa vijana, si tu vijana waliosoma hata vijana walioko vijiji na mtu akapinga hoja hii kwamba ni hoja isiyokuwa na msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inanisikitisha, nasema hivyo kwa nini? Wabunge hapa wanakubali kwamba vijana hawana ajira na wanaunga mkono kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inataka kutekeleza llani iliyosomwa kwa kuzingatia hoja hii ili kuwashawishi Watanzania waikubali Serikali yao, naam ndiyo kazi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Hivi ni Serikali gani eti iogope uchaguzi kutatua kero za wananchi wake ambao ni wapigakura wake, mimi sijapata kuona Serikali ya namna

hiyo. Serikali makini, Serikali inayoelewa, itatambua matatizo ya wananchi na wapigakura wake na itayatatua mpaka siku ya mwisho ya utawala wake. Namwonea huruma Mbunge ambaye hatafurahia Serikali itekeleze llani kwa hoja hii leo kwenda kutatua kero za vijana wetu, Mbunge huyo namwonea huruma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme yafuatayo; hoja hii inasema hivi na baada ya kurekebishwa na Mheshimiwa Ester Bulaya, Serikali ianzishe mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana kwa kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana wanaowekeza kwenye kilimo, lakini mara ya kwanza tukaona kwamba hatuwezi ku-*concentrate* kwenye kilimo tu, lakini twende kwenye viwanda. Mheshimiwa Ester Bulaya hapa, Mbunge wa CCM amesema twende kwenye mifugo, twende kwenye uvuvi, twende na kwenye sekta nyingine kama alizosema Mheshimiwa Ezekia Wenje, wale vijana wetu wasomi wajajiri kutengeneza hospitali kwa wale Madaktari, wale waliosomea *Engineering* watengeneze viwanda ambavyo vinahusiana na sekta yao, lakini Mbunge anasimama hapa anasema kwamba huu mfuko hauna maana. Hivi kweli kuna nchi ambayo haioni umuhimu wa kuwezesha vijana wake wafanye haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, nilihudhuria mkutano wa 101 wa Shirika la Kazi la Ulimwengu. Nchi kadhaa zimeleta maendeleo yao katika kutatua matatizo ya vijana na kila kilichofanyika katika kila nchi, *document* ninayo hapa na ninaweza kukuletea Mezani kwako nisionekane nalidanganya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila nchi ilikuwa na muundo wake wa kutatua tatizo la ajira kwa vijana. Tanzania imeamua kutatua ajira kwa vijana kupitia Azimio hili la Bunge leo, kwa kuanza na hii hoja ya kwanza ya kuanzisha Mfuko na kupelekea Benki ya Vijana, tatizo ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa naongea na Wabunge wa Uganda ili kujifunza uzoefu wa nchi ya Uganda. Waliniambia kitu kimoja, sisi hatuna lakini nadhani tutakwenda kujifunza, wana kitu kinachoitwa *cash transfer*, wanatengeneza fedha ya kuwasaidia wazee na watu wasio na ajira katika kujikimu. Leo Tanzania hatuna, sisi tukisema kwamba kile kinachofanywa na Uganda ni kitu kizuri halafu itaonekana Uganda haina maana. Uganda watakuja kujifunza kwetu sisi tukianza, nchi nyingine zitakuja kuanzisha Benki ya Vijana. Kwa hiyo, sioni tatizo, vijana wanahitaji kuwezeshwa na ninakuambia Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, umefanya vema kuisaidia Serikali yako ifanye maamuzi yaliyo sahihi ili kuwashawishi wapigakura kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio lingine hapa linasema kwamba Serikali itenge fedha kutoka kwenye bajeti yake na vyanzo vingine kwa ajili ya mfuko huo utakaotoa mikopo kwa riba ndogo na masharti nafuu. Hee! Mbunge anakataa, Mbunge anakataa? Hivi tunaposema kila siku hapa ndani na nitakwenda kuangalia *Hansard*, niangalie ni Wabunge wangapi wamelalamika kwa riba kubwa zinazotolewa na mabenki ambazo haziwasaidii maskini vijijini. Leo tunapitisha Azimio hili ili kwenda kuwakomboa vijana wetu waweze kupata mahali pa kupata pesa

kwenye mikopo ya riba nafuu, Mbunge hapa anasema kwamba Azimio hili halina msingi.

### **MBUNGE FULANI:** *Security!*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee, wakati Mheshimiwa Ester Bulaya anafanya marekebisho haya, aligundua tatizo hilo lililozungumzwa la mambo ya *security* na vitu vingine na ndiyo maana akaamua kuijenga hoja hii mpya, hayo mambo mengine yatajadiliwa kwenye *regulations* siyo kazi yetu Bunge kuyatengeneza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea, hoja ya Azimio hili inaendelea kusema hivi, Serikali kupitia sekta zote za kiuchumi zinazohusika na mpango huu, huu mpango maalum, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka unanisikiliza na utatakiwa kuusimamia Waziri wetu, Serikali kupitia sekta zote za kiuchumi zinazohusika na mpango huu ihakikishe vijana wanafanikiwa kupitia malengo yao katika mnyororo wote wa thamani (*value chain*) na mnyororo wa thamani ni kutoka kwenye *production*, *processing* na *marketing*. Kuzalisha na kuhudumia huduma zote na baadaye kwenye masoko. Leo tunalamika masoko ya mazao ya wakulima wakiwemo vijana wetu vijijiini, Azimio linaenda kutatua tatizo hilo, tunasema Azimio hili halifai! Ninaomba Waheshimiwa Wabunge muelewe umuhimu wa Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina vikundi vingi sana kule kwenye Jimbo langu la Peramiho vyा vijana. Nina wasomi wangu wengi kwenye Jimbo la Peramiho, wanahitaji kujajiri

ama kuajiriwa, huu mfumo tunasema kama tutasimamia vizuri *value chain*, ina maana tunaweza kuwasaidia wasomi wakaajiriwa na wale vijana wetu wengine na wao wakajajiri. Leo tunaona hapa tunalima mbegu nyingi za mafuta, hatuna viwanda. Mimi ni Mwalimu, maendeleo ya Ulaya yalitokana na viwanda vidogovidogo baada ya mafundi wadogo kuwezeshwa, hayakutoka kwingine kokote, ninaomba niendelee kusitiza Azimio hili ni jema na mwafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili linakwenda kujenga maeneo maalum ya vijana kwa ajili ya shughuli za kiuchumi. Nani haelewi vijana wengi wamezaliwa wamekuta wazazi wao ndiyo wanamiliki ardhi. Anapotaka kuanzisha shughuli yoyote ya kiuchumi ni lazima akaombe ardhi kwa baba yake na mama yake na inategemea baba na mama wale wana mapenzi kiasi gani kwa mtoto yule ndiyo wamgawie ardhi ya kuweza kufanya kazi. Leo Serikali hapa kwa Azimio hili inaagizwa kwenda kutenga maeneo maalum ya kuwawezesha vijana wetu hawa kufanya kazi hizo nzuri za kupunguza tatizo la ajira, mtu anasimama hapa anasema wasitengewe maeneo ya kufanya kazi hizo!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi inanishangaza na inanichanganya. Matokeo ya sensa yanasema Tanzania sasa hivi tupo karibu milioni arobaini na nne na kitu na kadiri ya taarifa za awali, naomba niseme za awali, vijana ni takribani 61%, niambie ni Serikali gani haitataka kujishughulisha na asilimia hiyo 61 ya Watanzania ambao ni watu takribani milioni ishirini na nne ikakaa tu bila kujua kitakachotaka kuendelea kwa vijana wetu? Hiyo Serikali itakuwa ni Serikali ya ajabu, itakuwa ni Serikali ya ajabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana niwaombe Wabunge wenzangu tuunge mkono Azimio hili, asilimia 61 ya vijana waliosoma ndani yake, vijana ambao wako vijiji ni wanahangaika ambao sasa hivi ndiyo hawa wamehama vijiji ni na kufika mjini na hawana shughuli maalum za kufanya matokeo yake inakuwa tu ni vurugu ambazo hazina uelekeo. Kumbe kwa Azimio hili tuna uwezo sasa wa kuwawezesha vijana hawa 61% wakatulia walioko vijiji ni wakabaki vijiji ni, walioko mijini wakaendelea na kazi, waliosoma wakapata ajira zao. Azimio hili ni muhimu sana kwa sasa kwa Serikali yetu na kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwengine mzuri wala siwezi kuukataa, ni kweli inawezekana mifuko hii imekuwa mingi katika nchi yetu, tutazame uwezekano wa kuiunganisha na kutengeneza mfuko utakaokuwa na nguvu kubwa ya kujibu hoja na maswali yote ya vijana wa nchi hii katika tatizo la ajira. Hilo nakubali ni wazo jema kabisa lakini wazo la kusema Azimio hili halina maana, halina msingi nalikataa na ninamshangaa Mbunge ye yote atakayeunga mkono kwamba wazo hili halina msingi, kwa kweli nitamshangaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza maneno haya kwa uchungu nikiwahurumia vijana wangu wa Jimbo la Peramiho wasomi na wasiosoma na nikijua ukombozi wa vijana wa Jimbo la Peramiho na nchi nzima ya Tanzania uko njiani kuja kwa kupitia kwenye Azimio hili na ninaamini kwa uwezo wa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi watafanya haya na ninaamini kwa nguvu ya Wabunge wa

Chama cha Mapinduzi ndani ya Bunge hili watasimamia *agenda* hii ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi na ninaomba niunge mkono Azimio la Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa 100%, nashukuru sana.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeke kwa kifupi sana.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa chini ya Kanuni ya 68(7) na 64(d) na lengo langu ni moja, ni kuomba Mwongozo wako ili tuweze kuweka mambo bayana maana Bunge ni mahali pa heshima sana na ni mahali ambapo watu wazima wanaosikiliza Bunge wanahitaji kuambiwa habari ya kweli lakini wanahitaji pia kuambiwa kwa lugha ya staha na pale ambapo Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeke amekosea, naye akosolewe kwa lugha ya staha na kwa kutumia maneno yanayofanana na mahali tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa kukwazwa na maneno ya rafiki yangu mpendwa Mheshimiwa Tundu Lissu, mtu ambaye mnajua hata ninyi wote mimi namheshimu sana lakini maeneo mawili sikfurahia.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni kubeza mawazo ya busara na kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Mbunge Dkt. Hamisi Kigwangalla kwenye hoja ya msingi kabisa ya kuzungumzia mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana

na kuanzisha mfuko wa vijana utakaokopeshaw Vijana kwa riba ndogo na masharti nafuu. Kwa kauli alizozitoa Mheshimiwa Tundu Lissu, zilikuwa zinabeza, ni kauli za kuudhi maana zilikuwa zinaonyesha kana kwamba Mbunge aliyefanya kazi kubwa kama hii hakufikiria wala hakutafakari kazi alioiletakini kazi hiyo siyo kwamba sisi tumeiunga mkono lakini hata Wabunge wa chama chake, wameleta marekebisheso na wakakubaliana na marekebisheso ya hoja ya Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla, sasa sijajua kama wasiofikiria ni wapi maana wote kwa pamoja, Wabunge wa pande zote tumeiona ni hoja ya maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi ya yote, bado mimi siyo mtaalam sana wa lugha ya Kiswahili lakini najua nina uwezo wa kwenda kumshawishi mama kwa jambo aelewewe na kila mmoja anaweza akasema mama hakulielewa akamshawishi lakini huwezi ukamuambia mtu nenda kamtongoze mama yako. Kwa hiyo, neno la kutongoza na kushawishi ni maneno yanayotumika katika mazingira tofauti na vizuri wataalam wa lugha wawasaidie pia Waheshimiwa Wabunge kulielewa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nilikuwa nataka tu kuomba Mwongozo wako kama lugha za aina hii za kushambuliana zinaruhusiwa ndani ya Bunge au wakati mwingine ni vizuri hata kama Mbunge anachangia utusaidie kukatisha Wabunge badala ya kusubiri Wabunge wawakatishe na kuomba Mwongozo ili kuweka mambo kwenye barabara iliyo nzuri na hasa tunapozungumza na Waheshimiwa Wabunge ambao tunawaheshimu sana, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Muda wangu ni mdogo sana, Waheshimiwa nina mambo fulani Mezani hapa Mheshimiwa Mchungaji kwa dakika chache.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, mimi naomba Mwongozo wako, natumia Kanuni ya 68(7), kuna wakati ulizungumza kuhusiana na jengo hili kuwa lina- *leakage*, sasa kwa bahati mbaya tuna Serikali ambayo mara nyingi imekuwa *reactive* badala ya kuwa *proactive*, nilitaka tu Mwongozo wako kama hili jengo liko salama kwa uhai wa Wabunge kwa sababu linavuja sana na uuhakikishie umma wa Tanzania kwamba tunapoendelea, hapa nilipo penyewe ninapokaa panavuja, pale kwenye nafasi yangu panavuja na sehemu nyingi. Sasa niliomba Mwongozo wako kuwashakikishia Watanzania kwamba Serikali nzima na Wabunge wote 357 hapa kama tuko salama kwenye jengo hili. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa. Nakuomba Mheshimiwa Modestus Kilufi pale ulipo kwa dakika moja ulikuwa umenipa habari fulani, naomba ujaribu ku-share na Waheshimiwa Wabunge kwa kifupi sana.

**MHE. MODESTUS D. KILIFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa majonzi makubwa, nimepokea taarifa ya ajali mbaya ambayo imetokea kwenye shamba la mwekezaji wa lililokuwa la NAFCO Mbarali - Kapunga. Huwa anatoa lori kwenda kuchukua vibarua kwenda shambani kwake, lilibeba vijana zaidi ya 100 na kwa bahati mbaya limeanguka na kuua wanne palepale, watano wamefia Hospitali na watu zaidi ya 50 wana hali mbaya,

wako Hospitali ya Chimala na wengine wako Hospitali ya Rujewa ya Wilaya na wengine wamepelekwa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Mbeya. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuungana kwa pamoja na nyie Waheshimiwa Wabunge kuwapa pole wananchi wa Mbarali waliopatwa na maafa haya na kuwapa pole na kuwatachia afya njema wale wengine wote ambao wanaendelea kuugua katika Hospitali mbalimbali Mkoani Mbeya na Wilayani Mbarali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, niliona jambo hili lifahamike na Waheshimiwa Wabunge tuungane nao katika kuwapa pole na kuwatachia afya njema wale majeruhi ambao wanaendelea kupata huduma katika Hospitali mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa pole sana kwako Mheshimiwa Mbunge, uongozi wote wa Wilaya ya Mbarali na familia za ndugu waliopoteza maisha pamoja na ambao ni majeruhi ambao wako Hospitali na tunawaombea sana majeruhi wapate nafuu ya haraka lakini pia tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu waliotangulia mbele ya haki mahali pema peponi, poleni sana.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, baada ya hatua hiyo, nije kwenye masuala ya miongozo, mwongozo wa kwanza ni wa ujumlajumla wa hoja aliyotoa Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye na ikarudiwa na kuzingatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ya kuhusiana na kuchagua maneno kadiri tunavyozungumza.

Waheshimiwa Wabunge, tutakumbuka mara nyingi sana ninyi wenyewe mmelalamika na Kiti hapa mara nyingi sana tumelalamika kwamba iko haja kubwa sana ya kutumia lugha vizuri, inaelekea Waheshimiwa Wabunge baadhi yetu tuna tatizo kubwa hilo. Basi wajibu wetu kwa kweli ni kuendelea kukumbushana. Pamoja na tofauti zilizopo, pamoja na nini kilichopo, ni vizuri kuhakikisha kwamba tunakuwa na lugha zisizokuwa za kuudhi kama vile Kanuni zetu zinavyotutaka tuwe. Asubuhi nilieleza kwamba tunaitwa Waheshimiwa, ni vizuri tukawa na lugha za kiheshimiwa vinginevyo itakuwa ni tatizo sana na tukumbuke kwamba wananchi wanatuona na ni wananchi wa rika zote, wananchi wa kila aina watu wazima, kina mama, kina baba, wengine wasingepeenda kusikia lugha fulanifulani na inatufikisha mahali inatuweka kidogo mahali pa kudharaulika. Kwa hiyo, natoa wito tena kwa mara nyingine, kwamba tujitahidi kuangalia tunatamka nini kwa kadiri tunavyoweza. Kiubinadamu mtu akiwa na hasira kidogo anaweza akapitiliza hapa na pale kwenye mistari lakini ni wajibu wetu kujichunga.

La pili linaloendana na hilo hilo ni kwamba tuwe na uvumilivu kidogo, pande zote, wakati mwingine kasheshe za namna hii ni *expected* lakini sio za lugha mbaya. Kasheshe za kutingishana hapa na pale zinatarajiwa. Kwa hiyo, yale mambo ya kuzomeazomea na nini tuyapunguze sana.

Kuhusu jengo, jengo ni kweli lina matatizo. Lina matatizo kwenye paa pale katikati. Kama nilivyoeleza asubuhi, wako wataalamu wetu wanahangaika sana kuhakikisha kwamba jambo hilo linarekebishwa haraka iwezekanavyo.

Nakuja kwenye mwongozo wa Mheshimiwa James Mbatia, asubuhi kulitokea yale yaliyotokea, bahati mbaya akatoka nje na baadhi ya Wabunge. Huku nyuma kama nilivyokuwa nimeahidi kwamba nitatoa maelezo yangu, baadaye yeye alikuwa nje nafikirki hakuweza kunisikia lakini nilikwishashughulikia jambo lile ambalo alikuwa anataka nilitolee mwongozo. Yeye dai lake anaomba kwamba Waziri, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, alipokuwa anachangia hoja yake alikuwa na kijitabu alichokionyesha cha kuhusu Mitaala, kwa hiyo, yeye alitaka kiwekwe Mezani.

Majibu ambayo ninayo ya uhakika kutoka Serikalini ni kwamba Mheshimiwa Waziri amekwishaagiza Dar es Salaam kwa wachapishaji *copy* 300 kwa ajili ya Wabunge na *copy* hizo zitaletwa kwa Katibu wa Bunge tarehe 6/2/2013, wiki ijayo. Kwa hiyo, tunaamini kwa yale ambayo tumesema na yale ambayo tumeagiza sisi kama Meza katika Mwongozo wangu asubuhi ulikuwa ni kwamba Serikali ilete Mitaala tajwa Bungeni kabla ya Bunge hili kuahirishwa tarehe 8/2/2013, kwa hiyo wameahidi kwamba *by* tarehe 6/2/2013 Mitaala hiyo itakuwa katika Ofisi ya Katibu wa Bunge, kwa hiyo, naomba subira, tutafika mahali tu pa kuelewana.

Mwisho ni matangazo, tangazo langu ni moja tu, ni kutoka kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, anawaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane kesho tarehe 2/2/2013, saa nne asubuhi katika ukumbi 219, jengo la utawala.

Baada ya maneno hayo, bado orodha ya uchangiaji inaendelea na kwa hiyo tutaendelea Jumatatu asubuhi na kwa jinsi hiyo...

## MWONGOZO WA SPIKA

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Bahati mbaya mmechelewa, nimeshasimama, naomba kuhairisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 4 Februari, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*

## VIAMBATISHO

### MAJIBU KWA MAANDISHI

**MAJIBU KWA MAANDISHI YA HOJA BINAFSI YA MHESHIMIWA  
DKT. HAMISI KIGWANGALLA YA KULITAKA BUNGE LIPITISHE  
AZIMIO LA KUANZISHA MPANGO MAALUM WA KUKUZA  
AJIRA KWA VIJANA KWA KUANZISHA MFUKO WA MIKOPO YA  
VIJANA WANAOWEKEZA KWENYE KILIMO NA VIWANDA  
VYENYE UHUSIANO WA MOJA KWA MOJA NA KILIMO**

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuchangia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala, Mbunge wa Nzega.

Awali ya yote, nampongeza sana Mheshimiwa Kigwangala kwa jinsi alivyoguswa na matatizo yanayowakabili vijana pamoja na ubunifu wake katika kuyatafutia ufumbuzi kama hoja yake inavyodhahirisha. Aidha, nampongeza Mtoa Hoja kwa kukubali marekebisho ya hoja yake yaliyoiboresha hoja hiyo. Nampongeza pia Mheshimiwa Gaudensia Kabaka (Mb.), Waziri wa Kazi na Ajira kwa kuleta mapendekezo ya marekebisho ya hoja hii; pamoja na Mheshimiwa Fenela Mkangara (Mb.), Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mchango wake ulioboresha hoja hii.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, sote tunakubaliana kwamba suala la kuwakwamua vijana na adha ya ukosefu wa ajira, na umaskini wa kipato unaotokana na adha hiyo; ni changamoto inayohitaji ushiriki wa wadau wengi na siyo Wizara moja au Serikali pekee. Napenda kuwapongeza Mhe. Esta Bulaya (Mb) na Mheshimiwa Ezekiel Wenje (Mb) kwa mapendezo yao ya marekebisho yaliyoboresha hoja hii. Aidha, niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii na kudhihirisha kwamba Waheshimiwa Wabunge ni wadau muhimu sana wanaopaswa kushirikiana na Serikali katika kupata ufumbuzi wa uhakika na endelevu wa changamoto mbalimbali zinazowakabili Vijana ikiwa ni pamoja na ukosefu wa ajira. Ushirikiano huu utatuwezesha kuongeza kasi ya maendeleo ya Nchi yetu na kuwahakikishia Vijana wetu maisha bora.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, kimsingi, nakubaliana na Mtoa Hoja kwamba vijana ni nguvu kazi ya Taifa ambayo haijatumika ipasavyo; na kwamba ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 7 kwa mwaka haujaenda sambamba na ukuaji wa fursa za ajira kukidhi mahitaji ya ongezeko la

nguvu kazi. Mathalan, kuna ongezeko kubwa la wahitimu katika ngazi mbalimbali za elimu lisiloendana na fursa za ajira zinazozalishwa na uchumi wetu. Hali hii inatokana na ukweli kwamba ukuaji wa uchumi unatokana na sekta ambazo hazina uwezo wa kuajiri watu kwa wingi kama vile sekta ya madini. Hii ni changamoto inayohitaji mikakati ya kukabiliana nayo ikiwa ni pamoja na kuweka msukumo zaidi kwenye sekta zenye uwezo wa kuajiri watu kwa wingi zaidi kama vile sekta ya Kilimo. Hii ndiyo sababu ya jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba rasilimali nyingi zaidi zinaelekezwa katika kubadilisha kilimo cha Tanzania ili kiwe cha kisasa na cha kibiashara badala ya hali ilivyo sasa ambapo kilimo chetu ni kile cha kujikimu.

Jitihada hizo ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunaondokana na kilimo cha kutegemea mvua na kuzingatia kilimo cha umwagiliaji. Jitihada nyingine ni zile za kuhakikisha Wakulima wetu wanatumia zana bora za kilimo ili hatimaye tuondokane na teknolojia duni na kilimo cha jembe la mkono. Sambamba na jitihada hizi Serikali pia inahimiza Wakulima kuzingatia mbinu bora za kilimo ikiwa ni pamoja na matumizi ya pembejeo za kilimo kama vile mbolea, madawa ya kilimo na mifugo pamoja na mbegu bora. Vilevile, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuweka mfumo wenyewe uhakika wa masoko ili kumhakikishia mkulima bei ya haki ya mazao yake. Lengo la jitihada za Serikali ni kuongeza tija katika sekta ya kilimo; inayojumuisha kilimo cha mazao, mifugo, uvuvi, ufugaji samaki, ufugaji nyuki na misitu. Aidha, ili kuhakikisha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kilimo, Serikali iko katika hatua za mwisho za kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Nchini. Benki hiyo pia itatoa mikopo itakayoimarisha mlolongo wa thamani

wa mazao ya kilimo "Value Chain". Dhamira ya Serikali katika kutekeleza Azma ya KILIMO KWANZA na Mpango wa Kukuza Kilimo kwenye Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) ni kufikia malengo hayo. Tukifikia malengo hayo tutakuwa pia tumeipatia ufumbuzi changamoto ya ajira kwa vijana kwa kiasi kikubwa.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, natoa wito kwa Wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Wizara na Idara zote za Serikali pamoja na Sekta Binafsi kushiriki kikamilifu kuhakikisha kwamba malengo haya ya Serikali yanafikiwa kwa maslahi ya Taifa letu. Aidha, natoa wito kwa Vijana wote kujipanga ipasavyo kwa kuhakikisha wanachangamkia fursa za ajira zilizopo kwenye sekta ya kilimo. Hii ni pamoja na kujielimisha na kupata ujuzi stahiki unaolingana na mahitaji ya sasa ya sekta hii. Mahitaji ya nguvu kazi yenye ujuzi mahsusni wa kilimo cha kisasa ni makubwa kwa kuzingatia kwamba uzalishaji unapaswa kukidhi viwango vya ushindani vya Kimataifa na Kikanda ili kujihakikisha masoko ya uhakika. Tusinghau pia kwamba matumizi ya sayansi na teknolojia ni mhimili muhimu katika kujenga misingi ya kilimo chenye tija. Hivyo, napenda kusisitiza umuhimu wa kukuza ushindani wa bidhaa zetu za kilimo kwenye masoko ya Kimataifa na Kikanda ikiwa ni pamoja na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Hapa napenda kuunga mkono msisitizo uliowekwa na Mtoa Hoja kwenye miradi ya kilimo na viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, utekelezaji wa mapendekezo ya Hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangala ni utekelezaji wa maelekezo ya Ibara ya 79 na Ibara ya 81 ya

Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Ibara hizo zinasisitiza umuhimu wa Serikali kutekeleza Mpango wa kuwawezesha wasomi kujajiri pamoja na umuhimu wa Vijana ambao ni kundi kubwa la nguvu kazi linalokabiliwa na changamoto za ukosefu wa ajira, ujuzi na maarifa ya kisasa kwa ajili ya uzalishaji mali na biashara. Hivyo, jitihada za Serikali zitaelekezwa zaidi katika kuwawezesha vijana kutumia vipaji vyao, nguvu zao na wingi wao katika kuijendeleza na kuchangia kwa kiwango kikubwa zaidi kwenye ukuaji wa uchumi wa Taifa. Eneo la kilimo na viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo lina fursa nyingi za ajira kwa Vijana. Serikali itaendelea na jitihada za kuwawezesha Vijana waliojipanga vizuri na kuandaa michanganuo ya miradi inayokidhi vigezo vya kukopesheka. Kama Taifa tunao wajibu wa kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kizazi hiki na kijacho kwa kuzingatia kwamba Vijana wenyewe nguvu wasipotumika vizuri watatumiwa vibaya na watu wasioitakia mema Nchi yetu hasa katika maandamano na fujo zisizo na tija.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Mikakati mbalimbali ya Serikali ya kuwawezesha vijana kumiliki uchumi wa Nchi yao na kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira imetekelizwa kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kuundwa kwa Mifuko mbalimbali ya kuwawezesha vijana kuanzisha na kuendesha miradi ya kiuchumi. Serikali imeunda Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama Chombo cha Kitaifa cha kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Baraza hili limeundwa chini ya Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Na. 16 ya mwaka 2004. Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inatoa mwongozo wa jumla

utakaohakikisha kwamba Wananchi wanapata fursa mbalimbali za kiuchumi ambazo zitawawezesha kujenga na kufaidika na uchumi wa nchi yao. Sera hii inalenga katika maeneo yenye kuleta matokeo ya haraka hasa yale yanayogusa maisha ya Wananchi wengi katika sekta zote za kiuchumi hususan sekta ya kilimo. Utekelezaji wa Sera hii unahuishisha Wadau wengi ambaao ni pamoja na Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sekta Binafsi. Kutokana na upana wa dhana ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na kuhusisha watekelezaji wengi Serikali iliona umuhimu wa kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia na kuratibu shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinazotekelawa na Wadau mbalimbali chini ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Mojawapo ya majukumu ya msingi ya Baraza kwa mujibu wa Sheria namba 16 ya mwaka 2004 ni kusimamia utekelezaji wa Mpango Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mifuko inayotekela Mpango huo. Baraza linaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mpango huo ikiwa ni pamoja na kuwapatia vijana maeneo maalumu ya kuendeshea shughuli zao za kiuchumi na kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana hao. Mpango huo unatekelezwa na Wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Habari Vijana, Utamaduni na Michezo inayosimamia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Mfuko huu ni mahsus kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana ili kuwawezesha kujajiri na kuajiri vijana wenzao kwa kuanzisha na kuimarisha miradi ya kiuchumi. Hadi sasa Mfuko huu umetoa mikopo yenye

thamani ya Shilingi Billioni 1.094. Changamoto kubwa ya Mfuko huu ni kiasi kidogo cha fedha kinachotengwa kisichokidhi mahitaji ya Vijana wote Nchini. Ni imani yetu kuwa Mfuko huu ukiimarishwa kifedha na kiutendaji utaweza kukidhi mapendekezo yaliyotolewa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali pia inawawezesha vijana kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi (*Mwananchi Empowerment Fund*) ambao upo chini ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mfuko huu unatoa mikopo yenyе masharti nafuu kupitia SACCOS ambapo wanachama wake ikiwa ni pamoja na vijana wamenufaika na mikopo inayodhaminiwa na Mfuko huu kupitia Benki ya CRDB. Hadi sasa mikopo yenyе thamani ya Shilingi Billioni 8.47 imetolewa katika mikoa 11 na Wilaya 12. Serikali pia inatekeleza Mpango wa kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wanaomaliza masomo ya Vyuo Vikuu ili kuwajengea uwezo wa kuanzisha miradi ya kibiashara katika fani walizosomea. Mpango huu unatekelezwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*), ambapo Vijana wanaokidhi vigezo maalum huwezeshwa kuanzisha miradi kwa kipindi maalum cha usimamizi (*incubation period*) hadi watakapopata uzoefu na kuwaunganisha Vijana hao na Taasisi za Fedha zitakazoendelea kuwapatia mikopo kwa ajili ya kuendeleza miradi hiyo.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Vijana pia wanawezeshwa kupitia Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wanawake Katika Sekta Isiyo Rasmi. Mfuko huu unasimamiwa na Wizara

ya Kazi na Ajira kwa lengo la kuwapatia wanawake, wakiwemo wanawake vijana, mikopo yenyé masharti nafuu ili kuwawezesha kuanzisha na kuendeleza miradi inayotoa fursa za ajira. Vilevile, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*Women Development Fund -WDF*) ulioanzishwa kwa Azimio la Bunge ambapo unapata fedha zake kutoka Serikali Kuu na asilimia 5 ya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi sasa Mfuko huu umetoa mikopo yenyé thamani ya Shilingi Bilioni 4.04. Aidha, Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali (*National Entrepreneurship Development Fund - NEDF*) unasimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (*SIDO*) kwa lengo la kutoa mikopo kwa wenyé viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo ili waweze kuanzisha na kuendeleza miradi ya kiuchumi. Tangu mfuko uanzishwe umeshatoa mikopo yenyé thamani ya Shilingi Bilioni 26.012. Vilevile, Serikali inashirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania kuanzisha Mfuko wa Kuendeleza Wakandarasi Wazalendo Nchini (*Construction Industry Development Fund*) utakaowasaidia Wakandarasi hao kupata dhamana zinazotakiwa kuandamana na maombi ya Zabuni mbalimbali za ujenzi. Uanzishwaji wa Mfuko huu utakapokamilika utaongeza kwa kiasi kikubwa ushindani wa Wakandarasi wa ndani sambamba na fursa za ajira hasa kwa Vijana wanaohitimu katika fani ya Uhndisi.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali pia inatekeleza Mradi wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (*Small Entrepreneurs Loan Facility - SELF*) unaosimamiwa na Wizara ya Fedha kwa madhumuni ya kuwawezesha Watanzania wakiwemo Vijana kupata mitaji na kuwajengea uwezo wa kushiriki

katika shughuli za uzalishaji mali, kujiongezea kipato na kuondokana na umaskini. Tangu mfuko huu uanzishwe umeshatoa mikopo yenyе thamani ya Shilingi Bilioni 36.6 kwa wajasiliamali 80,372 katika Wilaya 101. Vilevile, Vijana wananaufaika na Miradi na Programu mbalimbali zinazotekelawa na Serikali kama vile Programu ya Maendeleo ya Kilimo (ASDP) na Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Masoko, Kuongeza Thamani ya Mazao na Huduma za Fedha Vijiji (MIVARF). Mifuko mingine ni pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao tayari umewawezesha Wananchi wakiwemo vijana kuongeza fursa za kuongeza kipato kwa kufadhili miradi yenyе thamani ya Shilingi Bilioni 428; Mfuko wa Pembejeo (AGITF) uliota mikopo kwa wakulima na wasambazaji wa pembejeo za kilimo yenyе thamani ya Shilingi Bilioni 49.448; Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*Presidential Trust Fund -PTF*) ambao hadi sasa umetoa mikopo kwa vijana na wanawake yenyе thamani ya Shilingi Bilioni 6.8; Mpango wa Udhagini wa Mikopo kwa Mauzo ya Nje (*Export Credit Guarantee Scheme- ECGS*) uliota dhamana ya mikopo yenyе thamani ya Shilingi Bilioni 47.265 na Mpango wa Kudhamini Miradi Midogo na ya Kati (*Small and Medium Enterprises Credit Guarantee Scheme -SME-CGS*) uliodhamini mikopo ya Shilingi Bilioni 6.505. Mifuko yote niliyoitaja kwa pamoja ilio mikopo na dhamana zenye jumla ya Shilingi Bilioni 690.5. Hata hivyo, jitihada hizi za Serikali zimetawanyika kwenye Wizara na Taasisi mbalimbali, kwa hiyo hoja ya Mheshimiwa Kigwangala inatukumbusha umuhimu wa kuimarisha uratibu wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Nichukue fursa hii kuwahimiza Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwahamasisha Vijana kujenga utamaduni wa kushiriki kikamilifu kwa kujituma zaidi

na kuchangamkia fursa zitokanazo na Miradi, Programu na Mifuko hii.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, nashindwa kukubaliana na Mtoa Hoja kuhusu kuanzishwa kwa Mfuko mwingine maalum kwa vijana kwa kuzingatia Mifuko mingi ambayo tayari imeanzishwa na Serikali kama nilivyoeleza kwenye mchango wangu. Siamini kwamba hoja ya Mheshimiwa Kigwangala kwamba uanzishwe mfuko utakaoitwa *Tanzania Youth Enterprises Challenge Fund* kwa ajili ya kutoa mikopo ya Uwekezaji kwa vijana wa Tanzania ambao Maandiko ya Miradi yao itashinda; itakuwa ufumbuzi wa changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana. Ninaamini kwamba kwa kuimarisha Mifuko iliyopo; kwa kuipatia rasilimali fedha za kutosha na kusimamia utendaji wake ipasavyo tutakuwa tumewatendea haki Vijana wa Taifa letu. Aidha, hoja ya kushindanisha Maandiko ya Miradi ya Vijana tayari inatekelezwa na Serikali kupitia Miradi wa Kukuza Ushindani wa Sekta Binafsi (*Private Sector Competitiveness Project - PSCP*), chini ya Mpango wa Fanikiwa Kibiashara (*Business Development Gateway - BDG*), Mpango wa Ruzuku ya Kuchangia (*Matching Grants*) na Programu ya Kukuza Ushindani wa Kongano (*Cluster Competitiveness Program*). Kupitia Miradi hii, inayotekelizwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania; michanganuo ya miradi ilishindanishwa, na washindi wa miradi iliyokidhi vigezo vya kitaalam, wakiwemo vijana, walipewa ruzuku ya mbegu mtaji kwa ajili ya kuanzisha au kuendeleza miradi hiyo. Kwa ujumla miradi yote inayotekelizwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ina thamani ya takriban Shilingi Bilioni 75.

Vilevile, Serikali kuitia Taasisi zake ambazo ni Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inashirikiana na Taasisi za Sekta Binafsi kama vile Benki ya CRDB na Kampuni ya *Ernest and Young* kushindanisha Maandiko ya Biashara ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu mbalimbali vya hapa Nchini. Tathmini ya Maandiko hayo inafanywa na Wataalam Waliobobe (Peer Group) na kupata washindi ambao Maandiko yao yamekidhi vigezo vilivyowekwa. Tayari shindano hilo linalojulikana kama ***University Entrepreneurship Challenge*** limefanyika mwaka wa 2011 na 2012 na washindi kupatikana. Washindi hao sio tu kwamba hupatiwa zawadi, bali pia huunganishwa na Taasisi za Fedha ili waweze kupata mikopo kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ambayo hutoa fursa za kujajiri na kuajiri vijana wengine. Kinachotakiwa ni kuimarisha Mpango huu ili uwafikie vijana wengi zaidi kuliko kuanzisha Mpango mpya.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Vijana wengi wanaohitimu mashuleni na vyuoni wanashindwa kutimiza masharti ya kukopesheka kwenye Taasisi za fedha kama vile kuwa na mali isiyohamishika. Ninawahimiza vijana kuanzisha na kujiunga na Vikundi vya Uzalishaji Mali, Vyama vya Ushirika, VICOBA na SACCOS ili kukabiliana na changamoto hii; na kuongeza fursa zao za kupata mikopo kutoka kwenye Mifuko na Taasisi za Fedha. Aidha, natoa wito kwa Taasisi za Fedha kuona kwamba wao ni Wadau muhimu wenye jukumu la kuchangia ukuaji wa uchumi kwa kuwawezesha Wananchi Kiuchumi kama njia ya kujihakikishia uendelevu wa biashara zao. Hivyo, ni suala la muhimu kwa Taasisi hizi

kuongeza ubunifu katika kurahisisha taratibu zao za upatikanaji wa mikopo sambamba na kupunguza viwango vya riba. Nimeliagiza Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kukutana na Taasisi za Fedha kwa lengo la kujadili mchango wa Taasisi hizo katika kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Aidha, ninatoa rai kwa Makampuni ya Wawekezaji kwenye sekta mbalimbali kama vile madini, utalii, gesi asilia, mafuta na mawasiliano waone kwamba wana jukumu la msingi la kuchangia jitihada za kuwawezesha vijana kiuchumi. Hii ni kwa kuzingatia kwamba Makampuni yaliyowekeza hapa Nchini yananufaika na rasilimali za Taifa hivyo ni muhimu kwa Makampuni haya kuchangia kwa kuimarisha na kujenga uwezo na ujuzi wa vijana ili nao waone faida za uwekezaji. Wawekezaji wanalo jukumu la kuchangia faida wanayopata ili kuimarisha miundombinu, elimu, afya, kilimo na viwanda. Hivyo, natoa wito kwa Makampuni yaliyowekeza hapa Nchini kutimiza wajibu wao na kuwa na Mpango mahsus wa kutimiza wajibu huo, yaani *Corporate Social Responsibility*. Hali hii itaweka mazingira mazuri yanayolinda maslahi ya pande zote ikiwa ni pamoja na maslahi ya Wawekezaji.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, napenda kuhitimisha mchango wangu kwenye Hoja hii kwa kusositiza kwamba ufumbuzi wa uhakika na endelevu wa changamoto ya ajira kwa vijana ni kuongezeka kwa uwekezaji kwenye sekta zote za uchumi. Ni lazima tuhakikishe kwamba mikataba yote inayohusu uwekezaji inazingatia ipasavyo maslahi mapana ya Taifa ili kuondoa dhana iliyojengeka kwamba wawekezaji wanapora rasilimali za Taifa. Ongezeko la

uwekezaji ndiyo chanzo cha kukua kwa uchumi kwa kasi itakayoendana na ongezeko la nguvu kazi Nchini. Uwekezaji utaongeza fursa za ajira kwa vijana, utapunguzaa umasikini wa kipato, utaongeza mapato ya Serikali, utaongeza mauzo ya bidhaa nje, utaongeza mapato ya fedha za kigeni, na hivyo kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi na kupunguza umasikini Nchini.

Hata hivyo, ili vijana waweze kunufaika na fursa zitokanazo na ongezeko la uwekezaji ni lazima wafanye jitihada za makusudi za kuhakikisha kwamba wanatimiza masharti na vigezo vya kuajiriwa kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira Kikanda na Kimataifa. Hivyo, ni muhimu kwa vijana kujiendezea kulingana na mahitaji ya soko la ajira sambamba na kujenga utamaduni adhimu wa kupenda kufanya kazi kwa bidii na kuheshimu kazi kwa kuzingatia usemi wa wahenga wetu kwamba kazi ni kipimo cha utu. Natoa rai kwa vijana wote wa Tanzania kujiepusha na tabia zitakazopunguza sifa zao za kuajiriwa ikiwa ni pamoja na uvivu, wizi na ulevi. Sambamba na sifa zinazoongeza fursa za vijana wa Tanzania kuajiriwa, natoa rai kwa vijana wote kujijengea utamaduni wa kulipa madeni na nidhamu katika matumizi ya fedha ili waweze kuongeza sifa zao za kukopesheka. Aidha, nitoe rai kwa Wazazi na Jamii kwa ujumla kutambua umuhimu wa maadili haya na kuhakikisha kwamba kila mmoja wetu anatimiza wajibu wake wa kuimarisha maadili haya katika Jamii ya Tanzania na kukemea yale yanayotuletea sifa mbaya kama Taifa.

Napenda kusisitiza kwamba kote duniani, Mataifa yanashindana kuvutia mitaji kwenye Nchi zao, kwa kuweka mazingira yanayovutia wawekezaji na yanayotabirika ili

kujenga imani mionganini mwa jumuiya ya wawekezaji. Wawekezaji hawatachagua kuweka mitaji yao kwenye Nchi ambayo kila kukicha ni maandamano na vurugu kwa vile amani na usalama ni kigezo muhimu katika kuvutia uwekezaji. Natoa wito kwa kila mmoja wetu kuacha tabia inayozidi kuongezeka ya kushabikifa maandamano na vurugu kwani hazina tija kwa Taifa.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Napenda kuchukua fursa hii kuwahakikisha Vijana wote wa Tanzania kwamba kamwe Serikali haiwezi kuwapuuza. Serikali itaendelea kuthamini, kujali na kulinda maslahi ya Vijana kwa vile tunatambua umuhimu wa vijana katika uhai wa Taifa letu na kwamba mchango wa vijana katika uchumi wa Nchi yetu ni mkubwa.